ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.

14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae

30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni

53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nne – Tarehe 21 Januari, 2013

Kikao kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Juma

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, napenda kuwasilisha Mezani mapendekezo ya Rasimu ya Mswada wa Sheria ya kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar, Kazi, Uwezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo 2012.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Salma Mussa Bilali (Mjumbe): (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi…

(Umeme ulikuwa unaleta matatizo ya kuzimika zimika)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe inaonekana kwamba umeme haukutulia. Naomba radhi sana kutokana na matokeo hayo. Nafikiria sasa imewezekana itakuwa mambo yapo mazuri. Mhe. Salma Bilali karibu.

(Mhe. Salma Mussa Bilali) (Kny Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, naomba Kuwasilisha Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar, Kazi na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 41

Uboreshaji wa Soko la Kinyasini

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Soko la Kinyasini lililoko Wilaya ya Kaskazini "A" kwa hivi sasa limeonekana ni Soko muhimu na ni kimbilio la wafanyabiashara wa sehemu tofauti katika Mikoa yote ya Unguja, lakini soko hili bado linakabiliwa na matatizo mengi katika kuhudumia idadi kubwa ya wafanyabiashara na wananchi wanaofika hapo kila siku kuuza na kutafuta huduma mbali mbali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" kuboresha huduma zitolewazo hapo hasa miundombinu na huduma muhimu zikiwemo maji, vyoo na kuweka sakafu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 41 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kukubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba Soko la Kinyasini ni muhimu na mbali ya kuhudumia Mkoa wa Kaskazini lakini hata Mkoa wa Mjini Magharib na Mkoa wa Kusini Unguja wanakwenda kupata huduma zao katika soko lile.
Vile vile naomba nikubaliane nae kwamba kuna changamoto za kihuduma ambazo zinalikabili soko lile.

Mhe. Spika, hata hivyo serikali ina mipango thabit ya kuliendeleza Soko hilo kutokana na umuhimu wake huo nilioutaja. Hadi sasa Serikali inaendelea na juhudi zake za kutafuta namna ya kuliendeleza soko hilo ambapo kwa mwaka jana Serikali ya Mkoa wa Kaskazini, kupitia Wilaya pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kasikazini "A" kwa pamoja zilipendekeza fedha za mradi wa MIVARF huu ni mradi kupitia Wizara ya Kilimo kwa upande wa Wilaya ya Kaskazini "A" usaidie ujenzi wa soko hili. Kwa bahati mbaya soko hilo halikubahatika kujengwa kupitia mradi huo.

Baada ya matokeo hayo Mhe. Spika, serikali iliendelea na juhudi zake za azma ya kuliendeleza soko hilo. Katika hatua iliyofuata serikali kupitia Halmashauri ya Kaskazini "A" imeanza mazungumzo na wenzetu wa ZSSF, kwa kuona namna gani soko hilo tutaweza kuliendeleza kwa maslahi ya wananchi na watumiaji wa soko hilo. Aidha ziara ya kulikagua soko hilo ilifanyika tarehe 29/11/2011 ambapo iliwashirikisha Maafisa na maafisa kutoka ZSSF.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa makubaliano yaliyotokana na ziara hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" imeshauriwa kutafuta hati miliki ya ardhi ya soko hilo na kuandika *project proposal* na kuiwasilisha ZSSF kwa hatua zitakazofuata. Aidha hatua za kuandika *project* tayari zimeshaanza na katika hatua za awali Halmashauri tayari imeshaandaa mchoro wa soko hilo.

Kazi ya kufatilia hati miliki ya ardhi nayo pia Mhe. Spika, imeshaanza. Imani yetu kwamba ujenzi wa soko jipya utakapokamilika utaondoa matatizo ambayo Mheshimiwa aliyoyazungumza ya vyoo, maji pamoja na kutokuwepo na sakafu. Ahsante.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwa sasa mvua za masika zinakaribia na soko lile kama nilivyoeleza katika swali la msingi kwamba ni soko moja muhimu sana na pana mkusanyiko mkubwa sana wa watu. Je, Mhe. Waziri huoni kama kuna umuhimu wa kufanya haraka ili kusaidia angalau choo tu wananchi wetu pale waweze kufaidika na huduma hiyo na kuepukana na maradhi ya kipindupindu ambayo kwa mwaka jana yaliwahi kutokezea katika soko lile.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi umuhimu wa vyoo katika masoko yetu. Nimuhakikishie tu mimi nimefanya ziara mwenyewe sokoni pale na vipo vyoo viwili vile vilivyojengwa zamani na Wizara ya Afya, vimeenea vile Unguja nzima na pale vipo. Lakini kutokana na idadi ya watu waliokuepo pale kwa kweli ni lazima nikiri kwamba choo kimoja hakitoshi. Kwa hiyo nakubaliana na wazo lake tutajitahidi kuongeza huduma za vyoo haraka iwezekanavyo kabla ya huo ujenzi mkubwa wa soko jipya. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na Waziri kukiri kuwa soko la Kinyasini linakabiliwa na matatizo, lakini imekuwa ni kawaida kwa Mawaziri pamoja na Waziri kukiri lakini utekelezaji wake hauonekani katika Baraza hili tokea kuingia mimi. Iliwahi kutoka kauli kama hiyo kuhusu Soko Kuu la Darajani kuhusu kuchanjwa samaki chini. Je, ahadi hiyo mmeitekeleza vipi Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, sisi ni waungwana na sisi ni wasimamizi, sasa kama hali ipo kweli tusikiri? Ni lazima tukubali ukweli. Jukumu letu baada ya kukiri hali ya mapungufu tuifanyie kazi na huo ndio wajibu wetu. Wewe kama Mhe. Mwakilishi usione tabu kutuzindua kwa sababu mimi si mtendaji na wewe ndio mwenye jimbo, unapita kama Mhe. Ussi Jecha Simai, yeye ndiyo yupo jimboni, kaona mapungufu yale, sasa mimi siwezi kusema kama pale kuna vyoo 20 Kinyasini na hali yakuwa kuna vyoo viwili. Lazima ukiri kwamba kweli hali ipo na kuna mapungufu na tunayachukua, tunayakabili na tunayafanyia kazi.

Sasa umezungumza Marikiti Kuu, pale vyoo vipo, lakini tizama idadi ya watu waliokuwepo vinatosha? Lakini pia pale watu waliokuwepo nao wote wameruhusika kuuza sokoni pale. Wapo watu wengi wapo nje ya soko ambao hawaruhusiwi na wewe Mheshimiwa kama Mwakilishi utusaidie wale wasiokuwa na leseni wanapanga vitu barabarani, waondoke, ili tujue huduma ya vyoo vilivyokuwepo viwatoshe waliokuwepo ndani. Ahsante.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, umechukua hatua gani ya kutokudhibiti watu kutokupanga vitu katika barabara kama ilivyo katika Soko la Mwanakwerekwe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa kweli soko lile la kinyasini ni soko jipya lilikuwa ndani pale pale Kinyasini na nimetaarifiwa hapo kabla kunako mwaka wa 2005 lilihama pale lilipokuwepo likahamia lilipo hivi sasa. Cha kufurahisha wale watumiaji wa soko wote kwa kweli au wauzaji wanafuata taratibu tulizokuwanazo za kutokupanga vitu pembezoni mwa barabara, jambo ambalo linakera sana kabisa.

Mimi ningewaomba sana ndugu zangu wanaopanga vitu katika masoko ya Mwanakwerekwe na soko hata la Darajani kuacha mtindo huo kwa kweli inakera, inatutia aibu ni fedheha, soko lipo ndani lakini wao wanaacha soko wanapanga vitu barabarani. Wewe hata kama unataka kupaki gari yako unapata tabu, lakini pia ni uchafu, Waziri wa Afya anakemea sana mambo haya.

Kwa hiyo kwa kweli nakuunga mkono sana Mhe. Shadya sote kama ni Wawakilishi kidogo tupige vita mambo haya. Maana sisi tunaweza kutumia nguvu lakini haina haja, twende pale halafu tutumia askari, tuwaondo, ni vyema tutumie elimu, tuwaelimishe watu wetu, wafahamu kwamba haipendezi kupanga vitu pembezoni mwa barabara. Kwa hivyo mimi nawapongeza sana watu wa Soko la Kinyasini wote wapo ndani na wanatii amri ya Halmashauri na vitu wanapanga ndani kwa utaratibu unaopendeza kabisa. Na ni mfano na inafaa wengine tukaiga mfano ule kule. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 27

Wananchi Kususia Zoezi la Sensa

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Wakati wa zoezi la sensa na Makaazi lililoanza Agosti 26, 2012 nchini kote, baadhi ya wananchi waliamua kususia zoezi hilo kwa madai mbali mbali ikiwemo kunyimwa kwa haki zao za msingi, ikiwemo vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, vyeti vya kuzaliwa n.k.

(a) Je, Serikali yetu imeingia hasara kiasi gani cha fedha na imejifunza nini kutokana na uamuzi wa wanachi.

(b) Je, ni sheria gani iliyovunjwa na wananchi na je, sheria hiyo ilipitishwa au kuridhiwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

(c) Iwapo sheria ipo na inafanyakazi ni kwanini vyombo vya Dola vikaamua kuwapiga na kuwasumbua wananchi badala ya sheria kuchukua mkondo wake.

Mhe. Waziri Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakilishi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, tarehe 26 Agosti, mwaka 2012, serikali iliendesha zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi kwa nchi nzima. Wakati zoezi hilo likiendelea baadhi ya wananchi walisusia zoezi hilo kwa madai mbali mbali. Kitendo cha baadhi ya wananchi kususia Sensa kilisababisha gharama kubwa zaidi katika kuendelea kuelimisha na kuhamasisha umma kukubali zoezi hili muhimu kwa maendeleo ya taifa letu, hasa pale serikali ilipoongeza wiki moja zaidi kwa ajili ya kuendelea na kazi ya kuhesabu watu.

Mhe. Spika, sio rahisi kupata tathmini ya fedha zilizotumika kugharamia zoezi la ziada zilizofanywa na makundi ya watu mbali mbali waliohamasisha na kuelimisha wananchi washiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi baada ya kugomea kuhesabiwa kwa wiki ya kwanza. Aidha tulichojifunza kwa upande wa serikali kutokana na kadhia hii ni kuwa linapotokea jambo kubwa kama hili ni kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wetu.

(b) Mhe. Spika, sheria iliyovyunjwa na wananchi ni Sheria ya Takwimu ya Zanzibar ya Namba 9 ya mwaka 2007, sehemu ya Tano kifungu cha 14 (2) na (3) na sheria hii ilipitishwa na Baraza la Wawakilishi.

(c) Mhe. Spika, haina taarifa kuwa wananchi waliosusia Sensa walipigwa na kusumbuliwa na vyombo vya dola. Na hakuna mwananchi waliyewasilisha madai ya aina hii katika chombo chochote cha kisheria hapa Zanzibar. Kinyume chake ni baadhi ya wananchi waliosusia zoezi hili ndio waliofanya fujo ikiwa ni pamoja:

(1) Kuwapiga, kuwakejeli,
(2) Kuwatukana makarani wa Sensa pamoja na kuwanyang'anya vifaa vya Sensa walivyokuwa wakivitumia
(3) Kuyaharibu Magari ya Serikali na
(4) Kuvuruga amani na usalama wa wananchi wenzao katika baadhi ya maeneo.

Mhe. Spika, katika muda wote huu serikali ilichukua busara na hekma kubwa na ilijiepusha na vitendo vya kutumia nguvu na iliunda tume ya viongozi kama vile Masheha, viongozi wa dini na watu mashuhuri kwa lengo la kuwaelimisha zaidi wananchi badala ya kuchukua hatua za kisheria.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali la nyongeza lenvye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba haikuwa rahisi kwa serikali kujua gharama zilizopatikana baada ya kuongezeka kwa siku kutokana na tukio la wananchi. Lakini kwa sababu fedha imetumika na ni fedha ya walipa kodi je, Mhe. Waziri haoni kwamba kwa sababu serikali haikuwa makini na kuwatayari kurikodi na kufanya uratibu wa fedha, si mwanya wa wajanja wachache kula fedha za umma kwa kisingizio kwamba wananchi walikataa kuhesabiwa.

(b) Kwa kuwa Sensa ni jambo la Muungano naomba Mhe. Waziri anisaidie yeye kama Waziri ana Wizara yake na alishirikishwa vipi tangu kupanga na kutumia fedha za umma.

Je, Tanzania tulitumia shilingi ngapi kwa suala hili la Sensa hasa kwa vile Wazanzibari ni milioni moja laki tatu ni kiasi gani cha fedha ambayo serikai yetu ilichangia kwenye suala hilo la Sensa.

Mhe. Waziri Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika,

(a) Kwanza kulikuwa kuna gharama ambazo zilitoka moja kwa moja serikalini. Baada ya zoezi hili kuongezewa wiki moja ya ziada kuna watu maarufu kama nilivyosema viongozi wa dini na viongozi maarufu walilazimika kutumwa na serikali kwa kujitolea ili waendelee kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao ili wakubali kuhesabiwa. Gharama zile sio rahisi kuweza kuunganishwa na gharama ambazo zilizotoka serikalini ili kuweza kupata ujumla wake.

Kwa maana hiyo ndio nikasema kwamba haikuwa rahisi katika eneo kama lile la wiki moja kuweza kupata gharama kamilifu. Lakini kile kilichotoka serikalini kwa ajili ya maafisa na makarani kinafahamika, lakini wale viongozi tuliowaomba wafanye kazi hiyo ikiwa ni pamoja na baadhi ya Mawaziri waliombwa kwa wakati wao wa ziada wafanye kazi hiyo kuwahamasisha. Na nataka kuwapongeza sana wale walioifanya kazi hiyo na hatimaye baadhi ya wananchi wetu walikubali kushiriki na kuhesabiwa.

(b) Swali lake pa pili ushirikishwaji wa Zanzibar tokea kupanga hadi kukamilika kwa Sensa yenyewe. Nataka kumuarifu Mhe. Hija na wananchi wote, kwamba Zanzibar imeshirikishwa tokea kupanga mpaka Sensa kukamilika kwake. Kulikuwa kuna Kamati ya Taifa ambayo Mawaziri kutoka Zanzibar na Mawaziri wa Muungano tulikuwa tunakutana ambayo kamati hiyo ilikuwa chini ya Mwenyekiti Waziri Mkuu na Mwenyekiti mwenza Makamo wa Pili wa Rais.

Lakini vile vile kulikuwa kuna kamati za wataalamu, wataalamu wetu wa takwimu na wataalamu wa muungano walikuwa wanakutana. Vile vile tulikuwa tunashirikishwa katika upangaji wa fedha. Fedha ya Sensa yote imetoka katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kama ndiyo yenye mamlaka ya kuendesha Sensa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa lengo la serikali ni kufanikisha kile ambacho kimekusudia. Na kwa kuwa kuna baadhi ya watu ambao hawakuandikisha na kuna baadhi ya watu ambao wameandikisha. Na kwa kuwa tathmini ya fedha si rahisi kupatikana je, tathmini ya idadi ya watu alioandikisha na wale ambao hawakuandikisha ni kiasi gani.

Mhe. Waziri Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, tulifanya tathmini ya kina kwa kushirikiana na Masheha watu wote katika Wilaya zote kumi za Zanzibar kwa upande wetu na kwa upande wa Tanzania Bara na wao walifanya hivyo hivyo kaya zilizokataa ambao walikataa kuhesabiwa watu wao takwimu hizo zipo. Lakini kwa utaratibu wa Sensa kulikuwa kuna fomu mbadala, fomu hiyo kwa sababu Sheha alikuwa

anawaelewa watu waliokuwemo katika kaya ile sheha kwa kushikiana na maafisa wetu wa Sensa walilazimika kuandikisha watu waliokuwemo pasi na wao wenyewe kutoa taarifa.

Sheha alikuwa anajua kwamba nyumba hii inakaa fulani na fulani fomu mbadala zilijazwa. Kwa maana hiyo kaya zilizokataa taarifa zake tunazo lakini na idadi ya watu wanaokaa katika kaya ile vile vile kwa kutumia fomu mbadala tuliweza kuzipata. Mhe. Mwakilishi akihitaji hiyo idadi basi nitampatia kwa mujibu wa Wilaya ambazo zimekataa. Wilaya iliyokuwa inaongoza kwa upande wa Kisiwa cha Unguja ilikuwa ni Kaskazini "A" na kwa upande wa Pemba ilikuwa ni Wilaya ya Wete.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako, pamoja na majibu mazuri sana na ya kina ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Ametwambia hapa katika kujibu swali la nyongeza kwamba Masheha kwa bahati nzuri wana taarifa zote za wananchi wanaokaa katika vijiji vyao. Sasa kama hivyo ndivyo hizi gharama za kutafuta makarani zina haja wakati kumbe wangepata maelekezo yote kupitia kwa Sheha.

(b) Mhe. Spika, watu waliogoma Sensa walikuwa wana madai tofauti, lakini miongoni mwa madai hawa hapa Zanzibar walikuwa wana kilio kwamba Masheha wakiwaendea kutafuta huduma kama za kuandikishwa vitambulisho vya Uzanzibari Masheha walikuwa na kauli na ni nyimbo wakiimba kwamba weye miye sikutambui. Sasa wakasema ikiwa Sheha hanitambui wakati wa kitambulisho anakujaje kunitambua wakati wa Sensa. Kwa hivyo wakagoma, sasa kwa kuwa hilo lipo je, serikali inampango gani wa kuwaelekeza masheha wasiwanyime watu haki hii ili hatimaye na watu wasigome katika mpango ya serikali.

Mhe. Waziri Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, Sheha anaelewa taarifa za watu waliokuwemo katika maeneo yake, lakini si kwa ukamilifu, si kwa mujibu wa madodoso ya Sensa yanavyotaka. Sheha anaweza akaelewa nyumba hii anakaa Omar Yussuf Mzee mwanamme, Fatma Ali mwanamke, lakini Sheha sio rahisi kuweza kujua kiwango cha elimu walichonacho wale watu. Sheha sio rahisi kuweza kujua nyumba ile ina vyoo vingapi hizi ndizo ambazo zilizotulazimisha sisi serikali kuwaajiri wakusanyaji wa sensa, makarani ili wakapate taarifa *in detail*. Ili tuweze kujua idadi ya watu wetu na makaazi yao. Kwa hivyo kuna taarifa Sheha hana na kuna taarifa sheha anazo na ndio maana tukasema sensa ya watu na makaazi. Na hili ni zoezi ambalo linafanyika kila baada ya miaka kumi Mhe. Spika, na ni zoezi moja wapo ambalo linatuunganisha watanzania. Kwa hivyo mimi nitawaomba tu ndugu zangu wasisusie sensa, sensa ni zoezi linalotuunganisha watanzania.

Lakini la pili mimi nakubaliana na maelezo ambayo aliyoyasema Mhe. Abdalla kwamba tuendelee kuwaelimisha masheha wetu, kushirikiana na wananchi wao waliomo katika maeneo yao ili pale wanapotaka huduma badala ya kusema hawawatambui, basi nadhani kutumia busara zaidi, kuelimishana zaidi ili hatimae kuwe kuna mustakbali mzuri wa maelewano, baina ya wananchi katika eneo lile na sheha wetu. Zoezi la sensa hata mtu aliyekuwa hatambuliwi anatakiwa kuandikwa madhali amelala ameamkia usiku wa sensa katika eneo lile ndio maana hata wageni wanaandikishwa katika zoezi la sensa halina anayetambuliwa halina asiyetambuliwa huku katika kubagua ndio tunaelewa kwamba huyu ni mgeni, huyu ni raia.

Kwa hivyo mimi naomba tu kwamba tuendelee kushirikiana katika mazoezi kama haya ambayo yanatuunganisha watanzania, yanatuunganisha wazanzibari badala ya kuyasusia.

Nam. 39

Kazi za Tume ya Idara Maalum

Mhe. Ussi Jecha Simai - Aliuliza:-

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Umma No. 2 ya mwaka 2011, katika kifungu cha 104(2) kimefuta vifungu vya 5 na 6 vya Sheria ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum (SMZ) wakati ambapo kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum vifungu hivyo ndivyo vilivyotaja kazi za Tume hiyo. Kama vile:-

- Kupendekeza majina ya watumishi wanaostahiki kupatiwa vyeo vya uafisa kwa mara ya kwanza
- Kufuta mkataba wa Ajira kwa yule aliyeenda kinyume na Sheria za Utumishi za Idara Maalum
- Kupanga mishahara na maslahi mengine ya wafanyakazi wa Idara hizo, pamoja na Pension.

(a) Je, hii Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ina kazi gani kuwepo hadi hivi sasa.

(b) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kuendelea kukutana kwa Tume hii ni kuitia hasara Serikali na ni kinyume cha Sheria.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 39 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa, naomba kwa ruhusa yako, nirekebishe kidogo jina la Sheria iliyonakiliwa kwenye suala hili. Sheria hii inaitwa Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011, na sio "Sheria ya Tume ya Utumishi wa Umma**"** kama ilivyoelezwa katika suali lake Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, pili, nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011, kifungu cha 104(2) kimefuta vifungu vya 5 na 6 vya Sheria Namba 6 ya mwaka 2007 ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu suali lake Nam. 39 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, pamoja na kwamba vifungu vilivyotajwa hapo juu vimefutwa, hatua hiyo imechukuliwa ili kuleta uwiano wa Miundo na Kazi za Tume zote za Utumishi katika Utumishi wa Umma. Sheria mpya ya Utumishi wa Umma, imefafanua na kuweka wazi

Muundo, Majukumu na Uwezo wa Tume zote za Utumishi ikiwemo Tume ya Utumishi Idara Maalum, katika vifungu vya 33(d), 34(4) na kifungu cha 36(1) hadi 36(7). Kwa hivyo vifungu vya 5 na 6 vilivyofutwa katika sheria ya Tume ya Idara Maalum vimeelezwa na kufafanuliwa kwa kina ndani ya vifungu nilivyovitaja hapo juu, hususan vifungu vya 36(1), (2), (3) na (6).

(b) Mhe. Spika, kutokana na maelezo niliyoyatoa katika kifungu (a) hapo juu, ni dhahiri kwamba Tume ya Utumishi ya Idara Maalum bado inahitajika na kwamba ina majukumu ya kutosha katika eneo lake. Kwa hivyo, dhana ya kwamba kuendelea kukutana kwa Tume hii ni kuitia hasara Serikali si sahihi hata kidogo, hasa kwa vile Tume ya Utumishi ya Idara Maalum inakutana na kufanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria na sio kinyume cha Sheria.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, kwa mujibu wa swali la msingi alililiuliza Mhe. Mjumbe juu ya vifungu vilivyofutwa na kutolewa maelekezo katika maeneo mengine, ambayo ni dhahiri inaonekana ndio msingi wa kuanzisha Tume ya Utumishi wa Idara Maalum na kuwa sheria hii tayari imetungwa na chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi na ni wajibu wetu kufanya hivyo. Lakini sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011 imeonekana ina mapungufu mengi. Je, Mhe. Waziri haoni iko haja sasa sheria hii iweze kupitiwa upya ili kuondosha dosari nyingi ambazo zinaonekana zipo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali langu mama linahusu sheria au vifungu vya Tume ya Utumishi Idara Maalum, vifungu hivyo vimefafanuliwa vizuri zaidi katika sheria ya Utumishi wa Umma kifungu namba 36 mpaka 36(7) ya Tume ya Utumishi ya Umma. Kwa hivyo kazi zile ambazo zimekuwa zimeelezwa kwenye Tume ya Idara Maalum sasa zimefafanuliwa vizuri kwenye sheria ya Utumishi wa Umma. Hata hivyo ni utaratibu wa kutunga sheria pale inapoonekana kuna mapungufu ya utekelezaji wa sheria, sheria hii kufanyiwa marekebisho kama sheria nyengine zinazofanyiwa marekebisho.

Itakumbukwa ni kipindi kifupi nyuma sheria hii hii tumeifanyia marekebisho ndani ya Baraza hili kwa kuona kwamba kulikuwa kuna vifungu ambavyo vina utata. Sasa kama ikithibitika kwamba ufafanuzi uliotolewa kwenye sheria hii unaohusu vifungu vilivyofutwa vya Idara Maalum hilo ni jambo la kawaida kwa serikali kuleta marekebisho ya sheria ndani ya Baraza lako.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ninakushukuru Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri, fasaha ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, katika maeneo ya kazi ambayo yalitajwa katika sheria hizi za zamani zilizoanzisha Tume ya Utumishi za sekta mbali mbali katika utumishi wa umma, na hata katika sheria hii mpya namba 2 ya mwaka 2011 Mhe. Waziri ameinukuu vizuri ilipoweza kuweka uwiano bado imeweka jukumu la kupendekeza au kupanga mishahara na maslahi mengine ya wafanyakazi sio tu Idara Maalum lakini hata katika sekta nyengine katika Tume ya Utumishi ya ile sekta inayohusika. Lakini katika utekelezaji wa sheria yenyewe namba 2 ya mwaka 2011 na katika uhalisia bado kuna malalamiko mengi sana kwamba Tume hizi za Utumishi za sekta zimeachwa zikiwa hazifanyi kazi na badala yake kazi hii mara

nyingi imekuwa ikifanywa na Wizara ya Utumishi wa Umma na sio hata na Tume au Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Sasa kama ni hivyo Waziri haoni kwamba kuna haja ikiwa serikali imeamua kuondosha jukumu hili kwa Tume za Utumishi za sekta ikaifanyia marekebisho sheria hii ili kuondosha jukumu hili ikajulikana tu kwamba ni wizara inayopanga mishahara, marupurupu na maslahi mengine ya wafanyakazi katika sekta zote. Hiyo (a) Mhe. Spika.

Lakini (b) katika hiyo hiyo Tume ya Utumishi ya Idara Maalum pamoja na kupewa jukumu hili bado kumekuwa na malalamiko yasiyokwisha kwamba watumishi katika sekta hii ya Idara Maalum, wamekuwa mara nyingi wanakatwa mikato mbali mbali katika mishahara yao na kufanyishwa michango mingi na pamoja ahadi nyingi za serikali kusemwa ndani ya Baraza hili na kutoa uhakikisho kwamba mambo haya yatarekebishwa lakini bado ukifatilia unakuta malalamiko kutoka kwa watumishi wa sekta hii yapo pale pale. Ni hatua gani Wizara inachukua ili kuona kwamba mambo haya yanayofanywa na wakuu wa vikosi yanakomeshwa ili wafanyakazi wote wa sekta ya utumishi wa umma waweze kupata haki zao za mishahara kwa mujibu wa mikataba yao na kwa mujibu wa utumishi ambao wanaifanyia nchi hii. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza nataka nimthibitishie kwamba kazi ya kupendekeza inafanywa na Tume za Utumishi mbali mbali ambazo zipo kwa mujibu wa sheria. Suala la maslahi la watumishi wao, suala la kuwapandisha vyeo, na mambo mengine bado kazi hii kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma ni kazi ya Tume kupendekeza, suala la serikali kwa maana ya wizara, wizara haifanyi kazi ya Tume za Utumishi, bali inafanya kazi ya serikali hasa pale tunapokuja kwenye maslahi kwa maana ya kuoanisha kama nilivyosema kwanza sheria hii ya Utumishi wa Umma au imetungwa kwa madhumuni ya kuoanisha watumishi wote wa umma kuwa na uwiano sawa wa mambo mbali mbali yanayowahusu kiutumishi.

Kwa hivyo pale wizara yangu inaposimamia será, wizara yangu kazi yake ni kusimamia utekelezaji wa hii sheria. Lakini majukumu ya kupendekeza kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma ni majukumu ya Tume za Utumishi mbali mbali ambazo zipo kwa mujibu wa sheria.

Swali (b) kukatwa mishahara kwa watumishi wa Idara Maalum, ni kweli jambo hili limekuwa likijitokeza, kuuliziwa maswali mbali mbali katika Baraza lako tukufu. Na serikali kazi yake kutoa maelezo au maelekezo kwa Tume husika na wafanyakazi husika kupeleka malalamiko yao ili yaweze kushughulikiwa.

Jambo hili tunaweza tukaulizwa ndani ya Baraza la Wawakilishi. Lakini kama tunavyojua katika Idara Maalum, katika vikosi kuna kanuni na taratibu zao za kufanya kazi na kanuni zao za nidhamu, kanuni zao za uendeshaji. Kwa pale askari yoyote anapohisi anakatwa fedha kinyume na utaratibu ni wajibu wake kupeleka malalamiko yake ndani ya Tume ya Idara Maalum. Tume ya Idara Maalum ikeshalishughulikia hilo jambo itatoa taarifa, kama mtumishi yule hakuridhika anakata rufaa Kamisheni ya utumishi wa umma.

Kwa mara ya mwisho hili jambo limeletwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma moja kwa moja tukasema si utaratibu, utaratibu watumishi wanatakiwa kwanza waanzie kwenye Tume yao ya Utumishi kupeleka malalamiko yao na halafu yaweze kushughulikiwa. Lakini pamoja na hayo yote serikali haiwezi kukubaliana na utaratibu wa kukatwa watumishi fedha zao kinyume na utaratibu na kanuni ambazo wameweka wao wenyewe ndani ya vikosi vya SMZ.

Nam. 32

Uhuru wa Kutoa Maoni

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Duniani kote, Kanuni, Sheria na Katiba zimetambua kuwa uhuru wa kutoa maoni ni haki ya msingi ya Binaadamu na Umoja wa Mataifa umepitisha Maazimio maalum kusudi kusisitiza uhuru huo. Aidha katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Mpya Tanzania iliyopitishwa na Bunge mapema 2012, imetamka wazi kuwa ni kosa la jinai kumzuia mtu kutoa maoni yake kwa mujibu wa Sheria katika mchakato huo wa kupata maoni juu ya Katiba mpya. Hata hivyo wapo viongozi wanaothubutu kuwazuia, kuwatisha na kuwabughudhi wale wanaotoa maoni yao kwa vile wanavyoona wao kuwa nafasi juu ya upatikanaji wa Katiba na Mfumo wa Muungano.

(a) Kwa kuwa Sheria hii ya Bunge ipo wazi, kwa nini wanaokiuka hadharani hawachukuliwi hatua.

(b) Kuingilia uhuru wa maoni ya mtu mwingine si kuvunja Katiba na kukiuka maazimio ya Umoja wa Mataifa ambapo Tanzania imeridhia.

(c) Kwa utaratibu huu, Zanzibar na Tanzania kwa ujumla haioni kuwa inajenga tabaka la watu na viongozi walio juu ya Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 32 kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Zanzibar kama zilivyo nchi nyingi duniani inaheshimu haki za binaadamu na ndio maana sura ya tatu ya Katiba inaelezea kinga za haki za lazima, wajibu na uhuru wa mtu binafsi.

Kifungu cha 12 cha Katiba kimeweka masharti ya usawa mbele ya Sheria na kwamba watu wote ni sawa mbele ya Sheria, na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya Sheria. Lakini ni wajibu pia wa kila raia anaposoma Katiba hususan kifungu cha 12 basi ni vizuri sana akasoma kwa pamoja na kifungu cha 24 cha Katiba hiyo hiyo ambacho kinaweka mipaka ya uhuru wa mtu kutomkera au kumbughudhi mwengine na kwamba bado akiona kuwa haki zake zimevunjwa, basi mwananchi huyo atumie kifungu cha 25(a) cha Katiba kutafuta haki yake Mahkamani.

Kifungu cha 25(a) kinasema kwamba kinasema kwamba, mtu yoyote anaweza kufungua shauri katika Mahkama Kuu iwapo ataona kwamba katiba hii imevunjwa au inavunjwa au inaelekea

kuvunjwa na kifungu hiki ni sawa sawa na kifungu cha 30 (3) cha katiba ya Jamhuri ya Tanzania. Bahati mbaya watu wetu hawataki au hawapendi kutumia vifungu hivi kwa kutumia haki zao.

Serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha taasisi za utoaji haki ili kuhakikisha Sheria zinafuatwa na hatua zinachukuliwa baada ya kukamilika kwa taratibu zote kwa wanaovunja Sheria hizo.

Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar inaeleza kuwa watu wote ni sawa mbele ya Sheria. Serikali na viongozi wote kwa ujumla wanaheshimu na kufuata masharti ya Katiba na hivyo sio sahihi kwamba kunajengwa tabaka la watu na viongozi walio juu ya Sheria.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali langu la msingi amekubaliana na matakwa ya katiba na kanuni kama alivyoeleza kwamba ni haki ya kila mwananchi kutoa maoni yake kwa mujibu wa katiba. Lakini ni kinyume na hali halisi katika mikono na hali halisi katika wananchi wetu, kwamba wapo wananchi wanaonyimwa haki hii ya kutoa maoni na wakati mwengine hubughudhiwa. Kwa kuwa Mhe. Waziri amebainisha hilo kwamba ni haki ya kila mtu kwenye katiba, na kwa kuwa kuna wananchi wengine hunyimwa haki yao hiyo,

(a) Naomba Mhe. Waziri anieleze nini kauli ya serikali ya kuwachukulia hatua wale wote ambao wanaowanyima fursa wananchi wengine.

(b) Imekuwa ni mazoea kwa wizara zetu au serikali yetu kuchukua hatua haraka sana kwa kesi ndogo ndogo zinazowakumba wananchi, kama vile wizi wa ndizi, wizi wa nazi na hata uvutaji pengine wa sigara. Lakini pengine ni jambo adimu sana kuchukuliwa hatua kwa haraka kwa makosa ya jinai kama mauaji, ubakaji, dawa za kulevya na mambo mengine. Ni kwa nini wizara yake inashindwa kuchukua hatua kwa mambo ya msingi ya jinai kwa haraka na ikachukua hatua haraka sana kwa mambo madogo madogo kama ya wizi wa ndizi na nazi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nilisema kwamba Katiba inaruhusu haki hizi kwa mtu yoyote yule lakini unaposoma kifungu cha 12 ni vizuri kusoma kifungu 24 kwa sababu kifungu cha 12 kinatoa lakini kifungu cha 24 kinatoa haki ya mipaka ile, kwa hivyo huwezi ukawa na uhuru wa kufanya kila unalolitaka kwa misingi ya kumkera mtu mwengine au kumuudhi mtu mwengine. Hicho kifungu cha 24 kimesema hivyo kwamba kuna mipaka ambayo lazima uende nayo, ukivuka mipaka hiyo kwa hivyo unakwenda kinyume na katiba na unakwenda kinyume na sheria. La kwanza.

Lakini la pili, kesi hizi ambazo alizitaja kuna kesi ndogo ndogo kwa mfano wizi wa nazi na mambo kama hayo na kuna kesi kubwa kubwa za mauaji na ubakaji. Ni kweli kesi ndogo ndogo zinakwenda haraka haraka lakini kesi kubwa kubwa kama ubakaji na uuaji zinachukua muda na huu ndio utaratibu. Kwa mfano kesi ya ubakaji lazima upate mashahidi kama unavyotaka mashahidi kesi ya nazi. Lakini mashahidi wa ubakaji jamii yetu tunaijua, mzee aliyeona kitendo kile akiambiwa aende akae shahidi hataki na haya ndiyo matatizo tunayoyapata. Wazee na jamii hawataki kukaa ushahidi kwa kesi kama hizi. Kesi ya mauaji mtu akiambiwa akakae ushahidi

hataki na ndio matatizo. Sasa hii ndio moja katika sababu ambazo kesi kama hizi zinachelewa sana.

Mimi ninawaomba wananchi kwa ujumla kwamba pale ambapo kesi hizi zinatokea wawe mstari wa mbele kutoa ushahidi ili wahalifu waweze kuhukumiwa haraka haraka.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, ninakushukuru kunipa nafasi hii nikamuuliza swahiba wangu Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mhe. Hija wa Kiwani, alielezea kwamba kutumia kifungu cha 12 katika kutumia uhuru wa kutoa maoni lakini vile vile alikuwa mtu anatakiwa azingatie kifungu 24 kama sikosei kama alivyosema ili kuwa na mipaka. Sasa swali langu liko hapa, katika kutoa maoni ya Katiba ina maana mwananchi alikuwa katika kutoa maoni kwa vile anavyohisi yeye ilikuwa kuna mipaka ya aina gani ya kumzuia yale maoni anayotaka yeye asitoe kama mwananchi wa kawaida. Kwa kutumia hicho kifungu cha 24 kuna mipaka gani katika hii elimu ya Katiba ambayo yeye hakupaswa kusema kitu fulani.

Lakini (b) kama alivyosema Mhe. Hija kuna baadhi ya maeneo yametokezea mambo kama hayo. Je, hatuoni serikali yetu kwamba ile kutotoa elimu kama tulivyoshauri mwanzo kuhusu maandalizi ya mwanzo kuwaandaa wananchi katika kutoa maoni, haoni Mhe. Spika, Mhe. Waziri hii ndio ilisababisha hata watu waliokuwa wanatishwa na wao ikafika kutishika.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza alikuwa anataka kujua ni mipaka gani ambayo mtu anaweza kuifikia katika kutoa maoni. Unapotoa maoni chini ya kifungu cha 12 hasa katika masuala haya ya mchakato wa katiba unaweza ukasema kitu chochote unachokitaka. Lakini mipaka yake usije katika kutoa maoni ukaanza kufanya vurugu, kutaka kumtukana mtu mwengine hiyo itakuwa unakwenda kinyume lakini unaruhusiwa kusema chochote ambacho unahisi kipo. Na kama katika kutoa maoni umekataliwa na sifikirii kama imefanya hivyo na kama umekataliwa ndio unatumia kifungu cha 24 kudai haki yako mahkamani.

Mipaka ya hapa ni kwamba usifanye vurugu ili kuwafanya wenzako wasiweze kutoa maoni ndio mipaka yake lakini si mipaka ya kwamba useme hiki, hiki, hiki usiseme hiyo unaruhusiwa kusema chochote.

Lakini swala la pili hebu kidogo arudie swali la pili.

Mhe. Spika: Hebu rudia swali la pili.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, swali langu (b) lilikuwa kwa kuwa tuliitaka serikali kabla ya kuanza mchakato wa Katiba itoe elimu ya katiba ili wananchi waweze kujua kile wananchi kitakachokujahitajika kuzungumza. Na kutokana na serikali hawakuweza kutoa elimu ya kuwaandaa wananchi, haoni ndio sababu iliyowafanya wananchi wale waliokuwa wakitishwa katika uhuru wao wa kutoa maoni na wao wakafika mahala wakatishika?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, serikali katika swali hili ni *neutral* haitaki ionekane inapendelea upande wowote ule. Na unapoitaka serikali itoe elimu ya Katiba bila shaka elimu hiyo ita-*base* katika mambo fulani fulani, kwa maana hiyo serikali ikasema kwamba isiji-

involve katika masuala haya tuwaachie wananchi wenyewe vikundi vinavyohusika wenyewe na kila mtu awe na uhuru wa kutoa maoni yoyote anayotaka. Na ndio maana kwamba serikali haijajishughulisha na wala haitojishughulisha katika suala zima la kutoa maoni ya Katiba. Huo ni uamuzi wa wananchi wenyewe na serikali itaheshimu maamuzi ya wananchi isingelipenda serikali kuingilia katika suala hili.

Mhe. Spika: Ninafikiri inatosha maana naona hali imekaa vibaya. Mhe. Waziri ninakushukuru.

Waheshimiwa Wajumbe tuna tatizo la umeme, umeme unaotoka kwenye Shirika la Umeme huu ulitangazwa rasmi kwamba unazimwa leo sijui mpaka saa ngapi na kwa bahati mbaya jenereta letu kubwa limetuletea matatizo limewaka kidogo lakini baadae likazimika, hili tunalotumia ni jenereta dogo ambalo halina uwezo wa kuendesha viyoyozi ndani ya ukumbi huu. Sasa hali ya hewa haivutii kuweza kuendelea na shughuli zetu na wamejaribu hata kupunguza taa lakini naona bado haijasaidia. Nadhani hii hali hata kiafya haipendezi kuendelea na kazi humu ndani, sijapata taarifa mpaka saa ngapi jenereta kubwa litakuwa linafanya kazi, sasa ninafikiri ipo haja kwa dharura hii humu ndani tuondoke na tukafanye shughuli nyengine.

Lakini kwa kuwa kuna shughuli inayoendelea hivi sasa niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe nafasi hii ambayo tunaakhirisha shughuli kwa kipindi hiki mpaka jioni nadhani itatosha kuona kwamba wanarekebisha mambo yote tuje tufanye kazi kwa wasaa mzuri zaidi. Nimepewa taarifa kwamba Waheshimiwa Wajumbe wote tunaarifiwa kwamba zoezi la uandikishaji kwa ajili ya vitambulisho vya taifa NIDA linaendelea katika chumba cha Kamati namba 2 na chumba cha kusomea hapo juu. Hivyo Waheshimiwa wote mnaombwa kufika kuanzia sasa kwa utaratibu maalum ili tuweze kujiandikisha kwa ajili hiyo.

Wale Waheshimiwa ambao washachukuliwa taarifa zao lakini bado hawajapiga picha nao pia wanaombwa waende kwa ajili ya kukamilisha zoezi la kupiga picha. Lakini kwa wale ambao taarifa zilikwishachukuliwa na wamekamilisha mambo yote hayo itakuwa hakuna haja. Kwa hivyo tunaombwa sana Waheshimiwa Wajumbe twende pale chumba namba 2 chumba cha kamati na pia chumba cha kusomea pale juu ili kuifanya kazi hiyo ya kuandikisha vitambulisho vya kitaifa.

Waheshimiwa Wajumbe kutokana na hali hii ya dharura, naomba sasa nichukue nafasi hii kuakhirisha kikao hiki hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 4.00 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mswada wa Sheria ya Shirika la Meli ya Mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai, uzima na taufiq ya kuwepo hapa jioni hii ya leo.

Kwa ruhusa yako naomba nihudhurishe mbele ya Baraza lako tukufu mapendekezo ya rasimu ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar, Kazi, Uwezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo ya mwaka 2012.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mbele ya kikao hiki Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar. Kuanzishwa kwa Shirika la Meli Zanzibar chini ya sheria hii mpya inayopendekeza ni miongoni mwa utekelezaji wa Sera ya Usafiri Zanzibar na Mpango Mkuu wa Usafiri mwaka 2008 na kuliwezesha Shirika jipya la Meli kutoa huduma za usafiri zilizo bora na zinazoendana na matakwa ya viwango vya ushindani wa kitaifa na kimataifa. Pia ni miongoni mwa mikakati ya wizara katika kutekeleza maelekezo ya serikali ya kuwa na usafiri wa baharini ulio bora zaidi na endelevu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kutunga sheria ambayo itaanzisha upya Shirika la Meli la Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Shirika lililopo sasa lipo kwa mujibu wa amri ya Rais iliyotolewa mwaka 1988 chini ya sheria ya Mashirika ya Umma Nambari 4 ya mwaka 1978. Sheria hiyo ilifutwa na Sheria ya Mitaji ya Umma Nambari 4 ya mwaka 2002 ambapo Mashirika yote ya Umma yanasimamiwa na sheria hii.

Mswada huu umegawika katika sehemu tano zenye jumla ya vifungu 30. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya awali ambayo jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika katika mswada yameelezwa.

Sehemu ya pili inahusu kuanzishwa kwa shirika, malengo ya shirika na kazi za shirika.

Sehemu ya tatu inaelezea utawala, uongozi wa shirika, masharti kuhusu uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na uteuzi wa Maafisa Waandamizi wa shirika, kuansishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi, uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi na Muundo wa Bodi na Bodi kuwa chombo cha kinidhamu.

Sehemu ya Nne ni masharti ya fedha. Sehemu hii imeeleza mambo mbali mbali kuhusu fedha na rasilimali za shirika, matumizi na bajeti ya shirika na mahesabu na ukaguzi wa mahesabu ya shirika. Uwekezaji wa shirika na taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa kazi za shirika.

Sehemu ya Tano na ya mwisho ni masharti ya jumla na mambo mengine yanayohusiana na hayo ambayo ni kitabu cha orodha ya viwango kwa huduma zinazotolewa na shirika, kuhaulisha wamiliki wa meli zilizokuwa zikiendeshwa na shirika, masharti yanayohusu umiliki wa meli nyengine, ushikiliaji wa maofisi na mikataba.

Mambo mengine pamoja na makosa na adhabu, kutunga kanuni, kufuta sheria na kubakiwa na baadhi ya vifungu.

Mwisho kumewekwa jadweli linalohusu muda wa Mjumbe wa Bodi na masharti mengine yanayohusiana na utaratibu na mwenendo wa vikao vya bodi.

Mhe. Spika, baada ya kutoa muhtasari huo sasa naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waupokee, waujadili na baadae waupitishe pamoja na marekebisho yatakayokubalika.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Marina Joel Thomas (Kny. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema kiasi kwamba tumemudu kukutana tena katika mwaka mpya wa 2013, kwa lengo la kujadili mambo mbali mbali yenye manufaa kwetu na kwa wananchi wetu kwa ujumla. Hivyo napenda kuchukau fursa hii kuwatakia kheri ya mwaka mpya Wajumbe wote wa Baraza hili na wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Spika, pili napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu mswada wa Sheria ya kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar kazi, uwezo na mambo mengine yanayohusiana nayo

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupa wakati wa kuupitia na kuuchambua Mswada huu.

Mhe. Spika, nitakuwa sikutenda haki ikiwa sitowapongeza Wajumbe wa Kamati ya Mawasilliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri waliyoifanya na hatimae leo hii nawasilisha maoni ya Kamati hii mbele ya Baraza hili

Mhe. Spika, naomba kuwataja Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe
4. Mhe. Subeti Khamis Faki - Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
6. Mhe. Marina Joel Thomas - Mjumbe
7. Ndg. Aziza Wazir Kheir - Katibu
8. Ndg. Maryam Rashid Ali - Katibu

Mhe. Spika, kabla ya kutoa maoni ya kamati naomba kwanza nilipongeze Baraza lako tukufu kwa kufanya marekebisho ya kanuni zake kwa kuingiza kanuni ya 83 (2) ambayo inahusiana na Mswada kusomwa kwa mara ya tatu. Hatua hii imetoa nafasi zaidi kwa Waheshimiwa Wajumbe

wa Baraza hili kupata nafasi ya kuwashirikisha wananchi kutoa maoni na ushauri wao katika miswada mbali mbali inayowasilishwa katika Baraza.

Sambamba na hilo, tunaishukuru Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kutekeleza vyema kanuni ya 83(5) ya kanuni za kudumu za Baraza la wawakilishi. Aidha, kwa kuipatia Kamati hii nafasi ya kuonana na wadau kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi na ufahamu wa mswada husika, kwa mnasaba huo kamati inawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao kwa Kamati hii.

Mhe. Spika, Baada ya Pongezi hizo sasa napenda niende moja kwa moja kwenye mswada husika. Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar umetungwa kwa madhumuni ya kuanzisha upya kwa Shirika la Meli Zanzibar ili kutekeleza Sera ya Usafiri Zanzibar na Mpango Mkuu wa usafiri 2008 na kuliwezesha Shirika jipya la Meli kutoa huduma za usafiri zilizo bora na zinazoendana na matakwa ya viwango vya ushindani wa kitaifa na kimataifa. Pia ni miongoni mwa mikakati ya wizara katika kutekeleza maelekezo ya serikali ya kuwa na usafiri wa bahari ulio bora zaidi na endelevu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati yetu imeridhishwa na azma ya serikali ya kulianzisha upya shirika la meli na ikiwa miongoni mwa malengo ya Shirika ni kuendesha na kuimarisha huduma za meli kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi na kibiashara. Tunaamini kwa kufanikisha malengo haya Shirika litaweza kujiendesha wenyewe na kuweza kurahisisha shughuli za usafiri kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, ili kuhakikisha malengo hayo ya Shirika yanafikiwa Kamati inashauri katika uteuzi wa wajumbe wa bodi ambapo kimsingi ndio itakuwa na dhima ya kulisimamia Shirika kuwepo kwa mjumbe kutoka sekta binafsi ikizingatiwa kwamba watumiaji wakubwa wa sekta ya usafiri wa baharini ni kutoka sekta hiyo.

Mhe. Spika, katika kuona kuwa bodi inakuwa imara katika kulisimamia Shirika Kamati inapendekeza kuwa katika uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi, Mhe. Rais ahakikishe kuwa anateua mtu mwenye sifa na uzoefu katika mambo ya usafirishaji wa baharini ili kuona azma ya serikali inaweza kufikiwa kwa kulisimamia na kuliongoza Shirika ipasavyo.

Mhe. Spika, pamoja na mambo mengine, kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuweka ndani ya mswada huu utaratibu mzuri wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika ambapo pia umefafanua jinsi ya uteuzi wa wajumbe wa bodi, vikao vya bodi pamoja na mambo mbali mbali yanayohusu uendeshaji wa bodi hiyo.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba miongoni mwa shughuli au kazi za Shirika ni uwakala wa meli za nje, kama kifungu cha7 (e) kinavyoonesha. Shughuli ambayo huliingizia mapato shirika na serikali kwa ujumla, hivyo ni vyema kitengo hicho cha Shirika kikaboreshwa kwa kupatiwa wafanyakazi wenye uwezo ili kurahisisha shughuli za uwakala pamoja na kudhibiti mapato yanayopatikana kupitia shughuli hiyo

Mhe. Spika, baada ya kuupitia mswada huo, kamati yetu imependekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuimarisha mswada huo. Kwa ruhusa yako Mhe.Spika naomba niainishe baadhi ya marekebisho kama ifuatavyo:

Kifungu cha 3(2) (e) kimependekezwa kisomeke “kufanya jambo lolote au majukumu yoyote ambayo yanaweza kufanywa na Shirika kisheria” kifungu hiki kimependekezwa kisomeke hivi ili kuendana na mswada wa kiengereza.

Mhe. Spika, pia katika kifungu cha 9(1) katika maneno ya pembeni yamependekezwa yasomeke “kutoza ada na malipo mengine”. Kifungu hiki kimendekezwa hivyo ili kuendana na maelezo ya kifungu husika. Aidha, katika kifungu hicho hicho maneno “linaweza kutia nguvu malipo ya” yamependekezwa yasomeke “litatoza”. Kifungu hiki kimerekebishwa ili kuona ile dhana ya Shirika ya kutoza kodi na tozo nyengine inafahamika zaidi.

Mhe. Spika, kamati yetu pia imefanya marekebisho katika kifungu cha 10(2) (f) ambapo yameongezwa maneno “kutoka sekta binafsi” kifungu kimerekebishwa ili kutoa mwanya wa ushiriki wa sekta binafsi katika Bodi ya Wakurugenzi ili kutoa fursa kwao kuweza kuwasilisha mawazo yao katika sekta ya usafiri wa baharini.

Mhe. Spika, aidha katika kifungu cha 14(1) imeongezwa aya mpya ya 14(1) (d) ambayo itasomeka “kuidhinisha bajeti, kanuni na matumizi ya Shirika”, kifungu hiki kimeongezwa il kumpa waziri uwezo wa kuwa na usimamizi mzuri katika Shirika.

Mhe. Spika, kamati yetu pia ilifanya marekebisho ya uchapaji kama yanavyoonekana katika waraka wetu tuliouwasilisha kwako na nakala za waraka huo kusambazwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa msingi huo na kwa kujali muda wako Mhe, Spika nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waupitie waraka huo ili kuona baadhi ya vifungu ambavyo sikuwahi kuvitolea maelezo hapa.

Mhe. Spika, kwa muhtasari hayo ndio mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Mswada wa Sheria ya kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar kazi, uwezo na mambo mengine yanayohusiana nayo. Sasa kwa heshima nawaomba Wajumbe wote wa Baraza hili nao wauchangie vizuri Mswada huu kwa lengo lile lile la kuuimarisha zaidi na hatimae kuukubali bila ya pingamizi yoyote.
Mhe. Spika, napenda kutamka bayana kuwa mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kwa niaba yangu naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Marina Joel kwa kuokoa jahazi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni ya leo kunipa nafasi kuweza kutia baraka mswada huu wa kutunga Mamlaka ya Shirika la Meli. Kwanza niipongeze serikali kwa nia nzuri sana na kwa upeo na ikiongozwa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, mambo mengi yamezingatiwa katika mamlaka hii ya Shirika la Meli isipokuwa ni matatizo madogo madogo tu ya hapa na pale ya kibinadamu hayo yamo na ndio maana yaliyojitokeza humu hata kamati imeona iombe kurekebishwa. Lakini vile vile Mhe. Spika, hali halisi tunaitambua ya kuondoa shirika na kuweka mamlaka ni moja katika mambo ya ufanisi. Hii

niseme labda Mhe. Waziri ni mpya akiongozwa na naibu wake pamoja na wataalamu wa shirika na wanasheria waliona wafanye hivi kwa makusudi, kwa sababu kuna mambo ambayo huwa kama mamlaka kwa mujibu wa sheria huwa yanaweza yakapewa fursa. Lakini ukiweko katika shirika ina maana tayari wewe unakuwa tegemezi. Sasa hii sheria kwa kuwa leo imesomwa na mjumbe na ameisoma kwa ufanisi kabisa mimi nilisema labda kuna huyu mama wa Mambo ya Nnje, Asha Rose Migiro kaingia humu kwenye Baraza kwa jinsi alivyoisoma vizuri sana.

Kwa hivyo, Mheshimiwa kuna mambo ambayo tulipokuwa tukitembelea katika kamati walitwambia jamani kuna mambo ambayo sasa hivi tunarudi nyuma kutokana na kuwa hatuna uwezo wa kujiamuliwa wao wenyewe, huwa wanataka fedha za kujiendesha. Mfano mdogo hapa juzi tu, tulifanya mchango wa ghafla tu katika kutafuta fedha za ujengaji wa meli upya, japo umeshachukua muda manaake mpaka leo hatujaambiwa lolote kuwa meli ile imeshaanzwa mkuku au vipi. Hicho kitu Mhe. Spika, bado hatujapewa.

Lakini kwa makusudi serikali imeona hivyo kuwa lazima sasa hivi Shirika la Meli ambalo tunatamka rasmi itapopitishwa baadae na Mhe. Rais itakuwa na mamlaka yake yote kwa mujibu wa sheria na itakuwa na uwezo kutokana na mambo ambayo ikisimamiwa na mwenyewe Mhe. Waziri kwanza masuala ya kanuni na hili tulilisema sana. Kanuni isiwe bodi ambayo inaweza ikatunga ile kanuni, isipokuwa mwenyewe waziri aweze kutunga ile kanuni au bodi inaweza ikaonesha njia tu ili waziri ndie mwenye uwezo zaidi wa kuwezsa kuitoa kanuni ile na kuitangaza katika Gazeti la Serikali.

Mhe. Spika, mimi nashukuru sana kwanza hili shirika lenyewe na niwapongeze sana hasa kwa jitihada zao na mpaka leo bado wana uwezo wa kujiendesha wakisimamiwa na mwenyewe kapteni Sururu na naibu wake pamoja na watendaji wake.

Mhe. Spika, ingekuwa kama mashirika mengine sasa tuna hadhithi tu, lakini kwa kuwa hii ina wataalamu hawa wale ambao wa *International* na mpaka leo ina- *survive*. Kwa sababu kule inapata tija nyingi ndio tukasema basi kama ni hivyo tuache tuwakubalie na kama alivyosema Mjumbe hapa aliyesoma kwamba wajumbe wote kwa maana hiyo hapa mwaka wa porini. Kwa maana hiyo haya mimi mwenyekiti kusema tuwakubalie basi naamini na suala hili wajumbe wataona kuweza kulikubalia hili suala la Shirika ili kuleta ufanisi zaidi hasa kwa vile tunakwenda na wakati kama tulivyoambiwa, sheria duniani zinageuka tunakubaliana na hilo na ndio maana tukasema kuwa sasa tuelekee huko kunako sheria.

Lakini vile vile tukizungumza masuala ya uwakala kwa kuwa hiki ni chombo chetu ambacho kinatafuta *funds* na sasa hivi mtoto anataka kuachishwa kwa wazazi wake. Kwa hivyo, sisi tumeona iko haja ya kuweza kuwa awe yeye, kwa sababu sasa hivi bado hatujawa na mwengine, sheria hii ikubali kumridhi awe yeye ndiye wakala kama anavyoendesha hivi sasa. Tulijaribu kuonana nao na tukawauliza wamejipanga vizuri sana katika muundo huo wa kisasa unaokubalika duniani kuwa wakala.

Mhe. Spika, na hili tumeliona hili kwa makusudi tukasema basi kama ni hivyo hatukuwa na matatizo yoyote tutawaachia wao ili waendeshe na kitengo hiki na dhana ile mamlaka yenyewe lakini itakuwa ni nje. Kwa sababu sheria nayo imewapa wasiwe wao *totally* kabisa iwe kama wanawekwa kidogo pembeni wana kikampuni chengine ili kuondosha lakini itimize masharti

hayo yanayotakiwa na watu wa SUMATRA kule wamo katika hatua za mwisho sasa hivi. Nafikiri labda hili nalo Mhe. Waziri atakuja kutueleza kuwa hatua zenyewe zimefika wapi, kuwa tayari imepata *certificate* ya kuendelea na shughuli zake kama kawaida yao.

Lakini Mhe. Spika, hivi karibuni nilisikia tetesi kama Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais katika ziara zake alikwenda kule kunako Shirika letu huko tulikoungana nao katika wakala, labda na yeye tungepata kidogo fikra yake ikoje. Kwa sababu tulisikia kuwa kulikuwa na hitilafu za hapa na pale katika zile meli za nyuma zilizokuwa zifutiwe ule uwakala. Hili nalo limekuwa kimya, hatujapata tamko lolote sasa nalo hili tungeona kwa makusudi Mhe. Makamo wa Pili nalo akatumegea kidogo katika kupitia pale *transit* yake kama aliwaona hawa wakala labda kama kuna na *briefing* fulani hivi ya kuweza kuzungumza na ikatueleza angalau sisi wengine *pressure* ikapata kushuka ili tuweze kuelekea kunakofahamisha hivyo.

Mhe. Spika, kwa kuendelea kueleza hii mamlaka kama nilivyosema kuwa tulikubaliana kwa sehemu nyengine tukasema kifungu hiki kuhusu habari ya muhuri wao wawenao wa shirika, lakini muhuri wanaujua wao maana yake wafanye ule muhuri wa kisasa sio mihuri ile ambayo inayojengwa pale Mkunazini au wapi. Lakini hiki kitu ambacho tunasema sana mara nyingi kuna idara nyengine zinakuwa mihuri yao haikua katika *standard*. Kwa sababu unatengeneza muhuri kwa kutumia chombo hiki ni kikubwa lazima utafute muhuri ambao mtu mwengine atashindwa kuukopi. Sasa kifungu hiki nacho tukasema hapana tuachie, kuwe na ofisi iliyokuwa na muhuri wao lakini uwe *model* ambao hawezi mtu mwengine kuweza kuukopi.

Suala hili Mhe. Spika, tuliangalie sana, maidara mengi wanakuwa na mihuri ambayo anaweza kutengeneza mtu mwengine, hii tunaweza tukafanyiwa udanganyifu kwa sababu mtu anaweza akatengeneza vitu ambavyo tayari akaiibia. Sasa mimi naona hili suala kwa kuwa ni suala zito na ni nyeti basi katika kifungu hiki Mhe. Waziri lazima atuletee muhuri wa kisasa bwana, asione tabu, asione hasara kwa sababu jambo lolote ni hasara mchezo mzuri huwa ni hasara Mheshimiwa. Kwa hivyo, lazima tuletewe muhuri mzuri ili watu wengine wasiweze kuukopi na hasa kutokana na mamlaka yake kama alivyosema kwamba sasa hivi tayari imepewa *power*.

Lakini vile vile sio muhuri tu, tuangalia na hizi nembo zetu. Nembo nazo ni moja katika *security* nzuri ya ile sehemu yenyewe basi na hizi nembo nazo *art* ziwe ni nzuri, wapewe wataalamu, zitolewe *tender* watu wampelekee halafu ataona ipi ni nzuri, lakini tusiende ovyo ovyo tu. Kwa sababu hizi nembo watu wengine wanaweza kufanya tu kwenye kompyuta si mtandao sasa hivi, lakini nayo hii tunaona sana mara nyingi sana kuna mashirika mengine nembo zao kwa kweli zimepitwa na wakati, hivi tuseme ukweli Mhe. Spika, nembo haziendi na wakati wa kisasa lakini ukikuta sehemu nyengine wana nembo nzuri sana, wewe utakwenda kutizama ile nembo tu kwenye karatasi wanavyoiweka huangalii kitu chengine. Sasa na yeye Mhe. Waziri tumeona tuweze kumwambia naye aweze kutuonesha kitu hiki ili kufikia malengo mazuri.

Lakini Mhe. Spika, tulitizama katika sheria tukaona ni kweli hakuna asiyejua kwamba sisi sote tunatumia pesa ya *Tanzania Shillings*, lakini humu tuna mambo ya dola. Sasa mimi nikasema mheshimiwa bora alipe ile shilingi ya Kitanzania, tafsiri ya dola tukasema hebu tujaribu kuiondoa lakini kama itafaa sentensi ile ile ya kuwa dola iwepo basi angalau yule mtu aweze kulipwa kwa *Tanzania Shillings*. Mhe. Spika, nalo hili tukasema aah, tukubaliane nalo tuweze kufanya hivyo.

Mhe. Spika, tumesema kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika, ukurasa wa 305 huo. Lakini (b) kikasema kwamba, "ana uzoefu katika fani yoyote miongoni mwa sheria, uongozi, utawala, uchumi, fedha au fani inayohusiana na mambo ya usafiri wa baharini". Mhe. Spika hilo ni kweli, tujaribu kumshawishi Mhe. Waziri, kuna mambo yanakubalika kumuweka mtu ambaye tayari amekuwa ana *experience* na yale mambo, hivi kweli utamtoa daktari ukampeleke katika fani ile ya meli wapi na wapi Mheshimiwa na ndio maana mashirika yetu yenye shughuli kama hizi yanakuwa yanafeli kutokana na hivyo, hatuzingatii uwezo wa yule mtu, uzoefu wake kwa maana ya muda wake alioanza kazi zile tunakuwa tunateuwa mtu tu.

Sasa nalo hili nawaombeni sana Waheshimiwa Mawaziri mnapokaa na Rais na hili nalo mumshauri. Tukiweza kufanya hivi Mhe. Spika, basi sidhani kama mamlaka zetu zitaweza kufia njiani na kweli ukiangalia tulikuwa na mashirika mangapi hapa, mengi yamekufa. Sasa na hili mimi kwa kuwa naamini hivyo limejaa wataalamu basi mimi nina hakika kwa Mhe. Rais atayemteuwa mkurugenzi huyu basi na yeye atakuwa katika hali ambayo ya taaluma aliyopewa ili kuweza kufanyakazi kwa ufanisi vizuri, ili aweze kuiletea matunda mamlaka.

Lakini Mhe. Spika, kifungu cha 14 "Uwezo wa Waziri", mimi sikuwa na tatizo kubwa nalo sana. Mhe. Waziri kupewa uwezo huu tukasema kwa sababu yeye ndio *head of department* pale. Sasa ni lazima kuna mambo mengine tunaweza tukampa waziri lakini na yeye aangalie utaratibu wa ukomo wa sheria unatwambia nini. Kwa sababu unaweza ukampa waziri uwezo mkubwa baadae mkagombana kidogo tu akalitulimia rungu lake, ikawa ule uwezo wenyewe tumempitisha zaidi. Sasa nalo hili nimeona niweze kulisema kumtahadharisha Mhe. Waziri kuwa yasiteyasite rungu lake asilitumie, kwa kuwa tena sheria tumeipitisha akalitumia zaidi baada ya hapo tulipompa. Aangalie mazingira haya ili kwa kuweza kuliendesha lile shirika kwa kutoa taaluma ambayo aliyokuwa nayo na mashirikiano nayo pamoja na wafanyakazi wake.

Halikadhalika kifungu (b) tumeona ipo lazima. Kifungu nikinukuu kifungu hiki kwa, "Kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha ataidhinisha mabadiliko yoyote makubwa ya ushuru, kodi, nauli na tozo nyengine zinazowekwa kwa huduma zinazotolewa na shirika".

Mhe. Spika, mimi sioni tatizo kubwa sana na watu wamesema panapofungu ndio penye nyongeza. Mimi nitaona ajabu Mhe. Waziri akenda kumuona Waziri wa Biashara au Waziri wa Afya, hapana kitu huko, atamshauri nini. Lakini ni haki yake kwenda kwa Mhe. Waziri wa Fedha ndio panapofungu.

Sheria nyingi zipo pale wakati yeye hawezi kuzilimiliki sheria zile, hatujampa mamlaka hayo mengine sheria za kuweza kufanya pale bandarini. Lakini ni vizuri sana kuwa na uwezo wa kumwita Waziri wa Fedha wakakaa na kupanga kama haya tuliyozungumza.

Shirika au mamlaka Mhe. Spika, halitokuwa katika njia ya kuweza kuyumba kwa sababu tayari fursa hiyo tunampa waziri kwa kumwita Waziri wa Fedha, asimwite Waziri wa Kazi aah! hana kitu pale, amwite huyu huyu yeye Waziri wa Kazi wakitaka watu kazi atakwenda kumchukua atamwambia bwana wewe huku sasa nataka kutoa kazi niende nikachukue atakwenda kuchukua

kule. Lakini kwa ushauri wa fedha atamuonea bure kwa sababu hana fedha Waziri wa Kazi, yeye mwenyewe anatafuta kwenye serikali apewe na bajeti yake ndogo.

Lakini Mhe. Spika, bado naendelea. Tumesema mamlaka itakuwa ina uwezo wa kusomesha wataalamu na hii ndio maana ya mamlaka kwa sababu mfano mdogo Mhe. Spika, hivi sasa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, tumeipitisha sheria lakini hivi sasa wamechukua mzigo mzito wa kuwasomesha wataalamu. Na hivi Mhe. Spika, ndivyo tunavyotaka kwa sababu sheria sasa hivi tuchoke kuchukua ma-*experts*, tukichukua ma-*experts* basi tuhakikishe *expert* yule kwa muda miaka mitano basi aweze kumfundisha Mzanzibari ili aweze kufanya kazi ile.

Mhe. Spika, hapa ndio tunapofeli. Ukweli tuuseme. Tunawachukua ma-TX kwa pesa nyingi sana lakini akiondoka yule hana mtu anayemfundisha, ina maana sisi tunakula hasara kubwa sana.

Sasa mamlaka nayo iwe na uwezo wa kuwasomesha wataalamu ili kuweza kuliendesha ile mamlaka yenyewe, ndio tunavyotaka iwe hivi. Leo aangalia pale uwanja wa ndege *alhamdulillah* wataalamu wanapatikana, watoto wanakwenda kusoma, mambo yanabadilika siku hadi siku.

Na hii tunaitaka mamlaka halikadhalika kila baada ya muda tuone mabadiliko yake kutokana na nyinyi wahusika ambao mutachaguliwa kwa Mhe. Rais, Bodi pamoja ikiongozwa na wenyewe Mhe. Waziri basi waende katika hiyo niliyosema mimi, lazima wasomeshe wataalamu kwa muda mchache sana, tumechoka na wataalamu. Wasomi tunao na hiyo ni hakika Mhe. Spika.

Hivyo Mhe. Spika, unichukue mimi ukanisomeshe huko si nitafanya mambo ya maana hapa. Lakini leo unanidharau hatutaki kuwasomesha, sasa tutafika wapi Mhe. Spika, kwa sababu tayari uwezo unao.

Sasa mimi nafikiria Mhe. Spika, nalo hili tuliangalie kwa makini kabisa tuone kwa muda wa miaka hii tuliyobakia nayo mambo yanakwenda vizuri. Na mimi naamini sana Mhe. Waziri kwa hili jambo lilivyokuwa ni mtaalamu, ni mwalimu anajua, Naibu wake ni mwanasheria anachukua maana ya kusoma. Sasa leo *his failure* nitaona kitu cha maajabu sana kabisa, angalau jamani Mhe. Waziri siku moja ulipokuwa kwenye kamati ulisema, hivi mtu akiwepo katika ukurugenzi au katika *department* basi hakuna mtu akiondoka pale hasifiwi kwa uzuri? Ameweka kitu ambacho cha msingi kinachoongoza watu.

Sasa leo Mhe. Waziri ngoma imekugeukia hii. Angalau ukija ukiondoka watu wajue waseme aah! Katika mamlaka ile ina wataalamu thalathini kwa kila idara. Sasa mimi niseme hivyo Mhe. Waziri na mimi nakuamini kabisa unaweza kulifanya hili jambo na likaleta mantiki.

Mhe. Spika, kwa mara yangu ya kwanza leo nataka nikwambie naunga mkono asilimia mia kwa mia katika mswada huu wa kuunda mamlaka. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kupata fursa jioni hii ya kuchangia mswada huu uliopo mbele yetu, mswada wa kuanzishwa kwa Shirika la Meli Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, pia niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona kama kuna haja ya kuanzisha Shirika hili la Meli Zanzibar.

Mhe. Spika, suala hili limekuja wakati muafaka kabisa hasa ukizingatia kama tunategemea kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kama serikali imeahidi kutengeneza meli mbili kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Zanzibar. Sasa mimi niseme kama ni wakati muafaka. Lakini Mhe. Spika, mimi kama ni mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, mswada huu nimeupitia vizuri sana na mswada ambao uliokuwa hauna matatizo, upo safi kabisa isipokuwa kuna mambo kwa sababu kila kizuri hakikosi na kasoro japo ndogo ndogo, kwa hivyo nawaomba wajumbe wenzangu tuuchangie mswada huu na pale pa kuboresha tuboreshe, pale pa kuelekeza tuelekeze.

Mhe. Spika, mimi nashukuru sana kuona kama sasa hivi tunaanzisha shirika hili. Lakini Mhe. Spika, naiomba serikali ione kama shirika hili tunaanzisha shirika siku zote ni chombo ambacho huwa kinajitegemea. Kwa hivyo naiomba serikali ione kama kuna haja ya kuliboresha hili shirika liwe ni shirika la kibiashara linalojitegemea na linalofanya kazi kiushindani wa kisasa.

Mhe. Spika, kuanzisha shirika ikawa ni shirika halina uwezo itakuwa hatujafanya kitu. Kwa hivyo naiomba serikali ilipe fursa shirika hili ili lifanye biashara na liweze kujitegemea kwa kufanya biashara na pamoja na uwakala. Lakini liwe linafanya kazi kwa ajili ya kuleta matumaini kwa Wazanzibari, tusiwe tuna shirika tukawa tunarudi kama tulivyokuwa, tuone ule ubora wa shirika. Hivyo serikali iipe fursa na nafasi ili iweze kufanya biashara na kuweza kuhimili ushindani wa kisasa.

Lakini Mhe. Spika, pamoja na hayo yote tunaingia kwenye shirika tunaleta meli lakini kuna kitu ambacho naomba serikali ione kuwa kitu hiki basi kinaweza kikaturudisha nyuma pamoja na uwakala, kwa sababu hili ni Shirika la Meli na Uwakala. Lakini huu uwakala wanafanya kazi zaidi kwa zile meli ambazo zitakuwa zinakuja na wanafanya ili kuingiza mapato kwenye Serikali ya Mapinduzi.

Sasa Mhe. Spika, hatuwezi kufanya kazi ya uwakala kwa ubora zaidi kama na ile bandari yetu hatujaitanua. Kwa kweli Mhe. Spika, bandari yetu ni finyu, hali ambayo inarudisha nyuma hao wakala wenyewe. Kwa hivyo pamoja na kuwa tunaanzisha shirika na serikali ione kama kuna umuhimu wa kufanya kila linalowezekana ili kupata bandari ambayo itakuwa inakidhi haja na ili kuongeza mapato ya serikali, kwa sababu wao huo uwakala unakuja kwa zile meli kuingia kwa wingi.

Sasa kama meli hazipati kuingia kwa wingi huo uwakala wenyewe utakuwa haufanyi kazi. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba serikali kuwa hiki ni kitu muhimu sana, hivyo serikali ina azma ya kuboresha pale Mpigaduri au kujenga pale.

Hivyo ione kama hiyo azma yake inaifanyia kazi kwa hila na njia zote, kwa sababu hivi sasa Mhe. Spika, kama itakuja meli moja tu ya kigeni na ikiwa ni meli ambayo ni kubwa sana basi bandari yote inamalizwa na meli moja, meli nyengine zinakaa zinasubiri inakuwa hazipati kufanya kazi na huo uwakala wenyewe unakuwa haufanyi kazi kwa nguvu.

Kwa hivyo na hili Mhe. Spika, na hili naomba serikali ione kwamba kuna umuhimu sana. Lakini wakati huo huo shirika hili ikiwa litapewa meli za kufanya biashara basi ihakikishe serikali ione kama wamekabidhiwa meli basi zile pesa za meli zilizonunuliwa basi shirika linafanya kazi na kuona kama zile fedha walizopewa zinaingiza, kwa sababu ikiwa wamepewa mtaji ijue serikali kama ule mtaji tayari umeshaingia.
Sasa na wao wawe na uhuru, kama nilivyosema kwenye mswada kama ni kuuza meli basi wapewe uhuru, ikiwa tayari meli imeshachoka inataka kuuzwa wawe na uhuru wa kuweza kuuza na fedha zile kuingia kwenye shirika.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu ni mzuri kama nilivyozungumza na mimi kwa sababu ni mjumbe wa kamati sitaki nichukue muda wako mkubwa ilikuwa kwa kweli niboreshe boreshe kidogo, ili kuwapa fursa na wajumbe wengine waweze kujiandaa na kuuchangia mswada huu.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono mswada huu *mia fil mia*.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia masuala mawili matatu katika mswada wetu huu wa kuanzishwa kwa Shirika la Meli la Zanzibar na kazi zake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii na jioni hii ya leo baada ya asubuhi kupata matatizo ya hapa na pale, hatimaye jioni hii tukaweza kuendelea na shughuli zetu kama zilivyokuwa zimepangwa.

Mhe. Spika, vile vile niendelee kwa kuwashukuru sana, watendaji na wafanyakazi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano chini ya usimamizi wa Waziri wake na wasaidizi wake wote kwa ujumla kwa kukaa na kuweza kutuletea mswada huu kwa siku ya leo na tukaweza kuja kuujadili pamoja na kuweza kutoa machache yanayoweza kusaidia kuweza kutia baadhi ya nyama na maeneo mengine ambayo tunahisi tunaweza kusaidia katika kuchangia baadhi ya mambo mawili matatu.

Mhe. Spika, mimi nianze na sehemu ya pili ya mswada huu. Katika sehemu ya pili ya mswada huu kifungu cha 3 (2), kuna maneno hapa yamezungumzwa kwamba kuingia mikataba yoyote kama itakavyolazimika na ufanisi wa utekelezaji wa malengo yake chini ya sheria hii au sheria yoyote ile.

Mhe. Spika, ukiangalia katika baadhi ya vifungu ambavyo vinafuata chini, mamlaka haya yote ambayo yanakuwa yanapelekwa katika shirika hili yalikuwa mara zote yanapata ridhaa ya bodi. Lakini kipengele hiki bodi hapa haikuzungumzwa. Sasa tungelimuomba Mhe. Waziri atakapokuja atusaidie kama ambavyo amekuja kuzungumza katika kifungu cha 4 (1) na kifungu cha 5, vile vile imekuwa imezungumzwa baadhi ya mambo lakini hapo hapo yalikuwa yanahitaji maelekezo na ridhaa ya bodi.
Eneo hili vile vile tungeliomba vile vile kifungu cha (d) nacho kiweze kupata ridhaa ya bodi kama ilivyo katika maeneo mengine. Lakini vile vile kwenye mswada huu wa kiingereza kifungu hiki hiki cha (d) katika sehemu ya pili kifungu cha 3 (d) kuna maneno pale mbele baada ya *contract has made necessary*, kule kuna “or”. Lakini kwenye *translation* ya Kiswahili huku kuna “na”.

Tungeliomba ili iweze kuleta maana iliyoweza kukubalika tufuate ule ule mswada wa kiingereza ili iweze kuja maana hasa iliyokuwa imekusudiwa.

Jengine Mhe. Spika, mimi niseme tu mswada huu ambao umeletwa kwetu sisi Wawakilishi ni mswada mzuri na mswada ambao unastahiki kwa wakati huu kuweza kupitishwa na kukubaliwa wawakilishi wenzangu wote ambao wameweza kuja hapa leo na kuweza kuuangalia mswada huu.

Ningeliwaomba sana, kwa heshima zote tuwape ridhaa na tukubali mswada huu ili Waziri pamoja na kamati yake waweze kuendelea na taratibu ambazo tumekubaliana. Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii kuchangia mswada huu.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha mswada huu mbele yetu. Kwa kweli kama walivyotangulia wenzangu niseme mswada huu tuusome na kisha tuupitishe.

Kifungu cha 3 (1) kinachosema kwamba kuanzishwa kwa Shirika la Meli, mimi niseme kwamba ni sawa sawa shirika letu hili la meli ambalo tunaona kwa kutokana na hali ya uhitaji kwa sababu visiwa vyetu vimeambatana na bahari na ni lazima kama serikali ianzishe shirika hili la meli.

Vile vile kwenye kifungu cha 4 (1) kinasema kwamba kutakuwa na muhuri. Kwa kweli na mimi niseme kwamba kifungu hiki ni muafaka ni lazima shirika lolote au mahala popote kuwe na alama yake. Kwa hivyo na Shirika la Meli kuwa na muhuri ni jambo la maana sana.

Makao makuu ya shirika kifungu cha 5, vile vile Mhe. Spika, niseme kwamba jambo lolote likianzishwa basi kunakuwa na pahala ambapo panachaguliwa pakawa ni makao makuu na mambo yote yakafanywa pale. Kwa hivyo hiki kifungu niseme Mhe. Spika, naunga mkono kwa kuwepo kifungu cha 5 ambacho kinachozungumzia juu ya kuwa na makao makuu ya shirika.

Vile vile kuna malengo ya shirika. Nikisema nakwenda na kifungu kimoja kimoja, malengo ya shirika kuendesha na kuimarisha huduma za meli kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kibiashara Zanzibar. Kwa hivyo Mhe. Spika, ni lazima jambo lolote kwa mujibu wa kanuni zetu au sheria zetu na hasa jambo lolote linaloanzishwa linaanzishwa kwa munasaba wa kuwasaidia wananchi wa Zanzibar.

Kazi za shirika kama zilivyojitokeza vile vile kwamba kutakuwa na kazi zilizoainishwa hapa lakini vile vile kuna shirika kifungu cha 8 “Uwezo wa shirika”. Lazima shirika liwe na uwezo na kwa sababu yamejitokeza mara nyingi kwamba mashirika mengi na hasa hapa Zanzibar yananyimwa uwezo wa kuendesha mambo yake na baadae mashirika haya yakawa hayakuwa endelevu kutokana na labda kutokuwezesha serikali au kuwapa ule uwezo hasa lile shirika lenyewe.

Kwa hivyo ni lazima kama shirika liwe na uwezo wake. Mhe. Spika, uwezo wa kuwalazimika. Nasema shirika linaweza kutia nguvu malipo ya ada, nauli na malipo kwa huduma za meli zitolewazo na shirika likiwa ni pamoja na malipo ya huduma, malipo ya sasa na malipo mengineyo ya aina yoyote.

Uwezo huu vile vile kwa shirika inalazimu liweze kutoa pamoja malipo ya huduma ya malipo ya meli kama, ni lazima hili shirika lenyewe liwe linajipangia nauli na mambo mengine.

Vile vile tumeona kwamba kuna kifungu 12 (1) kwamba kutakuwa na mkurugenzi mkuu wa shirika ambaye atateuliwa na Rais kwa kipindi na masharti kama yatakavyoainishwa. Mimi niseme na kifungu hiki vile vile nakiunga mkono kwa sababu katika kifungu (a) na (b) vyote vinaonesha kwamba kutakuwa na (a) Mkurugenzi huyu ni muhumu atoke katika Chuo Kikuu kinachotambulika au taasisi inayolingana au ana uzoefu. Mimi niseme kwamba Rais atamteuwa mkurugenzi mkuu na ni lazima awepo mkurugenzi mkuu. Kwa hivyo Mhe. Spika, hili sina tatizo nalo na kwa sababu na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani nina jukumu la kupitisha sheria hizi, hivyo naunga mkono uteuzi huu wa mkurugenzi mkuu.

Mhe. Spika, nambari 13 kuhusu uteuzi wa afisa mwandamizi. Vile vile nasema kwa mujibu wa shirika na kwa sababu ni lazima ijipange na kwenye mambo yake ya ufanisi basi ni lazima kuwe na uteuzi ambao wa watu ambao watasimamia shughuli za shirika.

Vile vile uwezo wa waziri unasema kwamba yeye atakuwa kutoa maelekezo kwa jumla kwa bodi. Vile vile tunaona kwamba hizi bodi zinakuwa zinachukua majukumu, kwa hivyo nayo ili yawe ule uwajibikaji na kwa sababu pale kwenye bodi kunakuwa na pesa nyingi ambazo zitakuwa zinatumika, kwa hivyo ili shirika liende kwa faida, hivyo tutizame ile kinachoingia kwenye shirika isiwe kwamba kunasimamiwa lakini ikawa pesa nyingi zinakwenda kwenye vikao labda vya bodi na mambo mengine. Kwa hivyo ni lazima kuwe na uwajibikaji mzuri sana ili shirika liweze kuendelea na liwe endelevu.

Mhe. Spika, kuna taarifa ya mwaka kwenye kifungu cha 19 ni lazima bodi kwa kipindi kisichozidi miezi 6 baada ya mwisho ya kila mwaka fedha itawasilishwa kwa waziri na kwa kamishna na taarifa za mwaka kwa mwaka huo ikiwa na nakala za mahesabu ya shirika yaliyokaguliwa pamoja na taarifa za wakaguzi wa mahesabu hayo.

Ni sawa kwamba ili mashirika haya yawe endelevu ni lazima yawe yanafunga mahesabu na yanatoa taarifa kwa wahusika na hasa ikiwa sisi ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, mambo kama haya ni lazima yawepo wazi, tujue hesabu zinavyofungwa na vile vile kwa sisi ni wawakilishi wananchi kwenye mashirika haya ya serikali, kwa hivyo ni lazima kuwe na mahesabu ambayo yatajulikana.

Na vile vile kuna sehemu ya tano ambayo ina masharti ya jumla. Kwenye kitabu cha orodha na bei. Shirika linaweza kuandaa na kuchapisha kila baada ya muda kama bodi itakavyoona inafaa kitabu cha orodha ya bei ikiwa na maelezo ya huduma zinazotolewa na shirika chini ya sheria na kiwango cha kila moja malipo ya nauli ya ada.

Basi vile vile kifungu hiki mimi nasema kwamba ni lazima kuwe na vitabu na vitabu hivi basi viwe vinaoorodheshwa vitabu vya bei ambavyo vitakuwa na *counter folio* au *counter book* ambalo litakuwa linajiorodhesha hivi vitabu vya mahesabu.

Kuna kifungu cha 21 ambacho kinasema uhaulishaji wa miliki ya meli. Hapa pia Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwepo kifungu hiki cha uhaulishaji wa miliki za meli. Juzi au jana tulipitisha sheria moja hapa ambayo ya kuweka sheria ile ya vyombo vya baharini, kwa hivyo niseme nayo pia shirika litakuwa linasimamia juu ya umiliki huu wa meli na vile vile iwe ni chombo ili shirika ambacho kitakuwa kinasimamia hata usajili wa meli nyengine labda ili kuweza kuzisimamia vizuri.

Mhe. Spika, niende na jambo jengine ambalo tunaliona katika mashirika yetu haya ni ufungaji wa mahesabu. Kwa sababu sisi kwenye ufungaji wa mahesabu, mara nyingi yanajitokeza kwamba mkaguzi wa mahesabu ni CAG lakini kwenye mashirika kama haya mara nyingi yanayojitokezea ni kwamba wanakuwa wanatafuta CAG kutoka sehemu nyengine ambayo anakuwa sio CAG wetu.

Kwa hivyo vile vile hili ni tatizo kwamba mashirika mengi yanakuwa hayafungi mahesabu kama zilivyo na tunakuta kama ni tatizo, kwa sababu sisi CAG wetu hakupita, wanatafuta tu ma-CAG kutoka nje ya nchi. Kwa hivyo vile vile inakuwa ni tatizo kubwa kwa CAG wetu kupata mahesabu kwa uhakika, kwani mahesabu yale yanakuwa hayakamilishwi na vile vile kama serikali inakuwa haizijui raslimali zake hasa kwa sababu mahesabu yanakuwa hayafungwi kwa mujibu wa sheria za CAG wetu na inakuwa ni usumbufu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, niseme kwamba ni lazima wanapofunga hesabu kwa sababu kuna *financial year* ambayo wengine wanatumia kuanzia Januari mpaka Disemba na mashirika haya ndio mara nyingi ndivyo yanavyotumia kwamba Januari mpaka Disemba, lakini vile vile sisi *financial year* yetu ni kuanzia Julai mpaka Juni.

Vile vile Mhe. Spika, CAG huwa kila baada ya kufunga hesabu, tunatakiwa mashirika pamoja na serikali ifunge hesabu zake ikishakufika Julai na mpaka mwisho wa mwezi Septemba iwe imeshakamilisha kupeleka mahesabu yake kamili kwa CAG ambaye yeye anaziweka pamoja. Bila ya kuzipeleka hesabu hizo kwa CAG basi serikali itakuwa haijui mali zake ni zipi, kwa sababu kunakuwa na mapungufu ambayo yamejitokeza.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nitilie mkazo suala hili la kufunga mahesabu na hesabu zile kukaguliwa na CAG wetu ambaye yuko kikatiba, kwani kutopita hesabu hizi kwa CAG ni kumnyima ile haki yake ya kikatiba. Kwa hivyo, Mhe. Spika, na mambo mengi ambayo yanajitokeza katika maeneo mbali mbali ni kwamba hata zile *fixed asset register* pia zinakuwa hazikamiliki watu hawafungi. Sasa ningependelea sana kuwa Shirika hili la Meli lizingatie mambo hayo ya kwamba ziweke vile vitabu vyote, vile vile vifuate zile kanuni, sheria za fedha pamoja na sheria za manunuzi.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kukupongeza kwa kunipa nafasi jioni hii, ninaomba nitoe mchango wangu mfupi kwenye mswada huu wa Mhe. Waziri.
Mhe. Spika, nianze kwenye kifungu cha 3(1) (c) sehemu ya pili. Mhe. Spika, naomba ninukuu kwamba,

Kifungu cha 3(1) (c)

"Kuanzishwa kwa malengo na uwezo wa shirika, kazi moja ni kununua, kuchukua, kuhodhi na kutoa mali inayohamishika, isiyohamishika na ikiwa kwa kuwekeza au vyenginevyo".

Mhe. Spika, kifungu hiki cha 3(1) (c) naomba neno "kuhodhi" libadilishwe kwa sababu linaashiria ni sehemu ya nguvu. Ukisema neno "kahodhi" maana yake katumia nguvu. Kwa hivyo, naomba libadilishwe na badala yake iandikwe kumiliki, kwa sababu huu mswada mzima neno "kuhodhi" limetumika sehemu hiyo tu na mote limetumika neno "kumiliki". Kwa hivyo, badala ya kuhodhi tuseme tu kwamba shirika linaweza kununua, kuchukua au kumiliki badala ya kuhodhi, kwa sababu kuhodhi inaashiria kama ni sehemu ya kutoza nguvu na hasa kwa vile mswada mzima neno hodhi limetumika sehemu hiyo tu.

Mhe. Spika, sehemu nyengine ambayo ningependa kutoa mchango wangu ni kifungu cha 7(a) ambacho kinasema kama ifuatavyo.

Kifungu cha 7(a)

"Kusimamia na kuendesha meli za shirika kitaalamu na kwa gharama nafuu".

Mhe. Spika, najiuliza je kweli tutaweza kuendesha meli kitaalamu, kwa sababu tumezoea kufanya ile *business as usual*. Tumekuwa tunawatenga na kuwakataa wataalamu kwa mbali sana. Mtaalamu tumejenga mazoea kwamba sio mtu wa kusikilizwa. Kwa hivyo, najiuliza namuuliza na Mhe. Waziri aniambie je, wizara yake imejiandaa kuwatumia wataalamu kweli?

Mhe. Spika, unaposema kwamba unataka kuwatumia wataalamu je, mtaalamu hutumia gharama nafuu?

Mhe. Spika, kwa hivyo mimi napata mashaka, unaposema kwamba unataka umtumie mtaalamu, lakini unalazimisha atumie gharama nafuu nadhani hatujaweza. Siku zote uzuri una gharama. Watu wa mjini husema starehe ni gharama. Kwa hivyo, kama unataka utumie mambo kitaalamu maana yake ukubali kutumia gharama zinazostahiki na mimi napendekeza kwamba badala ya gharama nafuu, tuandike gharama zinazolingana na kazi hiyo. Usilazimishe mtaalamu atumie gharama nafuu tu. Haitowezekana kwamba meli inataka *service*, lakini umwambie tumia gharama nafuu, atumie gharama ambayo inalingana na *service* hiyo inayohitajika.
Kwa hivyo, Mhe. Spika, nashauri badala ya gharama nafuu, basi tuandike gharama zinazostahiki, ili usimfunge kwamba ni lazima akufuate wewe kwa gharama nafuu, ikiwa haiwezekani je. Hivi ikiwa *engineer* haja yake mashine ya kisasa, halafu umwambie tumia gharama nafuu, hiyo gharama nafuu mashine yake ataipata, wakati sisi hatuzalishi mashine hapa. Kwa hivyo, ni lazima tumuwekee mazingira ambayo yatamuwezesha kwa mujibu wa taaluma ambayo tunaruhusu.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu cha 8(c), naomba Mhe. Spika, ninukuu;

Kifungu cha 8(c)

> "kuamua kutoza na kukusanya malipo yoyote, nauli, madeni au ada kwa ajili au kuhusiana na huduma zake na adhabu zote za riba".

Mhe. Spika, mimi nashauri kwamba "adhabu zote za riba", neno hili liondoshwe na litafutwe neno jengine, kwa sababu adhabu sio lazima ya riba. Adhabu inawezekana ni ya makosa fulani, lakini usilazimishe kwamba lazima adhabu hiyo iwe ni ya riba na kwa hivyo nashauri litafutwe neno zuri zaidi litumike, badala ya kuweka adhabu zote za riba, kwa sababu adhabu nyengine sio za riba.

Mhe. Spika, vile vile kwenye *marginal note* huku ya kifungu cha 9(1), imeandikwa uwezo wa kulazimisha. Nashauri kulingana na mswada wenyewe ulivyoandikwa, basi tuweke uwezo wa kutilia nguvu, maana kulazimisha jamani ni nguvu. Kwa hivyo, tuweke ule uwezo wa kutilia nguvu kwamba sheria itilie nguvu badala ya kulazimisha, ukilazimisha maana yake unakwenda kinyume na utaratibu wa kisheria.

Mhe. Spika, kifungu chengine cha hiyo 9(4) kuna maneno kwamba;

Kifungu cha 9(4)

> "mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada au kutoa" nadhani hapa kuna maneno yameachwa, nadhani hapa ni "tozo", na "tozo zilizowekwa chini ya kifungu cha 3 cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa ada", nashauri tuongeze "ada hizo pamoja na nyongeza ya asilimia 50 ya ada hiyo kama adhabu ilivyoeleza". Mhe. Spika, hapa napendekeza tuongeze "ada hizo".

Mhe. Spika, kifungu chengine ni Sehemu ya Tatu kifungu cha 4 kuna;

Kifungu cha 4

> "mtu hatofaa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe na elimu na uzoefu katika mambo ya usafiri wa baharini, uongozi na utumishi wa umma".

Mimi nauliza Mhe. Spika, hii elimu ni ipi, mtu huambiwa ana elimu akiwa vipi, darasa la kwanza, Quran class, form six, digrii au *masters*. Kwa hivyo, hiyo elimu ni ipi. Mhe. Spika, mimi napendekeza tuiweke wazi wazi kwamba angalau elimu ya kiwango cha diploma. Ukisema elimu kuna wengine wana elimu ya uchawi tu, je tumchague mtu huyo awe Mwenyekiti wa Bodi, kwa sababu ana elimu ya fani ya ungo, ni lazima tuweke elimu ambayo isiyopungua kiwango cha diploma ili aendane na dunia ya leo.

Mhe. Spika, chengine ni kifungu cha 11(d), naomba Mhe. Spika, ninukuu;

Kifungu cha 11(d)

> "Upatikanaji rasilimali na kuhakikisha matumizi yanayofaa ya rasilimali hizo ikijumuisha kuidhinisha bajeti ya mwaka na bajeti ya ziada ya shirika".

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri kwamba lazima bodi iwe na kazi hiyo, lakini natoa indhari hapa kwamba Mhe. Spika, kuna baadhi ya bodi zimekuwa ni chanzo cha kuhujumu fedha za shirika. Sisi Wajumbe wako tunapotembelea baadhi ya bodi, huwa unagundua hasa kuwa ndio chanzo cha kuharibu na kugharimu fedha shirika. Kwa hivyo, licha ya kuwapa bodi uwezo wa kutafuta hizo rasilimali, lakini vile vile tuwasimamie ili rasilimali hiyo itumike kwa mujibu wa lengo la shirika, badala ya kuwa chanzo cha kuharibu fedha hizo.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu hicho hicho cha 11(2) kuna;

Kifungu cha 11(2)

> "Bodi itakuwa ni mamlaka ya kuidhinisha dhidi ya shirika na itachukua hatua za kinidhamu dhidi ya mfanyakazi yeyote".

Mhe. Spika, mimi nashauri kwamba isiwe mfanyakazi tu, lakini bodi pia iwe na jukumu la kumshughulikia mjumbe mwengine yeyote wa bodi kama atafanya kosa. Tumegundua kuna baadhi ya bodi wajumbe wenyewe ndio chanzo cha kuhujumu mali za shirika. Kwa hivyo, lazima bodi isimamie mfanyakazi wa kawaida, lakini pia iwatie hatiani wale wajumbe wa bodi iwapo watakiuka taratibu.

Mhe. Spika, tumegundua baadhi ya bodi huwa wanatoa maagizo kinyume na taratibu za shirika na watendaji wetu wanalazimika kukusanya matendo ambayo sio sahihi kwa mujibu wa sheria na hatimaye fedha za umma zinapotea kiholela. Kwa hivyo, bodi pia iwe na jukumu la kuwashughulikia wale watendaji wa bodi ambao wanatoa maagizo kinyume na taratibu ambazo zimewekwa.

Mhe. Spika, kifungu cha 12(2) (a) uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, "mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa (a) imesema ni muhitimu kutoka chuo kikuu kinachotambulika na taasisi inayolingana".

Mhe. Spika, tusiandae mswada kwa kumlenga mtu, SUZA hivi sasa inaandaa diploma ya IT na ni chuo kikuu SUZA. Tunguu ni chuo kikuu, kwa hivyo tuweke shahada ya kwanza angalau kwenye chuo kikuu itatambulikana, lakini ukisema muhitimu wa chuo kikuu, vyuo vikuu vyengine wanatoa programu ndogo ndogo za vyeti, diploma na hata *entrepreneurship*. Hivi mimi nimalize mtihani wa *entrepreneurship* halafu baadae unipe ukurugenzi. Kwa hivyo, lazima tuweke elimu angalau ya digrii ya kwanza katika chuo kikuu kinachotambulikana, tukiweka hivi maana yake mnamlenga mtu mwenye diploma yake ya kawaida kwa kuwa amesoma Tunguu au SUZA baadae mumpe nafasi hiyo Mhe. Spika, shahada ya kwanza katika dunia ya leo.

Mimi najiuliza Mhe. Spika, ni lini mtawaajiri Wazanzibari ambao hivi sasa wanahitimu kila mwaka zaidi ya 3000 hapa Zanzibar kwa digrii ya kwanza. Kwa hivyo, musiandae mswada kwa kumlenga mtu kwa ajili ya ajira fulani au wekeni digrii ya kwanza angalau ili awe Mkurugenzi

Mkuu wa shirika, shirika ambalo mnakusudia kufanya ushindani nje na ndani ya nchi yetu. Mhe. Spika, nashukuru sana.

Mhe. Spika, kifungu chengine ni kifungu cha 13(2) naomba ninukuu;

Kifungu cha 13(2)

"Shirika kwa ajili ya kurahisisha utendaji wa shughuli zake chini ya sheria hii, linaweza kuanzisha".

Mhe. Spika, mimi nashauri kwamba "litaanzisha", hii "linaweza" tusilishutize, lakini tulazimishe. Kwa nini Mhe. Spika. Tumegundua vile vile kuna baadhi ya mashirika wanakwepa kuanzisha vitengo idara za ukaguzi bila ya kuwa na idara ya ukaguzi ndani ya shirika, maana yake ni kuhujumu fedha za umma na kwa hivyo watendaji wetu wa mashirika wanakwenda idara hii kwa sababu sheria haiwalazimishi. Kwa hivyo, nashauri kwamba lazima sheria ilazimishe kuweko idara, tena ikiwezekana itajwe hasa miongoni mwa idara hiyo ni Idara ya Ukaguzi wa Ndani ya Shirika, ili kusaidia kudhibiti upotevu wa mali za shirika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo, ninasema tu kwamba kifungu cha 19 nipate ufafanuzi, naomba ninukuu;

Kifungu cha 19

> "Bodi kwa kipindi kisichozidi miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha kitawasilishwa kwa Waziri na kwa kamishna taarifa za mwaka kwa mwaka huo ikiwa na".

Sasa hii kamishna sijamuelewa kamishna wa nani, Kamishana wa *ZRB*, Kamishana wa Mitaji ya Umma au pia kuna kamisha hapa kwenye bodi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba nipewe ufafanuzi huo, baada ya hapo Waziri akinijibu vizuri mara hii nitakuwa laini kupitisha mswada huu, nakushukuru sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mawili au matatu katika mswada huu.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwenye madhumuni na sababu, tumeelezwa hapa kwamba madhumuni ya kuletwa mswada huu, kwanza ni kutekeleza sera ya usafiri ya Zanzibar. Lakini la pili ni kwamba hili Shirika la Meli lilikuwa liko chini ya tamko la Rais, kwa hivyo lilikuwa halina sheria. Pia lilikuwa halina mamlaka, lilikuwa chini ya serikali likipewa maelekezo, lilikuwa halimiliki wala halifanyi chochote. Kwa hivyo, kuanzishwa kwake ni kuliboresha na kulipa uwezo wa kufanya mambo yake kwa uhuru na ufanisi zaidi, hili ni jambo la busara sana.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwenye sehemu ya tatu ya mswada huu na kwenye kifungu cha 11 na huu ni uwezo wa bodi. Ukiangalia katika kifungu cha 11(e) kinasema;

Kifungu cha 11(e)

"Kutunga na kusimamia kanuni za utumishi na za fedha za shirika".

Mhe. Spika, uwezo huu wa bodi nadhani hautakuwa sahihi, kwa sababu kuna tume ya utumishi serikalini ambayo ndio yenye mamlaka ya kutunga kanuni za utumishi, kwa kweli na bodi hii ukiipa kazi hiyo, kuna hatari sasa kanuni za Tume ya Utumishi Serikalini na kanuni ambazo zitatungwa na bodi zikaja kugongana siku moja na ukawa ufanisi haupatikani. Kwa hivyo, nadhani kifungu hiki bodi isipewe, kwa sababu tayari tume ya utumishi imeshatayarisha kanuni na kila kitu kwa ajili ya utumishi. Vyenginevyo, labda Shirika la Meli liwe na tume yake ya utumishi, lakini kama wanatumia mtiririko ule wa ajira za kawaida za serikali, basi nafikiri tume ya utumishi inatoka kupanga mipango ya utumishi na bodi isipewe tena kazi hii. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kifungu kile tafadhili kifutwe.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, nije kwenye kifungu cha 13, hapa kuna uteuzi wa Afisa Mwandamizi. Hiki kifungu kinasema;

Kifungu cha 13

"Kwa kuzingatia masharti ya sheria ya utumishi wa umma".

Hapa *concern* yangu ilikuwa inajenga hoja kule juu kumbe, nilikuwa nimeweka alama hapa kwamba hiki kifungu cha 13 kina-*reflect* kwenye yale masharti ya sheria ya Utumishi wa Umma, ndio yatakayotumika kumpata huyu Afisa Mwandamizi. Lakini huku juu bodi inatakiwa iunde kanuni.

Kwa hivyo, nilikuwa nadhani hata ukiangalia hiki kifungu cha 13 kinatosha kuona kwamba kanuni zinazofaa ni zile zile za Utumishi wa Umma. Kwa hivyo, hicho kifungu ndio nilikuwa nasisitiza ni afadhali kikaondolewa.

Mhe. Spika, uwezo wa waziri katika kifungu cha 14 kinasema;

Kifungu cha 14

"Waziri anaweza;

(a) Kutoa maelekezo ya jumla au maalum kwa bodi kuhusiana na utendaji wa shughuli za shirika na matumizi ya uwezo wa shirika.

Sasa hapa nilitatanishwa na lugha kidogo, inaonekana kama haisomeki vizuri, labda kuna maneno pengine hayajapangika vizuri. Kwa hivyo, nilikuwa napendekeza mimi isomeke kama hivi inavyofuata;

> "Kutoa maelekezo ya jumla au maalum kwa bodi kuhusiana na utendaji wa shughuli za shirika na matumizi kulingana na uwezo wa shirika", halafu litiwe tena neno "na bodi itasimamia maelekezo hayo". Nadhani ikisomeka hivi itakuwa inasomeka vizuri zaidi.

Nafikiri Mhe. Waziri atakuwa kaiona hiyo, ni lugha iliyotumika, hapa sina hoja nzito ila ni lugha iliyotumika inafanya hiki kifungu kisisomeke vizuri na lugha nayo ina sehemu yake Mhe. Spika, katika kufahamu kilichokusudiwa.

Nikitoka hapo niende kwenye kifungu hicho hicho cha 14(c),

Kifungu cha 14(c)

> "Uwezo wa waziri", unaendelea huo "kutoa miongozo maalum kwa bodi kuhusiana na suala lolote linalohusisha makubaliano na au maslahi ya nchi yoyote".

Mhe. Spika, mimi sijafahamu hasa kilichokubaliwa ni kitu gani hapa. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja anifafanulie kidogo. Nilisomasoma nikaona sifahamu nikasema bora niulize.

Mhe. Spika, kifungu cha 17 kinahusu mahesabu na ukaguzi. Sasa hapa shirika litahifadhi vizuri madaftari ya mahesabu na si zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa kila mwaka wa fedha litatayarisha;

(a) Taarifa za mapato na matumizi ya mwaka huo wa fedha;
(b) Taarifa na rasilimali za madeni ya shirika;
(c) Taarifa nyengine zozote kama inavyoweza kuhitajika.

Lakini ukisoma kifungu cha 2 kinasema mahesabu ya shirika ya kila mwaka wa fedha yatapaswa kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi aliyeteuliwa naye. Hii ni sahihi kidogo, lakini ina mapungufu kwa sababu sheria inazitaka taasisi za umma, miezi mitatu baada ya mwaka wa fedha iwe tayari imeshapeleka mahesabu yake kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sasa hiki kifungu hakikutoa maelekezo hayo, kimeeleza tu kama hesabu zitapelekwa, lakini kimeacha huru. Matokeo yake kinachotokea ni kwamba kwa sababu sheria hii haijafunga basi Shirika la Meli linaweza kupeleka mahesabu yake kwa mkaguzi siku yoyote litakapoona sasa wakati umefika. Lakini nilikuwa napendekeza mimi ule utaratibu wa miezi mitatu basi uandikwe katika kifungu, na kwa maana hiyo basi kifungu cha 2 kibadilishwe kisomeke kama hivi ifuatavyo:

Kifungu cha 2

> "Mkurugenzi Mkuu sio zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha atayapeleka mahesabu yote ya shirika kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali".

Hii italeta yale matakwa ya sheria ya ukaguzi kwamba yawemo ndani ya miezi mitatu na si zaidi ya hapo. Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri afanye marekebiso hayo.

Kifungu cha 18 Mhe. Spika, kinahusu uwekezaji wa shirika, taasisi zetu hasa mashirika ya umma haya, yatapewa nafasi yatakapoona yana fedha za kutosha zisizohitajika basi yaweze kuwekeza katika taasisi tofauti. Lakini Mhe. Spika, kilichonitisha hapa ni kwamba Shirika la Meli limepewa uwezo wa kufanya hivyo hata nje ya Zanzibar. Kwa mfano, linaweza siku moja likajikuta limepata faida kubwa kama milioni 5 au milioni 10 zimekaa hazina matumizi ndani ya shirika, wakaamua kuziwekeza mfano kwenye mabenki kwa ajili ya kupata *interest* na mambo mengine. Lakini sasa wamepewa uwezo wa kuwekeza mpaka nje ya Zanzibar, kitu ambacho mimi sidhani kama ni kizuri kwa sababu hapa kwetu Zanzibar tuna benki yetu ya watu wa Zanzibar, ambayo inahitaji sana kupata mambo kama haya. Kwa hivyo, ukiwapa uwezo shirika wa kwenda kuwekeza pesa hizi Ulaya, zitakuwa hazitusaidii sisi hapa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba haya maelezo ya kuwa ndani au nje ya Zanzibar, basi yabadilishwe na iwe wanaweza

kuwekeza katika taasisi ziliopo hapa hapa ndani ya Zanzibar yetu, ili hizi pesa zikipita hapa itakuwa inatusaidia. Nafikiri watu wa mabenki wanajua habari hii.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye kifungu cha 19 ambacho kinazungumzia habari ya taarifa za mwaka za bodi. Sasa ukisoma hiyo aya (b) inasema taarifa ya maelekezo yote yaliyotolewa na Waziri wa shirika chini ya sheria hii katika mwaka huo. Yaani hayo yatawasilishwa kwa waziri, lakini sasa hayasomeki vizuri, kwa sababu waziri mwenyewe ndiye aliyetoa taarifa ya maelekezo kwa shirika, halafu uyakusanye yale maelekezo yake yote umpelekee mwenyewe mwisho wa mwaka, mimi nadhani sio sahihi. Sahihi ni kumpelekea waziri utekelezaji wa yale maelekezo aliyoyatoa, lakini sio kukusanya taarifa za maelekezo ukampelekea.

Kwa hivyo, nalo hili ni tatizo la kiuandishi, lugha hapa haijatumika vizuri. Nafikiri sahihi zaidi ni kusema taarifa ya utekelezaji, hilo neno "ya utekelezaji" ambalo hapo halipo, nilikuwa naomba liongezwe hapo ili maana yake ionekane kama waziri anapelekewa taarifa ya utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na waziri, kwa sababu waziri akishatoa maelekezo, anachohitaji yeye yale maelekezo yafanyiwe kazi na halafu apelekewe taarifa za utekelezaji wa yale aliyoyaelekeza, nafikiri nitakuwa nimefahamika. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hayo maneno yaongezwe hapo ili hiyo sentensi iweze kuleta maana vizuri.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu ni mzuri na nafikiri wajumbe wakiukubali na ukiwa sheria, basi tunaweza tukapata ufanisi mkubwa sana wa Shirika letu la Meli na hatimaye kuondokana na yale matatizo ambayo tumekuwa tukikabiliana nayo mara kwa mara ya usafiri wa baharini.

Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi naukubali mswada huu baada ya marekebisho hayo, nadhani Mhe. Waziri amenisikia. Naukubali Mhe. Spika, kwa asilimia mia kwa mia, ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipata fursa ya kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenye Mungu mwingi wa rehema kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutujaalia hazina ya afya na uwezo wa kuondoka katika maeneo yetu hadi hapa. Kwa kweli hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Spika, natumia fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia hoja iliopo mbele yetu.

Kwanza napenda niipongeze serikali kwa kuleta mswada huu, kwa kweli mswada huu umekuja wakati ndio, yaani umekuja wakati muafaka kwa sababu wakati hivi tunazungumza Mhe. Spika, hii sheria kama tulivyoambiwa kwamba Shirika la Meli lilikuwepo kwa *Presidential Decree* ya mwaka 1983 na ilifutwa na sheria nyengine hapa.

Sasa tangu kipindi hicho kwa kweli hakukuwa na chombo cha nchi ambacho kilikuwa kinasimamia usafiri wa baharini na hili ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Spika. Kwa hivyo, kwa kuwa sisi hapa ni kisiwa asilimia kubwa ya wazanzibari tunategemea usafiri wa baharini, sasa leo hakuna chombo kinachosimamia usafiri wa baharini kwa miaka yote hii tokea mwaka 1983 hadi leo hii na hili ni tatizo Mhe. Spika.

Kwa hivyo, nadhani kwa uzembe huu wa serikali ndio tukapata matatizo mengi hayo yaliyotupata huko nyuma yakiwemo ya maafa pamoja na meli zetu kuwa zinapotea fedha za walipa kodi. Kwa mfano, MV. Mapinduzi iliuzwa na baadaye tuliambiwa imezama, MV. Maendeleo ilikuwa inakodishwa huko na kule na wala hatujui fedha za walipa kodi zinakwenda vipi. Vile vile juzi tu ile meli yetu ya mafuta hatujui hata iko wapi MV. Ukombozi, MV. Uhuru almuradi hakuna chombo.

Sasa kuletwa kwa sheria hii nadhani sio tu kwamba shirika hili litaweza kusimamia usafiri wa vyombo vya baharini, lakini hata kudhibiti vyombo hivi. Mhe. Spika, kwa mnasaba huu naomba niunge mkono sana mswada huu na ninaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu waunge mkono. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kidogo niende kwenye kifungu cha 3(3) (d) naomba kunukuu.

Kifungu cha 3(3) (d) kinaeleza hivi:-

> "Shirika litakuwa na hadhi ya kisheria na linaweza kuingia kwenye mikataba yote kama itakavyolazimika na ufanisi wa utekelezaji wa malengo yake chini ya sheria hii na sheria nyengine yoyote".

Mhe. Spika, tukiangalia kipengele hichi cha 3(d) na kipengele cha 4(1) na kipengele cha 5 unakutia kuna *contradiction* ya hii sheria kidogo, kwa sababu shirika hapa linaweza kuingia mikataba, lakini ukija kwenye namba 4 muhuri wa shirika unakutia ni bodi ndio yenyewe dhamana hii kama alivyosema Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa pale mwanzo. Halikadhalika kwenye makao makuu ya shirika uwezo wa kufungua afisi ndogo kwenye kipengele 5 haikupewa shirika na imepewa bodi.

Kutokana na hali hiyo, nadhani shirika ni kulinyima uwezo kwa hali hii Mhe. Spika, naomba kwamba uwezo wa shirika ungekuwepo kwenye kifungu 4(1) na 5, yaani kifungu cha 4(1) kutakuwa na muhuri wa shirika ambao muundo na namna yake ni kama ilivyoelezwa na kuamuliwa na shirika na isiwe bodi.

Vile vile kwenye 5 Makao Makuu ya Shirika yatakuwa Zanzibar na inaweza kuanzishwa afisi ndogo, mawakala au wawakilishi ndani ama nje ya Zanzibar katika sehemu ambazo zitaamuliwa na shirika na isiwe bodi. Kwa hivyo, haya kwa upande huo namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika aangalie hapo, kwamba shirika lipewe uwezo zaidi kuliko bodi. Kwa hivyo, kwenye kipengele cha 4(1) na kile cha 5 uwezo huu uwe ni wa shirika na wala usiwe wa bodi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye kipengele cha 10(2) (a) cha mswada huu kwenye Bodi ya Wakurugenzi. Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais, sifa za Mwenyekiti huyu lazima kwanza Rais kabla ya kumteua awe na uzoefu mkubwa katika kuongoza mashirika ya umma mbali na taaluma na uwezo huo awe nao, kwa sababu mashirika mengi Mhe. Spika yanakufa kutokana na uongozi wake kuwa hafifu. Sasa katika uteuzi huu lazima Mhe. Rais asichukue tu mtu, lakini lazima aangaliwe ni mwenye uzoefu mkubwa katika kuongoza mashirika ya umma na kwa kesi hii, basi ni vyema awe na uzoefu katika mambo ya *Marine Science*, ili aweze kulisaidia shirika hili.

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie kipengele cha 12(2)(a)(b)na(c) vinazungumzia kuhusu uteuzi pamoja na sifa za Mkurugenzi Mkuu. Kwa hivyo, Mkurugenzi Mkuu ndiye atakayekuwa mtendaji Mkuu wa Shirika na kwa kweli yeye ndiye atakayekuwa *technical advisor* wa shirika hili.
Miongoni mwa sifa zake awe ni muhitimu kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika na taasisi inayolingana. Mhe. Spika, nadhani hapa ingetajwa hasa elimu isiyopungua *degree* ya pili katika masuala haya ya sheria, lakini zaidi ingekuwa mambo ya *navigation* angesaidia sana.

Lakini kumwambia mtu wa *degree* ya mwanzo tu, kwa mfano unamtoa kijana mwenye *degree* ya mwanzo na kumpa shirika kubwa kama hili na wala hana uzoefu. Kwa hivyo, nafikiri shirika hili tunawakabidhi vijana na jambo ambalo litakuwa ni tatizo.

Mhe. Spika, naomba sana hapa kwamba Mkurugenzi Mkuu sifa yake moja awe na taaluma ya *degree* ya pili na wala sio *degree* moja na itajwe hasa kwamba awe na *masters degree* kwenye hizi fani zilizotajwa humu na wala isiambiwe tu kwamba amemaliza Chuo Kikuu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kuendelea kumuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa kweli sheria hii ni muhimu sana na imekuja wakati ndio. Kwa hivyo, kwa vyovyote vile ahakikishe kwamba itakapopita sheria hii basi lazima usafiri wa baharini iweze kusimamiwa vilivyo, kwa sababu hivi sasa wakati tunazungumza Mhe. Spika kuna mashirika mengi ambayo yameanzisha usafiri wa baharini tayari yameanza kupotea.

Kwa mfano, hapa tulikuwa na *Sea Express, Sea Stars* zinaanza kupotea, kwa sababu hakuna chombo cha kusimamia vyombo vyao. Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika katika hili mara baada ya kupita sheria hii basi tuhakikishe kwamba meli zetu zinapata usimamizi mkubwa na usafiri kuwa hauna matatizo pamoja na kusafiri vizuri na wala sio kusimamia vyombo tu Mhe. Spika, kwa sababu vyombo peke yake havifanyi safari hata siku moja lazima kuwe na wasafiri.

Sasa ili kurahisisha usafiri baharini ni wale wasafiri kuweza kupata usafiri bila ya matatizo, lakini kwa sababu sheria hii ilikuwa haipo watu wanasumbuka sana kusafiri katika nchi hii Mhe. Spika na kupata usumbufu hawapati tiketi na kupelekea kulanguliwa kwa sababu ya kukosa hivi Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, naomba sana katika hili, ili ku-*modify* shirika pamoja na usafiri wa baharini namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika akae pamoja na Mhe. Waziri

anayeshughulikia mambo ya vitambulisho ambaye amekaa naye jirani tu pale, ili waangalie uwezekano wa kuwapatia vitambulisho hawa wasafiri wetu kwa ajili ya kuweza kusafiri kirahisi.

Kwa kweli inasikitisha sana Mhe. Spika, kwamba leo mtu anakwenda pale akiwa hana *ZID* kuna walanguzi ambao tayari wameshanunua tiketi kwa ajili ya kufanya ulanguzi na hiyo si haki Mhe. Spika. Kwa hivyo, nadhani kwa sababu mupo jirani hapo basi mutakaa pamoja na kuweza kui-*modify* hii sheria vizuri kwa ajili ya kuwapatia hawa wasafiri, ili waweze kusafiri katika hizi meli zetu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia kuja hapa leo, tukiwa wazima wa afya na pia kuendelea na shughuli zetu za kawaida zilizotuleta hapa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wetu.

Vile vile Mhe. Spika nakushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuweza na mimi kuchangia machache katika mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutuletea Sheria hii ya Kuanzisha Shirika la Meli ikiwa na lengo la kuleta ufanisi katika usafiri wa baharini wa hapa kwetu.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi kwanza kabla ya yote kwa sababu sina mengi ya kusema, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, na mimi katika dondoadondoa yangu nimeona kuna baadhi ya mambo kidogo ambayo ningependelea kuya-*highlight*, ili kama kuna uwezo haya mambo kuyaangalia tena basi tuyaangalie tena.

Moja kwa moja nianze kifungu cha 3 cha mswada huu kinachozungumzia suala zima la kuanzishwa kwa shirika. Katika kifungu cha 2 Mhe. Spika, inaeleza kuwa shirika litakuwa na hadhi ya kisheria na maneno kwenye mswada wangu yamefutika, lakini kuna a, b, c, d na nyengine.

Kwa hivyo, mimi nina wazo tu, kwa sababu hakuna shirika ambalo halina nembo maalum na hapa kuna muhuri, aidha sijui kama muhuri ndio umekusudiwa nembo. Lakini ningeshauri kwamba kuwe na nembo na muhuri, kwa sababu nembo sote tunajua kwamba katika mashirika yetu pamoja na afisi zetu za serikali zote zina nembo. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba kuwe na nembo pamoja na muhuri ambao utatumika katika shughuli za shirika hilo.

Jengine Mhe. Spika, nakwenda kwenye kifungu cha 8 ambacho kinazungumzia suala shirika katika kutekeleza shughuli zake chini ya sheria hii, litakuwa na uwezo ufuatao. Mhe. Spika, katika kifungu cha ‘a’ imeeleza kwamba shirika litamiliki, litanunua, litakodi au kukodisha ama kuzuia, kuweka rehani, kuuza. Kwa kweli kuna kitu ambacho nimekiona hapa kinakosekana kwamba shirika kuwa na uwezo wa kufanya ubia na shirika au taasisi nyengine yoyote hapa kimekosekana.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kwa hili pia aliangalie, kwa sababu wanao uwezo wa kumiliki, kununua, kukodi, lakini katika suala la kufanya ubia hapa halijatajwa sijui kwa sheria za shirika sijui kama kuna uwezo ambao shirika linaweza kufanya ubia na shirika au taasisi nyengine kwa ajili ya kufanya shughuli zake.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye kifungu cha 10 ambacho kinaelezea kuhusu utawala na uongozi wa shirika.

Mhe. Spika, nimegundua mara nyingi sana tunapokuwa na bodi hizi *consistence* ya Wajumbe wa bodi mara nyingi inakuwa inaangalia sana kwa upande wa serikali. Kwa kweli mimi naunga mkono ushauri uliotolewa na wenzetu kamati kwamba katika bodi hii kuwepo na watu au wajumbe ambao wanatoka kwenye taasisi binafsi, kwa sababu kama tunavyofahamu wadau wakubwa wa shughuli hizi za usafiri wako katika taasisi binafsi. Kutokana na hali hiyo, naomba kushauri kwamba wajumbe hawa wawili wanaobakia, basi wawe ni wajumbe kutoka taasisi binafsi.

Vile vile kwenye hicho cha 10(4) kama walivyotangulia wenzangu kinaelezea kuhusu sifa za Mwenyekiti. Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri kwamba hapa kingeelezwa kidogo cha elimu alichofikia pamoja na umri wa uzoefu wake.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye ukurasa wa 306 ambao unazungumzia masharti ya fedha. Kwa kweli hapa nayaona masharti ya fedha pamoja na masharti ya jumla ambayo yamewekwa vizuri sana. Masharti haya ni mazuri, lakini nina khofu katika utekelezeji wake na wala sio kama hayatekelezeki, lakini wanaotekeleza masharti haya watakuwa wagumu katika kumsaidia *CAG* wetu.

Mhe. Spika, wewe mwenyewe ni shahidi tulikuwa kwenye semina hivi juzi na tumeyazungumzia masuala haya. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika awaeleze watu wake kwa hivi sasa umefika wakati wa uwazi na wala hakuna sababu ya kuficha mambo, kwa sababu ukificha ina maana unaficha ubaya. Kwa maana hiyo, hakuna sababu ya kuficha taarifa zote zinazohusiana na hesabu za shirika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Spika katika sheria hii hasa kwenye shirika, kwa sababu tumeona mashirika yetu mengi sana yamekufa au yameshindwa kufanya kazi kwa sababu ya udhaifu wa kutekeleza masharti ya fedha ambayo yamewekwa kisheria. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naomba kumalizia Mhe. Spika kwa kumuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika katika mipango yake hii yote, basi kwenye pato lake ambalo litapatikana kuwe na asilimia fulani ambayo shirika itakuwa inatoa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii. Kwa kweli Mhe. Spika mashirika mengi yanafanya hivyo na wala humu sijaona na inawezekana itakuwemo, lakini itakuwemo kwenye kanuni na hilo ni muhimu sana, kwa sababu shirika hili litakuwa linaingiza.

Kwa hiyo, kwa kuwa litakuwa linaingiza na tayari tumeshaona mifano ya taasisi nyingi ambazo zinashughulikia masuala ya kuingiza fedha huwa zinachangia. Kwa maana hiyo, shirika hili pia nalo liwe na jukumu la kusaidia shughuli za maendeleo ya jamii.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache narejea tena kusema kwamba naunga mkono mswada kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, ahsante sana, kwanza na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kurudi tena jioni hii katika chombo chetu ambacho ni muhimu kwa taifa letu kwa mustakbali wa kutengeneza mambo yetu, ili yawe sawa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jinsi ya kuleta marekebisho ya mswada huu ambao ni wa kuanzisha Shirika la Meli.

Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao walimsaidia kurekebisha baadhi ya mambo kwenye mswada huu.

Mhe. Spika, nitaanza kwa kusema hivi kwanza kabisa nimpongeze sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba alisikia kilio cha wananchi katika Zanzibar hii, kuona kwamba imefika wakati badala ya meli zetu zile mbili kuwa hali hoi bin taabani, basi akaona kuna haja ya kuagiza meli nyengine mpya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, angalizo maana mimi nitachangia kijumlajumla tu. Kwa kweli tulikuwa na meli zetu mbili hapa ambazo ni madhubuti na wala sifikiri kama tutapata meli nyengine kama zile. Lakini kutokana na watu wetu ambao waliona meli zile ni kama zao na si za serikali wala wananchi basi ziliangamia nathubutu kusema hivyo Mhe. Spika. *(Makofi)*

Sasa niseme kwamba mswada huu umeeleza mambo mengi. Lakini mimi niiombe serikali kupitia kwako Mhe. Spika, sisi hujaribu kufanya mambo yetu, lakini hatuna wataalamu wa kutosha kwa ajili ya kuendesha mambo yetu.

Kutokana na hali hiyo, basi niiombe serikali kupitia kwako Mhe. Spika kwa heshima zote, kwamba hivi sasa imefika wakati tubadilike kama anavyosema mwenyewe Mhe. Rais. Meli tayari imeshaagizwa na wala sijui kama tunao wataalamu wa kutosha hapo itakapofika meli kuweza kuihudumia.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kama tunao basi tuwape ujuzi zaidi na ikiwa wapo kidogo tuwaongeze, ili shirika hili liweze kuja kufanya kazi zake ipasavyo.

Mhe. Spika, naomba kusema na kutahadharisha kwamba kitu kikubwa ni usimamizi wa mambo yetu, uaminifu, uangalifu kwa sababu hapa kidogo tunapwayapwaya.

Mhe. Spika, naomba niseme wazi kabisa tunapokuwa na kitu tukaunda shirika au mamlaka ama nini, lakini kunakosekana jambo muhimu la uaminifu Mhe. Spika, kwa sababu mtu anakifanya kile chombo kama ni chake, lakini anajisahau anakula na wala hali isipokuwa anafakamia. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, tuwe na utaratibu wa kuhakikisha watu wetu wanakuwa na uaminifu wa hali ya juu na usimamizi uwepo. Mhe. Spika, usimamizi katika mswada huu hautakuwepo kama hatuna wataalamu ambao wamebobea, tusijetukachukua mtu kwamba ni baharia tu amekaa ubaharia miaka 15 au 20 tukasema tunampa dhamana.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu bodi na hapa niunge mkono mazungumzo ambayo wamezungumza wenzangu. Lakini hasa kwenye shirika lenyewe Mhe. Spika tuwe waangalifu kweli tutafuta mtu ambaye ataliwezesha shirika hili kuliendesha ipasavyo.

Mhe. Spika, wenzangu wametoa mifano mbali mbali tena ni mifano ambayo imetokezea na iko hai na wala si ya kubuni. Mhe. Mgeni Hassan Juma amezungumza na kutoa mifano mizuri pamoja na wale wengine ambao waliochangia.

Sasa mimi niiombe tena serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba tuwe makini na mambo yetu na tuhakikishe tunajituma, tunasimamia ipasavyo pamoja na kuhakikisha kwamba tunafanya kitu ambacho wenyewe wananchi watafurahia na wala tusije tukafanya mambo siku ya pili wananchi wakaja juu.

Kwa hivyo, naomba sana mswada huu wa marekebisho tukesha kuupitisha, basi Mhe. Waziri na Naibu wake wakae na kutafakari haya maelezo ya Waheshimiwa Wajumbe waliyoyatoa katika Baraza hili tukufu. Mimi nimesema nichangie kidogo tu ili tujifunze kwa mambo ya nyuma yaliyopita tusije tukayaendeleza kwa kipindi hichi. Lazima tubadilike.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, niunge mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Spika, na mimi nashukuru Magharibi haya kunipatia fursa ya kuzungumza machache kuhusu mada hii iliyokuwepo mbele yetu. Juzi tu tulikuwa tunapitisha sheria ya kuanzisha usafiri wa baharini, lakini leo bahati nzuri, bahari tayari, usafiri wa bahari tayari, sasa tunaanzisha shirika la kuweka hiyo meli ya kusafirisha hao watu. Imekuwa vizuri sana kwamba kwanza imekuja ardhi baadaye imekuja miti na ndio dunia ilivyoumbwa.

Mhe. Spika, kama walivyopita wengine na mimi sitokuwa na mengi isipokuwa nafurahia tu kwamba serikali imeona kwamba upo umuhimu sasa wa kuwa na shirika madhubuti. Kwa kuanza labda ningekwenda katika utawala na uwongozi wa shirika. Nikiangalia hapa nawakuta wajumbe wa aina tofauti ambao wataunda hii Bodi ya Shirika. Kuna mjumbe mmoja kutoka Wizara inayohusika na masuala ya meli.

Mhe. Spika, mimi kwa mawazo yangu nahisi mjumbe kutoka shirika la meli ameshapatikana akiwa ni Mkurugenzi Mkuu, nahisi hii nafasi ingekwenda kwa watu wengine. Nina imani kuwepo kwake kutakuwa na utawala fulani kwa sababu Mkurugenzi yupo na mtu mwengine yupo anayetoka shirika hili hili moja. Kwa hivyo labda angetafutwa mtu mwengine akawa ni mjumbe.

Lakini katika hili pia katika marekebisho kifungu cha 10 (2) (f) yameongezwa maneno kutoka sekta binafsi baina ya neno wawili na watakaoteuliwa. Nafikiri tukiweka moja kwa moja kutoka sekta binafsi haitupi maana ya kwamba sekta binafsi ya watu wanaoshuhulikia mambo ya meli. Ukisema watu kutoka sekta binafsi kwa vile hapa tunaunda bodi basi anawezekana akawa ni mjumbe yoyote tu yule. Sasa nafikiri tungeongeza maneno ikiwa kama tumekusudia kwamba sekta binafsi wanaoshughulikia masuala ya meli basi tukayaainisha kwamba wakawa ni watu wa sekta binafsi wanaoshughulikia mambo ya meli. Lakini kwa hivi Waziri anaweza akawa na fursa moja kwa moja tu ya kusema mimi huyu namtaka au huyu simtaki kutoka sehemu yeyote.

Nikiendelea hapo Mhe. Spika, kifungu cha 4, kama tunavyosema tunataka tuende na sayansi na ndio maana mambo yetu siku hizi hasa hawa wateuliwa tunakuwa tunawapa viwango fulani. Kifungu cha 4 kinasema:-

> Kifungu cha 4 "Mtu hatofaa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe na elimu na uzoefu katika mambo ya usafiri wa baharini, uongozi au utumishi wa umma"

Elimu kwa kwetu sisi hata ya darasa la kwanza la pili hata ya Qur-an tunaihesabu kwamba ni elimu. Nafikiri kwa karne tulikwisha kufika kwa kusema tu kwamba mtu awe na elimu basi wengi tunayo elimu, nafikiri ingefafanua zaidi hasa kwamba tunataka mtu awe na kiwango fulani, elimu ya chuo Kikuu au elimu gani. Mwenyekiti asiwe ni mwenyekiti tu kwa kutumia uzoefu hivi sasa. Tuna wenyeviti ambao tutawataka waende sehemu mbali mbali ya kupata *exposure*. Lakini kwa kuwa ni mwenyekiti tu kama mimi aliyekuwa hajui chochote, yatamshinda hayo.

Kwa hiyo tutafute mwenyekiti, ambaye sifa zake zitamuwezesha ukimwambia nenda Australia leo ukaangalie wenzetu wanafanya nini ataweza kwenda na akaweza kujifunza na akarudi na utaalamu, hivi tulivyoiweka inaruhusu mtu yeyote tu. Mimi nahisi hivi sasa tumetangaza sijui asilimia ngapi lakini tunajua kusoma na kuandika.

Mhe. Spika, leo tunakuja kama yalivyosema madhumuni ya kuanzisha shirika ambalo litakuja na mambo mapya zaidi. Kifungu cha 24 kinasema:

> Kifungu cha 24 "Utumishi wa muajiri au mfanyakazi "

Yaani baada ya kuanzishwa shirika hili utahamia moja kwa moja kutoka shirika lililokuapo na kuhamia shirika jipya. Nafikiri nia ya serikali ya kuleta hii ni kupata ufanisi zaidi. Nahisi tukiendelea na utaratibu kama huu hautokuwa wa busara. Shirika hili lililopo kabla ya kuanzishwa sheria hii tumeliona utendaji wake na watu waliopo ni wale wale, tumefikia wakati kwamba tukafikwa na majanga tukataka tupate kununua meli.

Mhe. Spika, nasikitika kusema kwamba sijui kuna mchango wowote unaotokana na Shirika la Meli ambalo tunataka kulifuta kwa sheria ile ya amri na kuanzisha shirika jengine. Hii ina maana ya kwamba kwa njia moja au nyengine watendaji waliokuwepo hawakuwa na ubunifu labda pengine hawakuwa na uwadilifu kiasi kwamba tufikie Shirika lisiwe na mfuko wowote ule. Kwa nini sasa serikali isiwatafutie watu hawa ikasema sisi turithi watu ambao nahisi ambao uwezo wao sio mzuri.

Mimi napenda ikiwa kwamba tuna nia ya kujenga shirika litakalokuwa na uwezo na ufanisi basi hawa watu tukawatafutia chao tukawapa, tukaanza upya kama inavyosema madhumuni yetu ya kujenga Shirika jipya ambalo litakuja na watendaji wapya na njia nyengine.

Mhe. Spika, kama umeosha nguo na nguo ile ikawa imekuwa ina maji ukataka kwenda kuianika kwenye uzi sehemu lakini ukakutia nguo ambayo ishakauka pale. Nguo ile mara nyingi utaratibu wetu ni kuiondosha ile iliyokwisha kauka, kwa sababu ile mbichi unayokwenda nayo ukiiweka pale pale ile itairowesha kwahiyo nayo itakuwa ipo katika hali mbaya. Lamsingi tungetafuta utaratibu wa serikali kuwawezesha hawa watu ambao wapo katika shirika, tukawapa chao ili kama tunakusudia kuanzisha shirika hasa jipya na madhumuni yetu yakawa ni hayo basi tutaanzisha shirika jipya na watendaji wakawa wapya.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi kwa heshima kubwa nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Mswada huu wa kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar na kabla sijatoa mchango wangu nataka nithibitishe kwamba Mswada huu naukubali kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, sasa hivi tunalo Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar, ni kwa nini leo tuko hapa tunajadili Sheria ya kuunda upya Shirika la Meli, uwakala umetolewa sasa hivi. Tupo hapa inaonekana kwamba sherikka la meli liliopo sasa hivi halikidhi haja, inawezekana kutokana na sheria yake iliyoiunda au hiyo amri ya serikali au ya Rais au kwa namna nyengine yoyote.

Mhe. Spika, Baraza lako hili tukufu kila bajeti inapokuja na hata kama si kipindi cha Bajeti, kipindi cha maswali na majibu basi wajumbe walikuwa wanaonesha kutoridhika kwao na walikuwa wana malalamiko makubwa hadi kufikia wakati mwengine kwamba hakuna haja ya kuwa na shirika hili na kwamba shirika hili lingevunjwa. Wajumbe watakumbuka kwamba hoja hizo zilikuwa zinatolewa. Wajumbe walikuwa hawatoi hoja hizi kwa sababu tu ya kuvunjwa, naamini walikuwa wanatoa hoja hizi kwa sababu waliona kama vile Shirika la Meli lilikuwa halipo.

Mhe. Spika, Shirika la Meli liliopo sasa hivi ambayo sheria yake hii ikipita litakuwa Shirika la Meli tunalolitarajia, linaendeshwa kwa shughuli ndogo ndogo za meli zenyewe. Kama tunavyojua sasa hivi kuna meli mbili tu zinazofanya kazi meli ya MV. Maendeleo ambayo inachukua abiria na mizigo kidogo, na meli hii spana mkononi. Miezi miwili inakwenda miezi mitatu imekaa. Shughuli hasa zinazoendeshwa sasa hivi na shirika hili ni shughuli mbili tu kubwa. Moja ni shughuli zinazotokana na uwakala wa meli. Uwakala wa meli hapa Zanzibar unafanywa na shirika hili tu, mwahali mwengine uwakala wa meli ni biashara huria, serikali inaingia na mashirika binafsi wanaingia, hapa kwetu ni bahati nzuri ni shirika la meli tu ambao limepewa kazi hii.

Imani yangu ni kwamba tungefungua milango na taasisi nyengine za binafsi kama tulivyofungua kwa usafiri wa baharini. Basi tusingepata kipato hicho ambacho uwakala wa meli wanachangia kwenye Shirika la Meli. Naamini huduma za watu binafsi zingekuwa nzuri zaidi na kwa hivyo zingevutia meli za nje zaidi kuliko za serikali.

Shughuli nyengine ambayo inaipa Shirika la Meli fedha ni kwa kukodisha meli ya mafuta MV. Ukombozi, ingekuwa si shughuli hizi mbili kukodisha meli na uwakala basi shirika hili lingekuwa haliwezi hata kufumbua macho. Kwa sababu shughuli za meli ya abiria, kupeleleka mizigo Pemba na Dar-es-Salaam zingekuwa hazipo kutokana na ubovu wa meli.

Mhe. Spika, nataka niwambie Wajumbe kwamba kwa sababu tunaanzisha Shirika, si jipya tunalianzisha upya tu lakini Shirika ni lile lile. Shirika la Meli lililokuwepo sasa hivi ambalo Mswada huu ukipita na Mhe. Rais akiusaini hata kesho, maana yake kwamba Shirika hili litakuwa limeanzishwa, lina upungufu mkubwa sana wa wataalamu. Hata sheria hii ikiwa nzuri kiasi gani bado tutasota, Shirika la Meli halina wataalamu wa kutosha, waliokuwepo ni wachache mno tena katika fani pungufu kweli kweli. Kwa hivyo ili hili liende vizuri basi suala la kupata wataalamu, si mwenyekiti wa bodi tu au Mkurugenzi Mkuu kuwa na Digirii mbili au tatu, hawa ni *administrative* lakini Shirika la Meli wenyewe ni wale watendaji wakuu. Ukisikia Capten, Baharia, hawa ni watu wanatakiwa wawe wamebobea katika ile fani.

Mhe. Spika, Shirika la Meli, lilikuwa na wafanyakazi wengi lakini wamepunguzwa kidogo kidogo mpaka sasa hivi nafikiri waliobakia ni kama asilimia 35 – 40 wengi waliopunguzwa sasa hivi wamekuwa na umri wa kustaafu si dhani kama wataweza kuajiriwa tena. Na kwa sababu walipunguzwa muda mrefu wengine wana zaidi ya miaka saba au minane basi hata ukiwapata tena hao ni kuwafufua upya. Siujui ni utaratibu gani utakaotumika katika kulifufua shirika hili upya. Mimi ningeshauri yafuatayo:-
Shughuli za usafiri baharini, shughuli za kuendesha vyombo, shughuli za ubaharia, kikosi cha KMKM kina wataalamu wengi sana. Ningeshauri sana baada ya sheria hii kuanzishwa na hata kabla ya Rais kuisaini, nina hakika Mhe. Rais tukishakuipitisha hapa yeye hana tatizo ataitia saini.

Kwa hivyo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ikutane haraka na Afisi ya Rais inayoshughulika na Vikosi wajipange mapema ni watu gani na gani wanaweza kuwa *seconded* na ikiwezekana hata kupatiwa mafunzo ya dharura. Kwa sababu hapa katika bajeti iliyopita Mawizara yote yalipunguziwa bajeti yao ili panunuliwe meli mpya ya serikali na naamini kwamba shughuli hizi hazitochukua muda mrefu sana, meli mpya itakuwa imepatikana. Lakini ikipatikana meli mpya hapa halafu huna wataalamu wa kutosha tutarudi pale pale. Kwa hivyo wataalamu hao kama watatokea KMKM au kwengineko popote pale wapatiwe *crash program* ili meli mpya itakapokuja na shirika hili limeundwa upya isiwe tena kutafutana ikachukua mpaka miaka miwili au mitatu bado tunakuja hapa tunalalamika.

Mhe. Spika, mimi sina *specific* vifungu, vimo viwili vitatu, nitavisemea, lakini nikuwa nataka nitoe indhari hii. Kwa sababu tukianzisha Shirika hili upya kila mtu atakuwa ana matumaini kwamba malalamiko yaliyokuwa yanatolewa na Wajumbe wa Baraza kama hayatoondoka moja kwa moja basi yatapungua kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, naomba kunukuu:

Kifingu 16 (2) "Mkurugenzi Mkuu anaweza ikiwa kuna haja ya kufanya hivyo kuwasilisha kwa Bodi makisio ya ziada"

Hii ni *supplementary budget*, mimi si mwanasheria lakini nilikuwa namsikia sana hapa Mhe. Ismail Jussa katika Sheria kuna *may and shall and will*. Sasa hapa kwa Kiswahili anaweza ni *may* sasa unapompa *open check* ya kwamba hata *supplementary budget* kwamba anaweza. Hapa Mheshimiwa ndio ule mwanya ambao tunautoa na watu wengine wasiokuwa waaminifu. Maana yake hatusemi kwamba watu wetu si waaminifu lakini wapo wengine waaminifu na wengine sio waaminifu. Hatujui Mkurugenzi Mkuu atakuwa nani muaminifu au si muaminifu, lakini ukimpa mwanya huu basi anaweza akafanya *supplementary budget* na kwa sababu kaambiwa anaweza kuipeleka akawa asiipeleke na wala huwezi kumkamata.

Mimi nilikuwa nashauri hapa iwe Mkurugeni Mkuu atawasilisha (*shall*) kwa bodi, kwa hivyo hapa kidogo itakuwa tumempeleka pahali ambapo lazima awasilishe hata kama ni *supplementary budget* ya milioni mbili au tatu. Kifungu kingeni ni:

15(2) "Mapato na Fedha ya Shirika yatahifadhiwa katika *account* ya shirika"

Mapato yanatiwa kwenye *account* vipi, sijui maana yake hapa hayakuainishwa maana kuna mapato na kuna fedha. Inaonekana haya mapato si fedha, sasa mapato ambayo si fedha yatahifadhiwa kwenye *account, unless* sio *account* ya *bank*. Naomba kifungu hichi kiandikwe *in such a way* kusiwe na mkanganyiko.

Mhe. Spika, kama nilivyosema sina mchango mrefu lakini katika sheria hii suala la uwakala wa meli limetajwa kijuu juu tu, hivi kama shughuli za meli. Mimi naona liko *very light*. Kwa sababu wakala wa meli sasa hivi ndio ambao unahuisha shirika lenyewe kwa mapato. Basi suala la uwakala wa meli lisingetajwa juu juu, yaani lingewekewa vifungu kama viwili vitatu hivi ili kuona ule umuhimu wa uwakala wa meli na si vibaya kama shughuli hii inaipa serikali fedha nyingi katika shirika hili, ikaonekana kabisa kwamba taasisi binafsi hawawezi na hawatakuwa na ruhusa. Maana yake limetajwa hivi hivi hakuna vifungu vizuri.

Mhe. Spika, huko mbele wajanja wapo kwa kutumia sheria hii hii, wakaleta hoja hapa wala si lazima hapa, watakapoona tu imeanzishwa. Sasa wakianzisha mashirika mengine ya binafsi uwakala, uwakala katika Shirika la Meli utakufa. Na hii ndio *one of the major source* ya *funds* kwa ajili ya shirika. Shirika hili hata kama la serikali lakini ina pande mbili. Kuna upande wa huduma kama serikali, lakini vile vile lazima lishindane katika biashara, vyenginevyo tutakuja hapa kulalamika maana haitakuwa na *funds* za kutosha. Kwa hivyo wanatafuna, wanapuliza. Waende kibiashara kwenye Shirika la Biashara ili waweze kuliendesha. Lakini vile vile wanahuduma huku kwa sababu hili ni shirika la serikali, haiwezekani meli ya serikali ikawa na bei kubwa zaidi kuliko bei ya binafsi, kama meli zenyewe zina viwango sawa sawa. Hili vile vile ni suala la kuliangalia.

Mhe. Spika baada ya kusema hayo narudia tena kusema naunga mkono mimi binafsi na wananchi wa jimbo la Ole, kwamba Mswada huu tuupitishe na Shirika hili lianzishwe haraka iwezekanavyo. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nataka nikupe mkono wa mwaka mpya mwaka wa Kiislamu mwaka 1434 wewe na wajumbe wenzangu.

Leo Mhe. Spika, nimefurahi sana, sana, sana na nataka nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na akiwa Makamo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Vipi anatekeleza ilani, wakati alipokwenda kuomba kura kwa wananchi alipokuwa Pemba alisema nikipata baraka nitafanya kila utaratibu kubadilisha mambo ya baharini na tutatanua meli. Nampongeza kwa sababu hadithi za meli ni za siku nyingi sana. Nakumbuka Profesa Ali Denge mwaka 2006 alileta hoja ya kununua meli, jawabu ndio hizo hizo inanuniliwa, inanunuliwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Bajeti ya mwaka huu wamekata kila Wizara na wamekusanya billion 17 yaani kila Wizara imebanwa na ukiibana Wizara unawabana wananchi. Kwa nini? Kwa ajili ya kununua meli. Ndio maana nikasema nampongeza sana Rais. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tulikuwa na meli nne, Meli ya MV. MAENDELEO. Mali ya MV. MAPINDUZI, meli ya MV. UKOMBOZI, meli ya MV. JITIHADA na meli ya MV. UHURU. Hizi meli ziliuliwa na serikali, lakini baada ya mapinduzi tulikuta meli Said Khalifa mwaka 1956 na meli MV. SALAMA ilijengwa mwaka 1957.

Baada ya Mapinduzi meli hizi zikachukuliwa na serikali. Said Khalifa ikaitwa MV. JAMHURI na MV. SALAMA ikaitwa MV. AFRIKA. Baadaye zikenda zake kama kawaida. Meli ya Mapinduzi ilitengenezwa mwaka 1974, meli ile ilitakiwa miaka 20 mpaka 2004. Lakini ilipofika mwaka 2000 meli ilikuwa taaban ilianza katika *plate* ikaanza matatizo. 2002 Baraza lako tukufu hili hapa Mhe. Abubakar alileta hoja kubwa sana kulilaumu Shirika hili na uchafu wa meli ya Mapinduzi, tukaunda kamati si teule kamati ya Baraza tukaenda Mombasa kufanya uchunguzi. Nilibahatika kuwemo katika kamati hiyo mimi, Mhe. Machano, Mhe. Saada Ali Mbarouk, Mhe. Hafsa, tulikwenda Mombasa tukakuta uchafu mwingi sana. Lakini ile meli tuliilazimisha tu, tusharudi tukapiga siasa, tukapiga hivi meli ile inatakiwa iende miaka 20 tukaipelekapeleka Mheshimiwa mpaka 2006 ikawa *grounded.* Lakini ile meli ilishikiliwa tu aaa inafaa brigedia Mwakanjuki alifanya meli nzima, leo hivi.

Lakini Mheshimiwa iliundwa Kamati kuchunguza meli ile, ile meli imetembea kwa miaka 8 baada ya kuwa muda wake umekwisha mapato yaliyopatikana kwa miaka 8 ni 2.0 bilioni, matumizi 4.6 bilioni tulipeleka waraka Baraza la Mapinduzi meli iuzwe. Meli ya Mapinduzi na Meli ya Maendeleo ziuzwe. Mhe. Haroun yule pale, Mhe. Haroun akaunga mkono kuwa meli ziuzwe hazifai tena zote mbili. Mhe. Machano akiwa ni Waziri akaomba akasema naomba MV Maendeleo niachiwe iende Mombasa ikafanyiwe ukarabati ikirudi iuzwe. Sasa haijawa hivyo, ile ikauzwa.

Nataka nichukue nafasi hii vile vile nimpongeze Mhe. Mwinyihaji Makame akiwa Waziri wa Fedha wakati huo na ndiye aliyesimamia uuzaji wa meli na meli iliuzwa kwa pesa kidogo sana, 410,000 dollars. Lakini meli mwaka 2003 ilishapata dola milioni moja lakini ikawa kuna mzozo tutauzaje meli inaitwa MV Mapinduzi, mpaka mwaka 2008 tulipokubali kuuza meli, meli imeuzwa kwa 410,000 dollars. Sasa nataka kusema hivi kuna pesa Mwinyihaji ameandika barua Shirika la Meli mimi nilikuwa Mwenyekiti, fedha zilizouzwa meli ni pesa kidogo sana lakini 410,000 ndio chanzo 17 bilioni na nyengine zichanganywe kidogo tu hizo, lakini nataka kutoa pongezi zangu kwa wote, kwa sababu jambo hili hasa zuri lakini sasa tunaunda Shirika.

Mhe. Haji Faki Shaali mwaka 2006 alisema marehemu mtarajiwa Shirika la Meli zipo *hansard.* Mhe. Rashid Seif tena jana nilipitia *hansard* zake mpaka hivi juzi juzi wakati limekuja agizo tusinunue meli amesema sana jasho limemtoka lakini leo anaongoza. Ninaamini hatokubali kudanganywa wala kuchezewa kwa sababu huyu ni mwenzetu ana uchungu, sasa Shirika hili ninamuomba Waziri wa Fedha ambaye ndie mwenye mali, Waziri wa Fedha alituita sisi wakuu wa mashirika, alituita sisi Shirika la Meli, Shirika la Mabasi, Shirika la Utalii haya matatu aliita watarajiwa na Peoples Bank, Bandari, Shirika la Bima na ZSTC.

Lakini ndugu Omar ndie aliyefanya *restructuring* ya Peoples Bank mpaka ikawa benki leo ndie Waziri wa Fedha ndie msimamizi na ndie mwenye dhamana wa Shirika hilo jipya litakaloundwa. Mimi nasema Shirika jipya litoundwa, lakini shirika jipya huwezi kuchukua pesa za wananchi 17 bilioni na meli itanarajiwa haitopungua 21 million dollars ukenda ukakabidhi shirika hili, hilo haliwezekani, tunajidanganya lazima ifanywe *restructuring* naomba Wajumbe wakubali sheria hii tuipitishe, lakini Rais atie saini, lakini uoza uoza wote leo Mhe. Spika, Shirika lina wafanyakazi sasa hivi 160 mpaka 270. Wafanyakazi 80 *administration*, wafanyakazi 70 ni *crews* yaani wafanyakazi wa Uhuru, imekufa, Mapinduzi imeshakufa, wafanyakazi wa Ukombuzi iko njiani, Maendeleo alhamdulillah wote wapo pale wamekaa tu tunataka kufanya *sign off* haiwezekani. Serikali lazima itenge fedha iwastaafishe wengi waondoke Shirika litengenezwe jipya, *restructuring* libaki watu kidogo.

Na kwa nini serikali iwe na meli ni muhimu sana serikali kuwa na meli na ndio maana Rais akaliona hilo na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukakubali bajeti zikatwe. Kwa hivyo hili, suala wakala sijui nini, hizo hadithi Shirika lile limekwisha. Shirika lile limepata viongozi wengi. Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alikuwa Mwenyekiti wa Bodi, Jabir Uki alikuwa Mwenyekiti wa Bodi, marehemu, Ali Issa alikuwa Mwenyekiti wa Bodi marehemu, Ramadhan Abdalla Shaaban yuhai, alipoondoka yeye akakaa Issa Ahmed ambaye leo ni mshauri wa Rais aka-*act.* Mwaka 2008 mimi nikachaguliwa na mimi nimemaliza muda wangu akaja Mwalim Haji ambaye alikuwa Mwakilishi mwenzetu.

Lakini katika uongozi wangu ndio nimeweza kuuza meli ya Mapinduzi. Katika uongozi wangu ndio tumefika ku-*sign memorandum of understanding* ya kuagizia meli. Kwa hivyo Shirika ninalijua nalielewa. Mwaka 2007, 2008 Mhe. Hamad Masoud akiwa upande wa upinzani na Mhe. Nyonje walikwenda Mombasa kulichunguza Shirika la Meli na ripoti zao wakaandika wakasema limeoza bovu halifai. Mungu akajaalia baadae Hamad akaja akawa Waziri pale. Mhe. Omar Yussuf wewe ndie Waziri wa Fedha kwa niaba ya Rais na wewe Shirika ni mali yako lisimamie jambo hili. Na hakikisha kabisa wala Mhe. Waziri usije ukadanganywa ukaleta jawabu hapa hazina msingi sijui shirika liko hivi linakwenda, hakuna.

Mhe. Mwinyihaji aliagizia mwaka 2007 kuwa atapeleka *auditors* kwenda ku-*check* Shirika la Meli hajapeleka. Naomba Serikali Mhe. Waziri upeleke kabla hiyo *restructuring* uende uka-*audit* Shirika zima lile matumizi yake, matumizi yote ili jambo jipya likija lije jambo la maana. *Otherwise* Mhe. Spika, wanasema samaki mmoja akioza wanaoza wote. Mimi naupenda ule msemo samaki akioza usimtupe ukimtupa mwenzako atamtia viungo umtamani lakini huyu hata viungo haingii.

Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban Waziri ameliongoza Shirika anajua ukweli, mimi nimeliongoza Shirika ninajua ukweli, Hamad Masoud alikuwa Waziri anajua, halafu suala la *man power* hakuna.Mwenyekiti anasema kuna wataalam kuna nini, lakini nilipomuuliza akanambia aa nilikusudia Shirika la Uwanja wa Ndege aa. Shirika la Meli

Mhe. Spika, hakuna *man power* kuna mtu mmoja tu ndio ana *first class. Chief Officer, Chief Engeneer* hakuna vitu vya maana kwa hivyo lazima serikali kwanza itenge fedha za kustaafisha halafu kufanya *training* kwa sababu hiyo meli taarifa nilizonazo mimi hiyo meli bado kwa hivyo meli itachukua kama miezi 18 au miezi 15. Kwa hivyo kuna wakati mzuri wa kuliandaa Shirika ili meli zikija ikabidhiwe lakini huwezi kukabidhi hivi lilivyo. Lakini lazima sheria ithibitishe ili serikali ipate nguvu lakini serikali lazima itenge fedha za kustaafisha, haiwezekani kungojea pesa hizi za bajeti no, no. no, serikali iweke fedha isafishe kabisa halafu ianze upya.

Kwa nini nikafurahi, juzi tulipitisha sheria ya ZMA Zanzibar Maritime Authority na tumeweka viwango meli kiwango fulani, kiwango Fulani. Mhe. Spika, katika meli leo sheria ile tumeondosha watu wanasema sheria isiweke kiwango, kwa sababu ile sheria Maritime haina kiwango. Mtoto wake Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kaandika *thesis* juu ya *maritime* kitabu safi kabisa kaeleza kachanua kila kitu sawa sawa. Lakini Mhe. Spika, leo tumeweka sheria miaka 15 lakini miaka 15 mwaka mmoja mimi kwangu si muhimu. *management, administration* ndio tatizo mwaka 2000 General Manager aliyeingia pale kazikuta MV Ukombozi, kaikuta MV Mapinduzi, amekuta MV Maendeleo na MV Uhuru. Leo zote mauti *we are not serious!* lakini leo kwa bahati mbaya au bahati nzuri meli nyingi zilizozama ni meli za watu binafsi na serikali ndio maana ikanunua meli mpya, kwa sababu meli mpya ina uzuri wake.

Lakini Mheshimiwa meli zilizozama nitakwambia Mhe. Spika. Kuna meli inaitwa Alrahman hii ilizama watu wengi hawajui, kuna Aziza 11 iliungua, Skagit ilizama, Pemba Muzdalifa ilizama, kwa nini zinazama, ndio maana tukaja mwaka 2003 tukataka kuunda sheria yetu ya *Shipping Merchant Act* baadae tukenda tukaunda 2006 sheria hii ya juzi, hii sheria ya juzi muhimu sana hii *Zanzibar Maritime Authority* inataka ipewe nguvu tuisaidie ina matatizo. Juzi sijawahi kuchangia ina matatizo leo Mhe. Spika, umesikia watu hapa wanazungumza ulanguzi sijui wa tiketi, haya mambo Mheshimiwa wala si nini mimi nina gazeti hapa la mwaka 1952 Agosti, Afrika Kwetu, linazungumza alhadhara wanasema dalal minal hadhara watu wanafanyiwa tiketi zinauzwa, tiketi zimeisha yaani haya mambo ya tiketi kwisha hayajaanza leo 1952 alhadhara hili hapa gazeti la Afrika Kwetu la Mtoro Rehani wananchi wanalalamika na meli ya serikali Alhadhara. Kwa hivyo bado tiketi zinauzwa ovyo, usimamizi mbovu bado kwa hivyo Waziri tunakuomba tushirikiane, bado ZMA juzi sikutaka kuchangia naona nipige hapa hapa bado inataka sana kurekebishwa, mambo yafuatiliwe kwa sababu roho za wananchi ni muhimu sana.

Mhe. Waziri mimi sijagusa vifungu kwa sababu najua leo hamna vifungu, kwanza itengenezwe sheria ipitishwe baadae itakaa vizuri, lakini naamini chini ya uongozi wa Rais na Baraza la Mawaziri lenye Wajumbe kama hawa na sisi Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi wako wewe Mhe. Spika, meli yetu meli hii mimi natoa jina tu MV Wananchi. Maana yake 17 milioni wametoa wananchi ili wananchi tuwe na uchungu wa meli yetu tuilinde lakini shirika hili Mheshimiwa mambo ya wakala, kwanza dunia ya leo unataka ku-*control* meli Shirika hili limekuwa na meli zimekodishwa Mkunazini miaka wamekodishwa sijui mtu gani, meli ya mafuta imekodishwa. Meli ya mafuta Mhe. Spika, ilikamatwa ilikwenda Madagascar Ukombozi

ikakaa miaka 6 ikagombolewa na kampuni binafsi. Imekodishwa kwa Ecotec, Gapco, sasa faida gani. Shirika wana meli zake hawaziendeshi wanazikodisha. Kasema Mhe. Asha Bakari kama mali ya watu, kama mtu mali yake anafanya anavyotaka. Haiwezekani Shirika meli zake wenyewe ziendeshe, Mhe. Omar Yussuf kafanye upeleke *audit* wa kweli kweli. Kule mimi nimefika nimemkuta mtu wa *external auditor* keshapewa kazi ya Mhasibu haya pema hapo, *internal auditor* au mhasibu mpaka leo yupo, haya ni mambo ya ajabu ajabu.

Lakini napinga naungana na wenzangu katika bodi itayoundwa hii mpya asiwepo mtu anayehusika na Wizara ya meli hiyo ninasema wazi, Wizara ya Fedha lazima iwepo kwa sababu yeye ndie mwenye mali, Mwanasheria Mkuu na wengine lakini kutoka Wizarani ndio sometime kuna *interference* na *collaboration* pamoja na mabodi mimi nimeongoza. Najua Waziri, unajua shauri yake sisi tupo hapa. Lakini sisi kama Baraza la Wawakilishi ndio ngome ya wananchi, ndio wasimamizi wa wananchi ndio tuna haki ya kusema na sisi ndio tutajibu kwa wananchi hasa kwa kuwa tunatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi tutaulizwa na wewe Mhe. Spika, utaulizwa. Sasa Mheshimiwa lazima tufike pahala tuamue na sisi si kuulizwa tu mas-ul hata kwa Mwenyezi Mungu.

Leo mimi Mhe. Spika, jitihada yaani haitoshi muda tunataka semina lakini naomba Wajumbe wa Baraza tusihoji, tusipige kelele tuichangie tuipitishe hii sheria, ili sheria hii ikipita Rais akai-*sign* ndio tutafanya kazi na ninakuomba Mhe. Omar Yussuf ushirikiane na Mhe. Waziri kila wakati utushirikishe mpaka jambo hili likae sawa, watu wana mengi wanataka kusema wanataka kutwambia mengi lakini kwa ufupi sisi Rais tunampongeza,

Mhe. Spika, mpelekee salamu za Wajumbe wa Baraza kuwa tunampongeza tuko pamoja nae na wewe kwa dhamana yetu mwambie wale vijana wapo nyuma yako na wewe mwenyewe Spika, upo pembeni. Sasa nimeona Mhe. Spika, nieleze haya ili tumalize suala hili tupitishe. Mhe. Waziri tafadhali, tafadhali, tunazo *hansard* zako, tunayo maelezo yako na wewe ndio msimamizi wa haya tafadhali tuliunde Shirika jipya litokidhi mahitaji yetu kwa kuwahudumia wananchi wetu. Mungu ametupa meli hiyo inshaallah meli ya mafuta iko njiani Mhe. Spika, Mungu atatupa uwezo tutapata meli ya mafuta, tutapata meli nyengine inshaallah. Na wananchi wetu tuwape nguvu, tuwasaidie na wao waweze kuisema meli yenye maana iwepo hapa ili tujenge nchi yetu. Zanzibar Mhe. Spika, ni nchi ya *maritime* ni nchi ya meli.

Mhe. Spika, mwaka 1498 miaka 500 nakumbuka nyuma meli ya Vasco da Gama ilifika hapa, 1598 ilifika meli nyengine hapa, na mbali mameli, marekebu zilizokwenda Pemba na wapi. Mhe. Spika, kwa kweli naunga mkono na ninawaomba ndugu zangu Wawakilishi wote tuunge mkono. Mhe. Spika, ninakushukuru sana, Mwenyezi Mungu akupe kila la kheri akupe kila barka. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Hapana shaka Waheshimiwa Wajumbe mtakubali tumepata mjumbe wa kumalizia mazungumzo yetu kwa leo na kwa mazungumzo hayo basi kesho moja kwa moja tutakwenda kwa Wizara yenyewe na baada kufanya majumuisho yatayofanywa na Mhe. Waziri. Wajumbe ninawashukuruni na ninaakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 22/01/2013 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 22/01/2013 saa 3.00 asubuhi)

Kikao cha Tatu – Tarehe 18 Januari, 2013

Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

MASWALI NA MAJI BU

Nam. 40

Kulipwa kwa Wazalendo Walioshiriki Kuokoa Watu

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Kny. Mhe. Ussi Jecha Simai) - Aliuliza:-

Nchi yetu kwa kipindi cha karibuni ilikabiliwa na maafa yaliyopelekea kuzama kwa meli mbili za abiria ambazo zilipoteza uhai wa wananchi wetu wengi katika ajali hizo. Taasisi mbali mbali pamoja na watu binafsi walijitolea kwa hali na mali kuokoa maiti na majeruhi usiku na mchana, lakini la kusikitisha ni kwamba waliojitokeza kufanya kazi hiyo hawajalipwa chochote kama walivyoahidiwa na Serikali.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kwa kufanya hivyo, tunapoteza nguvu na ari za wananchi wetu wazalendo kufanya kazi hizo.

(b) Mhe. Waziri ni nini kauli ya Serikali kuhusu malipo ya wananchi hawa waliojitolea, na kufanya kazi kubwa ambayo kwa kweli inastahiki kupongezwa kwa nguvu zote.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 40 lenye kifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kabisa kufuatia maafa ya kuzama kwa meli zote mbili, taasisi na watu mbali mbali walijitokeza kwa hali na mali kusaidia katika matukio haya. Hii ikiwa ni pamoja na huduma za uokozi wa watu walio hai na waliofariki, huduma za kwanza, huduma za kiutu, huduma za mazishi pamoja na kusafirisha maiti na kuwarudisha makwao wale wote waliohitaji huduma hiyo. Mhe. Naibu Spika, na hayo yote yalifanyika kwa kujitolea na imani ya wananchi juu ya wananchi wenzao. Serikali bado inaendelea kutoa shukrani za dhati na pongezi kwa wale wote walioonesha upendo na moyo wa kujitolea katika kipindi hicho kigumu, tunawashukuru sana kwa imani hiyo kubwa waliyoionesha kwa nchi na watu wake. Aidha tunawaombea wale wote waliotangulia mbele ya haki malazi mema peponi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 40 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali haitoi ahadi ya malipo kwa wananchi wanaojitolea kusaidia watu wanaokumbwa na maafa bali wanaojitolea hufanya hivyo kwa kuonesha moyo wa kizalendo na imani waliyonayo juu ya wanadamu wenzao. Hata hivyo serikali imesaidia kwa vikundi na wazamiaji binafsi ambao walishiriki katika kazi za uokozi ambao ushiriki

wao ulikuwa zaidi ya siku moja ili kuunga mkono jitihada zao kubwa kwa nchi na watu wake. Lakini msaada huo hauhusu waajiriwa wa Serikali.

Vikundi vilivyopatiwa malipo ni pamoja na:-

- Kikundi cha watu wa Kojani watu tisa (9)
- Island Marine watu wanne (4)
- Easy Blue watu watatu (3)
- Red Cross watu watano (5)
- Wazamiaji binafsi watu watatu (3)
  Hawa wote ni wazamiaji na wamelipwa Tshs. 20,000/- kila mmoja kwa muda wa siku nne (4)
- Watoa huduma wa chama cha msalaba mwekundu wapatao 20, wamelipwa Shilingi 10,000/= kila mmoja kwa muda wa siku nne (4).

(b) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu ya kifungu (a) kwamba hayo yameshafanyika kwa imani na kujitolea kutokana na moyo wa kizalendo, hivyo naomba nitoe tena shukurani za dhati kwa wale wote waliojitokeza kusaidia wananchi wenzao wakati wa ajali zinapotokea, tukiamini kuwa wameonesha mfano wa kuigwa na moyo wa kujitolea na Serikali inatambua mchango huo mkubwa walioutoa na hati rasmi zimetayarishwa kwa ajili ya kuthamini msaada huo mkubwa. Aidha nitoe wito kwa wananchi wengine kuwa na moyo wa kujitolea na kutoa huduma kwa moyo mkunjufu wakati nchi yetu inapokumbwa na maafa. Naamini, Mhe. Naibu Spika katika matukio ya maafa si malipo ndiyo yatakayoengeza ari na nguvu bali ni utu, huruma na uzalendo kwa wananchi wenzetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kwa kuwa Zanzibar ni nchi ya visiwa serikali ina mpango gani wa kuanzisha kikosi cha uokozi pale inapotokea janga kama hili na Mwenyezi Mungu asije akajaalia likaja likatokea tena, badala ya watu wote wakifanya kazi hiyo ya uokozi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunacho kikosi cha Zimamoto na Uokozi lakini vile vile tunayo KMKM pamoja na Polisi Marine hawa wote wana wajibu wa kufanya shughuli za uokozi pale ambapo ajali zinapotokea. Lakini ushauri mzuri wa kuimarisha kikosi chetu hiki ili kuwa na nguvu zaidi na uwezo wa vifaa pale inapotokea ajali za kuzama kwa meli ili kutoa huduma za uokozi kwa haraka na kwa umakini, kuhakikisha kwamba kazi hiyo inafanyika vizuri ili kuokoa maisha ya watu wengi. Kwa hivyo ushauri ni mzuri serikali inaufanyia kazi tuone tutafikia hatua gani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba wananchi walijitolea na kama ambavyo wamepongezwa na Mhe. Waziri katika suala zima la uokozi katika ajali hizo lakini bado kimsingi tunakubaliana sote kwamba kazi ya uokozi ni kazi ambayo inahitaji ujuzi maalum na inahitaji watu wa fani hiyo. Na kimsingi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndiyo iliyosimamia kukabiliana na maafa lakini uzoefu umeonesha katika ajali zote mbili hizi kubwa serikali imeshindwa kabisa kujipanga kiasi ambacho hata wananchi kama waliojitolea huduma za msingi walishindwa kupatiwa, bali hata hivyo vikosi alivyovitaja Mhe. Waziri katika majibu yake navyo

vimeonekana vipo pale havina huduma. Hata mafuta ambayo yalitakiwa kutolewa na serikali kusaidia kuingia baharini na kufanya kazi ya uokozi serikali ilikuwa inapata wakati mgumu sana kuvihudumia kiasi ambacho ilikuwa inaweza kufikisha hata masaa sita wanapita wanashindwa kwenda baharini kwa sababu hakuna mafuta. Sasa nataka kuiuliza Ofisi ya Makamu wa Rais ile mikakati na sera walizotuletea hapa zimefikia wapi katika utekelezaji au ndio kama kawaida zinaishia kwenye makaratasi na zinazobakia katika makabati ya Ofisi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikuhakikishie kwamba serikali yetu imejipanga katika kufanya kila hatua za kusaidia kuhakikisha kwamba inapotokea ajali tunafanya wajibu wetu ili kuona tunaokoa maisha ya vatu wetu.

Mhe. Naibu Spika, sio siri hali yetu ya kiuchumi bado sio nzuri, uwezo wetu mdogo kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hakuna vifaa vya kutosha katika kufanya shughuli hizi ili kuzifanya kwa vizuri zaidi. Nia na dhamira ni kuwa na vifaa vya kutosha, kuwa na vikosi vyenye ujuzi katika mambo haya ili linapotokea tatizo hili tuweze kulishughulikia ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, vikosi vyetu vinafanya jitihada kubwa ikiungwa mkono na serikali na kila kikosi kinatakiwa kijipange ili inapotokea dharura ifanye shughuli za dharura. Inapotokea dharura hutakiwi tena kwanza utafute Wizara ya Fedha sijui utafute wapi unatakiwa mwenyewe katika kikosi chako na katika Idara yako uwe tayari umejipanga kuhakikisha dharura unaikabili na wakati huo huo unawasiliana na serikali kuona sasa utaratibu gani utaendelea kusaidiana nao.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, tutaendelea kuchukua ushauri huo wa Waheshimiwa Wajumbe ili tuone namna gani tutakavyoweza kuhakikisha tunachukua jitihada za makusudi kuhakikisha tunasaidia sana pale inapotokea matatizo basi wananchi wetu waweze kusalimika au kuwaokoa kabla ya kupata athari kubwa zaidi. Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, tunafanya *survey* ili kujua mahitaji halisi yanayotakiwa, kidogo ni kazi ngumu tulifanya mwanzo kwa kutumia wataalamu wetu wa ndani lakini inaonekana bado tunahitaji kufanya kwa vizuri zaidi ndio maana tumo katika kutafuta wafadhili wengine kutusaidia katika jambo hili, na UNDP wametukubalia kutusaidia fedha, kwa hivyo karibuni hivi tutapata mshauri mwelekezi atakayetusaidia kuhakikisha kwamba tunayajua mahitaji yetu na kujua hatua gani za kuchukua pale ambapo panapotokea ajali za namna hii.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake Mhe. Waziri, Mhe. Waziri kama utakumbuka hivi karibuni katika bajeti tumesema kuwa tuwe na mchango au tufanye jambo kwa makusudi kuna vifungu ambavyo tulivipunguza na tukapata fedha nyingi za kununua meli. Je, Mhe. Waziri huoni iko haja kwa makusudi sasa hivi serikali au Wizara yako ikafanya misingi hiyo hiyo ya kuweza kupata fedha za kuweza kupata viokozi kwa sababu ni kitu muhimu sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ushauri wa Mhe. Mshimba ni mzuri sana na ningependa ingefanyika hivyo lakini Mhe. Naibu Spika, hali yetu ndani ya Serikali ni ngumu uwezo uliopo ni mdogo katika kukata hizo fedha za meli basi tumepunguza mafungu sana. Na kama tutaendelea kukata mafungu mengine kwa sasa hata

uendeshaji wa shughuli za serikali kwa kila siku utakuwa mgumu mno, lakini ushauri mzuri, maombi yetu haya tutajitahidi kila mara kuyapeleka Wizara ya Fedha ili wayaone umuhimu wake na hatua zichukuliwe tupate fedha za kutosha. Na Mhe. Waziri amesikia na anacheka inaonekana kwamba ameshalikubali ombi hili.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kanuni namba 144 Mhe. Naibu Spika, inayozungumzia habari ya mavazi, naomba kwa heshima yako Mhe. Naibu Spika, ninukuu kanuni hii.

"Bila ya kuathiri masharti yafuatayo ya kanuni hii kila mtu anayeingia katika ukumbi wa Baraza na mazingira yake atawajibika kuvaa nguo na mavazi safi na yenye kuhifadhi heshima yake, hadhi ya Baraza na utamaduni wa Wazanzibari".

Sasa mimi nataka niongelee kuhusiana na hadhi ya Baraza kwamba uvae mavazi yanayoweka hadhi katika Baraza. Mhe. Naibu Spika, hili ni Baraza la nchi wananchi wote wanategemea Baraza hili na bila kujali itikadi za kivyama wananchi wengi wanalitarajia hili. Lakini kwa kutumia hii hadhi ya Baraza naomba Mhe. Naibu Spika, kwamba nguo aliyovaa Mwakilishi wa Matemwe Mhe. Abdi Mossi ni rangi ya kijani na ni sare ya Chama cha Mapinduzi. Ninakhofia sana Mhe. Naibu Spika, kwamba ikiwa leo yeye kavaa kijani kesho mimi nitavaa nyeupe na nyekundu, kesho kutwa na yule atavaa kijani tena Baraza zima litakuwa na sare za vyama, jambo ambalo hatutawatendea haki Wazanzibari.

Katika hili Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima ili kuliondosha Baraza hili katika sura za vyama, naomba sana kwa heshima na taadhima Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa tumuombe Mhe. Abdi Mossi abadilishe suti ya leo, ili kesho Mhe. Hija asije akavaa nyeupe na nyekundu.

Mhe. Naibu Spika: Taarifa imepokelewa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, nimemsikiliza sana Mhe. Mwakilishi nataka nimwambie tu kwamba sare ya Chama cha Mapinduzi ni kijani na nyeusi au manjano na nyeusi. Mwakilishi wa Matemwe amevaa suti ya rangi ya kijani, nadhani kwa kanuni zetu ile sio sare ya Chama cha Mapinduzi. Kama tutakuwa tunafuata maelezo yaliyotolewa na Mhe. Mwakilishi hatutovaa nguo humu ndani kwa sababu nyeupe ni sare ya chama, nyekundu ni sare ya chama, feruzi ni sare ya chama itakuwa sote humu ndani tunavaa sare za vyama. Ninakuomba sana Mhe. Naibu Spika, kwamba maelezo ya Mhe. Mwakilishi ambaye ni baba yangu naomba yawekwe kando na kama kanuni zetu zina mapungufu turekebishe kanuni zetu. Sare ya Chama cha Mapinduzi ni kijani na nyeusi. Ninamuomba sana Mhe. Mwakilishi baba yangu amridhie Mheshimiwa wa Matemwe kuvaa suti yake na mimi nasema amependeza! (*Makofi).*

Mhe Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe asome kanuni suala la mavazi 144 kifungu cha 3 Mjumbe mwanamme anaruhusiwa avae nini haikutaja rangi imetaja utaratibu tu kwamba nguo uliyovaa yote ilingane kama kijani juu na chini, nyeusi juu na chini. Kama koti, kofia, kanzu na makubadhi kwa hivyo haikutaja rangi naomba tuendelee.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abadalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza ninashukuru sana kwa jibu alilolitoa au maelezo ya ziada aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Fedha kuwa rangi ya kijani si alama ya CCM hii ni mpya kwangu mimi. Na ikiwa hivyo ndivyo ninashukuru sana nimesoma na ninavyoelewa ni kuwa hata bendera ya CCM mji wake wote ni wa kijani zile nembo ziliomo nyengine zinaeleza mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe kanuni imesema mtu avae nguo inayofanana kama kijani juu na chini kama nyeusi juu na chini sare ya chama ni rangi ya kijani na suruali nyeusi yeye hakuvaa hivyo naomba tuendelee.

Nam. 30

Maandamano ya Wanawake wa Kiislamu

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Hivi karibuni vyombo vya habari mbalimbali viliripoti kuwepo kwa Maandamano makubwa ya Wanawake wa Kiislamu Nchini Nigeria kwa lengo la kuishindikiza Serikali katika kuwapatia haki yao ya kupata Waume kama ilivyo katika Sheria za Kiislamu. Waislamu Wanawake wapatao milioni moja (1,000,000) walipanga kuandamana katika Mikoa yote inayosimamia Sheria za Kiislamu kwa lengo hilo, Serikali ikalazimika kukubali ombi lao na kuandaa utaratibu maalum kwa kuwajazisha fomu za maombi wanaume wote wanaohitaji kwa pamoja na kuwasaidia mambo ya msingi ikiwa ni pamoja na mahari, vyombo, pahala pa kuishi pamoja na mikataba maalum.

(a) Je, katika Sheria za Kiislamu utaratibu huo unakubalika.

(b) Kwa kuwa Nigeria imetamka wazi kuwa lengo la mpango huo unalenga kupunguza talaka, migogoro ya ndoa, watoto wa mitaani, umasikini na maradhi ya ukimwi, Je, SMZ haioni haja ya kuiga mpango huo.

(c) Kwa vile katika mpango huo ndoa hizo hufanywa kwa makundi na kwa siku ambayo iliamuliwa na Serikali, Je, ni nani anayekuwa Walii wa ndoa hizo – Mawalii katika familia zao au Serikali kwa ujumla wao.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Utaratibu huu katika Uislam unakubalika. Ndoa ni mkataba na hayo yote yaliyofanyika ni mikataba. Katika nchi za Kiislamu au zenye Waislamu wengi, utaratibu huu ni wa kawaida. Kwa mfano, nchi kama Sudan wanao utaratibu huu na wao wanauiita (Zawaju Zaharaa). Waislamu wa rika zote huhamasishwa na huandika majina yao, na hupangiwa

siku maalum ambayo hukusanyika mbele ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Kadhi ambaye huwa ameshaandaliwa kwa shughuli ya kuozesha. Kikawaida Serikali huwa inawasaidia mahari, makaazi na kitu kidogo cha kuanzia maisha pindi ikiwa Serikali inaweza kukidhi haja hiyo kifedha na mambo mengine muhimu. Lakini ieleweke kuwa Serikali hailazimiki kufanya hivyo.

(b) Hayo yote waliyoyazungumza wananchi wa Nigeria ni kweli lakini hapa Zanzibar bado hatujafika utaratibu wa kupunguza maradhi hayo kwa njia kama hizo. Isipokuwa kwa upande wa Masheikh hushirikiana na Idara inayohusika pamoja na Wizara ya Afya kutoa elimu ya kupambana na janga la Ukimwi kwa njia ya mihadhara, mawaidha na vipeperushi pamoja na njia nyenginezo, ambazo kwa Zanzibar tunahisi ni nzuri zaidi.

(c) Kikawaida walii wa ndoa hizo huwa ni wazazi wenyewe na kwa yule asiyekuwa na wazazi basi huozeshwa na Makadhi. Hapa Zanzibar zilishawahi kufanyika ndoa kama hizo katika Viwanja vya Ijitimai ya kwanza iliyofanyika Magogoni 1994 na watu wengi walipata bahati ya kufunga ndoa kwa njia hiyo. Waliosimamia ndoa hizo ni wazazi wenyewe na Kamisheni ya Wakfu kwa wakati huo, kwa upande wa wale waliokuwa hawana Mawalii waliozeshwa na Kadhi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo kifungu (a) na (b). Katika utaratibu wa kiislam sharti moja la ndoa ni kuwepo Ijabu na Qabuul. Sasa kwa utaratibu huu kwa serikali kuozesha ndoa pamoja naomba anielimishe nani atakuwa ijabu na nani atakuwa qabuul.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Naomba arejee sijafahamu.

Mhe. Naibu Spika: Naomba urejee swali kwa utaratibu hakusikia Mhe. Waziri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, katika utaratibu wa kiislam ili ndoa ikubalike lazima kuwepo na Ijabu na Qabuul kwa maana ya kwamba kuwe na idhini ya anayeolewa na idhini ya anayeoa. Sasa kwa utaratibu huu wa serikali wa kuozesha ndoa za pamoja nani anakuwa ijabu na nani anakuwa qabuul.

b) Hapa Zanzibar pamekuwa na wimbi kubwa la kughushi vyeti vya kuzaliwa; imeripotiwa kwamba kuna baadhi ya wakristo hughushi vyeti kwa ajili ya kupata waume, kama hilo ni kweli na kama likigundulika kwamba ni kweli, utaratibu huu wa ndoa Serikali itahakikisha vipi wanaoolewa ni waislam wa kweli.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, ndoa kama nilivyosema ni mkataba na inategemea ni ndoa ya aina gani, ikiwa ni mwanamke ambaye ameshaolewa basi si lazima kupata idhini ya walii. Lakini ikiwa ni ndoa ambayo mwanamke ni chuo cha mwanzo wazee lazima watoe idhini. Sasa kwa maana hiyo hata hizo ndoa za Magogoni zilizofanywa, kwanza ilitakiwa idhini kwa upande wa kuukeni na kwa upande wa kuumeni. Na kwa wale ambao walikuwa hawana walii ni kama tulivyosema Kadhi ndiye anayehusika kutoa idhini.

Suala jengine ikiwa kuna vyeti ambavyo vimeghushiwa wakati sisi hatujajua bado kama cheti hiki kimeghushiwa, tutai-*consider* ndoa ile kama ni ya halali. Lakini pale ambapo utapatikana

ushahidi kwamba cheti kile kimeghushiwa umri haujafika na pengine mambo mengine yanayohusika hayajapatikana bila shaka ni suala la kupelekwa mahkama ya Kadhi na mahkama ya Kadhi wao wanaweza kwa misingi ya dini ya kiislam wanaweza kuitengua ndoa ile au wanaweza kuihalalisha inategemea mazingira ya kesi yenyewe.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi la Mhe. Hija, amesema kuwa kwa wanawake waliokuwa wameshaolewa kunakuja na idhini ya mwanamke mwenyewe lakini kwa wanawake waliokuwa hawajaolewa idhini ya kuolewa inatoka kwa walii wake. Ni kwa nini mahakimu wa Kadhi wanawaozesha wanawake waliokuwa hawajaolewa na ilhali wanao mawalii wao.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba idhini ya mwanamke aliyekuwa hajaolewa ni lazima itoke kwa wazee wake. Lakini kwa sheria ya kiislam Kadhi baada ya kupata maelezo ya upande wa mwanamke na ikiwa maelezo yale ameridhika nayo kwamba idhini ile pengine isingetoka na kuna mambo ambayo yanaashiria kama hakuolewa kunaweza kukawa na matatizo mengine basi Kadhi anayo idhini hiyo ya kuozesha. Lakini hiyo inategemea kila kesi kwa utaratibu wake, kila kesi lazima isikilizwe na Kadhi na akiikubali yeye hata kama anae mzee au walii wa kuozesha kwa kesi hii yeyé angeliweza kuozesha basi anaweza akafanya hivyo, lakini hiyo inategemea kesi kwa kesi.

Nam. 69

Uhaba wa Mafuta ya Gari la Kubebea Wagonjwa

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:

Kwa kuwa Hospitali ya Vitongoji *Cottages* inalo gari la kubebea wagonjwa hususan wazazi kuwatoa maeneo ya vijijini hadi hospitali, sambamba na kuwasafirisha wagonjwa wa rufaa, aidha kuwapeleka Hospitali ya Chake-Chake au katika Hospitali ya Abdulla Mzee Mkoani.

Na kwa kuwa mara kadhaa gari hilo hushindwa kusafirisha wagonjwa hao kutokana na ukosefu wa mafuta.

(a) Je, Serikali inajua kuwa mafuta yanayotolewa katika Hospitali ya Vitongoji *Cottages* kwa ajili ya gari la kusafirishia wagonjwa hayatoshi.

(b) Ni kiasi gani cha mafuta ya *Diesel* hutolewa kwa kila mwezi kwa ajili ya gari hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Bajeti za mafuta kwenye hospitali huwa zinapangwa kulingana na mahitaji ya matumizi ya hospitali husika. Kwani utaratibu wa gari zote za serikali kunatakiwa kuwa na *log book*

inayoonesha ni mafuta kiasi gani yametiwa, lini na katika kilomita zipi. Imetoka wapi na imekwenda wapi kwa siku nzima na ilipolala ilitembea mpaka kilomita ngapi. Kwa hiyo, idadi ya mwezi mafuta yanaweza kukadiriwa kwa wastani wa kilomita zinazokwenda. Kama gari ni jipya basi lita moja ya mafuta ya *diesel* gari inakwenda kilomita 8 na kama imechakaa inashuka mpaka kilomita 5.

Baada ya kusema hayo sasa napenda kujibu swali

(a) *Ambulance* ya Vitongoji *Cottages* hospitali inapatiwa mafuta ya kutosha kwa mwezi na hasa ukizingatia iko umbali wa kilomita 5 kutoka hospitali ya Wilaya ya Chake Chake.

(b) Kwa sasa inapatiwa lita 300 za *diesel* kila mwezi mafuta ambayo yanatosha kabisa ukizingatia uchache wa wagonjwa wanaolazwa hospitali hiyo, umbali uliopo kwenda Chake Chake Hospitali na mara chache sana kwenda Abdalla Mzee Hospitali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa amejibu kuwa mafuta yanayotolewa kwa ajili ya *ambulance* yanakidhi haja na kwa kuwa kuna ushahidi wa kutosha kwamba kuna baadhi ya siku wagonjwa wanashindwa kupelekwa katika Hospitali ya Chake Chake pale wanapopata rufaa.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri anaweza kukubaliana nami kwamba katika Hospitali ya Vitongoji hakuna usimamizi mzuri wa mafuta haya.

(b) Mhe. Naibu Waziri anaweza akakubaliana na mimi kwamba katika hospital ile pana matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ukitizama msingi wa swali lake la mwanzo anasema kwamba gari ya hospital ya itoe wagonjwa vijijini kuwapeleka Kituo cha Afya cha Vitongoji, ikisha iwatoe Vitongoji na kuwapeleka Chake Chake na hospitali nyengine. Kama mafuta yatatumika kukusanya wagonjwa mitaani bila ya wewe kuchangia pale mafuta hayatatosha, kama mafuta yatatumia kutoka hospitali tu kwenda hospital nyengine kwa wagonjwa walioko Vitongoji nina imani kwamba lita 300 zinatosha.

Mimi nakushangaa Mhe. Saleh Nassor wenzako wote wawakilishi wanajitahidi kuchangia majimbo yao, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa mgonjwa yoyote anayekwenda pale anatoa mafuta ya kumtoa kumleta mjini, wewe unakuja hapa kulalamika kwa sababu ya kuwasaidia wagonjwa wako kutoka kwenye vijiji kwenda hospitali, ingekuwa wanatoka hospitali kwenda hospitali; mafuta usiyatumie huko. Wenzio wamenunua magari, wanachangia mafuta, wewe unakuja kulalamikia hilo. Mimi nafikiri badala ya kulalamika utusaidie, sisi tutoe mafuta ya kutoa hospitali kupeleka hospital na wewe utoe huko vichochoroni kupeleka hospitali.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri alisema kuwa mafuta wanakuwa wanapewa kiukamilifu kabisa hao watu wa *ambulance* kwaajili ya kuchukulia wagonjwa, naomba unipe *data* kwa mwaka mzima *ambualnce* hilo wanatumia lita

ngapi za mafuta? Lakini kama ukishindwa kunipa *data* huoni kwamba Baraza hili utakuwa unalidanganya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nimehakikisha kwamba kweli wanapewa lita mia tatu kwa sababu Pemba utaratibu wao tofauti na Unguja, Pemba kule wanapima mafuta yao, wanapewa pesa zao, katika bajeti zao na kwa Hospitali ya Vitiongoji wanapewa lita 300 na kwa ushahidi huo ninao na ukitaka nenda kaangalie.

Unguja inategemea na hospitali ukinambia Mnazi Mmoja nitakwambia hilo halina mjadala yanapokuwepo yanatiwa hayapo basi, ukinambia Makunduchi kule kuna utaratibu mzuri HIPZ (NGO) wapo wanasaidia watu wanakwenda kuchukuliwa kwenye mitaa wanapelekwa hospitali, ukiniambia Kivunge nina uhakika Mhe. Mbarouk Wadi kazi anaifanya kwa hivyo mimi sina wasiwasi na hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri ambaye yuko chini ya kamati yake kwa kufuatilia vizuri. Lakini suala ninalotaka kumuuliza ni kwamba wizara yake itadhibiti vipi ubadhirifu wa mafuta. Kwa sababu hata DANIDA wafadhili wetu wakubwa wametishia kusitisha msaada wao kwa Kivunge, Makunduchi na Vitongoji kwa sababu kuna ubadhirifu wa DANIDA. Sasa vipi wizara yake itadhibiti ubadhirifu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Saleh Nassor yeyé ndiye aliyeanza kusema mafuta hayatoshi halafu tena akasema mafuta yana ubadhirifu yeyé yeyé huyo mmoja, kwanza hayatoshi baadae ubadhirifu, lakini mimi nasema gari za serikali zina taratibu zake tuna *log book* pale mtu anaandika anapokwenda anaporudi kapewa mafuta kiasi gani, kwa hivyo ni rahisi kuweza ku-*calculate* kama haya mafuta yametumika inavyotakiwa. Sasa tena kama dereva kaondoka katoka vitongoji akenda kwengine halafu akaandika tena hilo litakuwa si rahisi, lakini kwenye vitabu sisi ndimo tunamoangalia na wagonjwa tunajua katoka Vitongoji kaja Chake Chake na tukitizama mgonjwa kalazwa sasa tunataka ushahidi gani tena zaidi ya huu.

Nam. 113

Tathmini ya Vikundi vya Vijana kwa Shehia zote za Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto iliahidi kufanya tathmini ya vikundi vya vijana kwa Shehia zote za Unguja na Pemba ili kufahamu mahitaji halisi ya vikundi hivyo kwa lengo la kuwaunganisha na fursa mbali mbali zitakazojitokeza kama vile mafunzo, mikopo na upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zao.

(a) Je, ahadi hiyo imeshatekelezwa na kama imeshatekelezwa ni vikundi vingapi mpaka sasa vimeshafanyiwa tathmini Unguja na Pemba.

(b) Je, ni vikundi vingapi vimeweza kuainisha mahitaji yao mbali mbali ambayo yanawiana na uwepo wa fursa zolizopo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 113 lenye Kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ni kweli iliahidi kufanya tathmini ya vikundi vya vijana kwa Shehia zote za Unguja na Pemba ili kufahamu mahitaji halisi ya vikundi hivyo kwa lengo la kuwaunganisha na fursa mbali mbali zitakazojitokeza kama vile mafunzo, mikopo na upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zao.

(a) Mhe. Naibu Spika, zoezi la kuvifanyia tathmini vikundi vya vijana limefanyika kwa Mikoa mitatu ya Unguja na jumla ya vikundi 789 vimetambuliwa, kwa upande wa Pemba zoezi hili limefanyika kwa kuanzia na Wilaya ya Micheweni ambapo jumla ya vikundi sitini (60) vimetambuliwa na zoezi linaendelea.

(b) Mhe. Naibu Spika, vikundi vyote vimeweza kuainisha mahitaji yake mbali mbali ikiwa ni pamoja na mafunzo, mahitaji, ushauri, masoko, kupatiwa umiliki wa maeneo ya kufanyia shughuli zao pamoja na mikopo na nyenzo za kufanyia kazi. Hadi kufikia sasa jumla ya vikundi arubaini (40) vimeweza kuainisha mahitaji yao. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa Mhe. Waziri vado vikundi vingi vya ushirika vinakabiliwa na tatizo la masoko ya bidhaa wanazozalisha. Je, wizara yako inachukua hatua gani ya kuwatafutaia masoko ya uhakika kuweza kuuza bidhaa zao na ziwe na ubora.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, ni kweli baadhi ya vikundi wanakabiliwa na tatizo la masoko, lakini tumewashauri, tumewaelekeza namna gani ya kufanya ili waweze kupeleka bidhaa zao kwenye masoko mbali mbali.

Nam. 5

Kupanda kwa Bei ya Umeme

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Katika kipindi cha karibuni suala la bei ya umeme limelalamikiwa kuwa ni kubwa na lenye kukatisha tamaa kwa watu wenye kipato kidogo ambapo ukitoa shilingi 10,000 unapata *units 39* wakati kabla yake ulikua unapata *units 70.*

Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zilizofanya bei ya umeme, Zanzibar kupanda kwa ghafla badala ya kupanda kidogo kidogo kama tulivyozoea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kupanda kwa bei ya umeme inatokana na kupanda kwa gharama za kumfikishia huduma hiyo mtumiaji na moja ya gharama hizo ni bei ya umeme tunayonunulia kutoka TANESCO. Hata hivyo, bei hiyo ya umeme kutoka TANESCO imepanda mara tatu, mwaka 2008, 2010, 2011 na shirika langu halikuwa na jinsi kupandisha huduma hiyo ili liweze kujiendesha.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini ningependa kumuuliza swali moja. Je, haoni kwamba kutokana na kupanda kwa bei ya umeme kuwa hali ya wananchi ni duni, masikini ambao wenye kipato cha chini wanahitaji kufikiriwa ili kupunguziwa bei hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ieleweke kwamba umeme tunanunua kutoka TANESCO kama hivi nilivyoeleza, basi na sisi hatuna jinsi tupandishe ili tuweze kujiendesha. Nia ya serikali ni kuwasaidia wananchi wote lakini hatuna jinsi kupandisha pale ambapo na sisi tunapandishiwa huduma hiyo.

Mhe. Asha Bakari Makame: Kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuingia katika Baraza hili tukufu kwa salama na uzima. Naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye vifungu a na b.

(a) Kwa kuwa unapokwenda kulipa umeme mwanzo wa mwenzi unaambiwa kwa kuwa ni mwanzo wa mwenzi unakatwa, ukinunua umeme wa shilingi elfu kumi unapata wa shilingi elfu tano. Je, ni sababu zipi ambazo zinapelekea kumkata mteja ambaye ananunua umeme kwa shilingi elfu kumi akalipwa kwa shilingi elfu tano.

(b) Huu ununuzi wa umeme kila kituo kina risiti za aina yake au unaponunua umeme wa shilingi elfu kumi au ishirini unapata *unit* zile zile. Naomba anijibu Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ni kweli baadhi ya wateja wanaponunua umeme kwa shilingi elfu kumi huwa wanakatwa kwa kiwango cha shilingi elfu tano lakini sababu maalum. Kama tunavyokumbuka kwamba wateja wengi walikuwa na mita hizi za kawaida lakini tunawabadilishia mita hizo kwa kuwawekea mita za TUKUZA na tunapowawekea mita za TUKUZA aidha tunaangalia deni ambalo linatokana na mita aliyokuwa akitumia. Kwa hivyo, tunapofunga mita ya TUKUZA tunamchaji deni la nyuma nusu kwa nusu na kumlipia deni la ile mita ambayo anaitumia katika gharama yake ya deni la mita ya nyuma ambayo alikuwa anaitumia.

Kuhusu risiti za kulipia Shirika la Umeme zote ziko aina moja, kama kumejitokeza labda kutokea aina nyengine basi ni kwa bahati mbaya, lakini risiti zote za Shirika la Umeme ziko katika hali moja.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu yake kwa lugha yake kwamba risiti zote ni za aina moja, lakini kwa wanaokwenda wakinunua wanajua kwa uhalisia kabisa

kwamba katika vituo tofauti huwa wanapata tofauti za umeme kwa kiwango kile kile cha fedha. Hili kwetu sisi tafsiri yake ni sawa sawa na kwamba Shirika la Umeme linawaibia wananchi wa Zanzibar. Sasa serikali itwambie hapa kwamba inachukua hatua gani kurekebisha suala hili ili dhuluma ile wanayofanyiwa wananchi iweze kukomeshwa.

Lakini pili Mhe. Naibu Spika, naomba vile vile anambie Mhe. Naibu Waziri kwamba katika huu utaratibu wa kubadilisha mita usiokwisha kila siku ambao sisi wengine huwa tunatafsiri kuwa ni mradi wa watu fulani. Karibuni kulibadilishwa mita zinazotumia kiwango cha fedha kuja kwenye mita zinazotumia *unit*, lakini cha ajabu wakati zinabadilishwa mita hizo zile fedha ambazo zilikuwemo katika mita za awali zilizokuwa zikitumia kiwango cha fedha zimeondoka na mita zake na watendaji wa shirika walikuwa wanawaahidi watumiaji kwamba baadae zitarudishwa lakini hadi sasa hazijarejeshwa. Hili Shirika la Umeme litasitisha wizi huu na kurejesha fedha za wananchi katika mita zao? Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwamba risiti za Shirika la Umeme ziko katika hali moja, na Mheshimiwa kanieleza kwamba kuna baadhi ya vituo aidha zinajitokeza risiti tofauti na vile vile kuna mashaka ya malipo. Nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kama limejitokeza hilo basi tutalifuatilia na ningeomba tushirikiane kulifuatilia hili ili kama Shirika letu lina makosa tuweze kuliweka sawa.

Mhe. Naibu Spika, suala la pili kuhusu ufungaji wa mita. Ni kweli kwamba huwa tunabadilisha mita pale inapokuwepo haja ya kufanya hivyo na haja moja ya kufanya hivyo ni kuwapunguzia usumbufu wananchi wa kila siku kukatiwa umeme ndani ya nyumba zao, isipokuwa tu kwamba unapokwenda kulipa umeme tayari ni kwamba unajiondoshea usumbufu kwa kununua umeme wenyewe bila ya kwenda kulipa fedha kwa kutumia mita ile ya kawaida na inayokwenda katika mwendo wa ringi. Sasa hilo ni jambo ambalo limesababisha kwamba sisi tuondokane na mita za ringi na tufunge mita za TUKUZA kwa ajili ya kuwapunguzia usumbufu wananchi au wateja wanaotumia huduma hii.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Suala langu nambari (b) halikujibiwa nadhani hakunielewa, nilichokuwa nauliza sio kutoa mita za awali zilizokuwa zinazungusha ringi, nilichozungumza mimi ni katika hizi mita anazozizungumza yeyé mpya, tumetoka katika mita zinazotumia viwango vya fedha hizo za TUKUZA halafu zimekuja mita zinazotumia *unit.* Ninachouliza wakati wa kubadilishiwa mita hizo kwa wale ambao tayari washabadilishiwa kulikuwa na viwango vya fedha mbavyo wananchi walikuwa wameshalipia umeme wao, sasa zilipong'olewa mita za TUKUZA za mwanzo zilizokuwa zikitumia kiwango cha fedha badala ya kuonesha kiwango cha *unit* hizi zilizowekwa, zile fedha waliambiwa zitarejeshwa baadae watu wende wafuatilie, lakini kila wakifuatilia hakuna mtu ambaye amerejeshewa, ndio nikasema hii ni sawa sawa na kuwaibia wananchi wanyonge wa nchi hii. Sasa nataka waziri atwambie lini wizara itasimamia shirika ili liwarejeshee wananchi fedha zao hizi ambazo wameondoka nazo kwenye mita zao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, pale shirikani tumeweka fomu maalum ya madai, kwa hivyo kwa mtu yeyote ambaye ana madai yake na

anaona hayajatekelezwa ni vizuri akachukue fomu ile ajaze bila shaka fedha hizo zitarejeshwa bila ya tatizo lolote.

Nam. 29

Uuzwaji wa Shamba eneo la Kwaumbaju

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya Januari 12, 1964 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa na shamba lake lililokuwa chini ya Wizara ya Kilimo na kupewa wafanyakazi wa wizara hiyo ili kuliendeleza. Shamba hilo lililokuwa eneo la Kwaumbaju Mchakwe – Mwambe lilimilikiwa na wafanyakazi walioitwa (*Diebeck*) kwa jina maarufu na kuwakusanya wananchi wa maeneo ya Mwambe, Kiwani, Kengeja na kadhalika ili kuweza kulishughulikia kwa kupanda miti ya kudumu ikiwemo minazi ya asili. Kwa bahati mbaya zipo taarifa kuwa katika miaka ya tisiini na mwanzoni mwa miaka ya 2000 shamba hilo alimilikishwa mtu binafsi pasi na wananchi waliohusika kuliendeleza kuarifiwa rasmi.

(a) Je, serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaweza kutupa ukweli kuhusu shamba hilo.

(b) Je, shamba hilo lina ukubwa gani, lilikuwa na minazi mingapi na liliuzwa kwa kiasi gani.

(c) Ni utaratibu upi uliotumika kulitoa shamba hilo katika mikono ya serikali kuliweka katika umiliki wa mtu binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-
Mhe. Naibu Spika, Shamba liliopo Kwaumbaju Shehia ya Mwambe Wilaya ya Mkoani Pemba halijawahi kumilikiwa na Wizara yangu, bali katika kipindi cha miaka ya 1970 wizara hii kupitia kwa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa (marehemu Rashid Abdulla) liliwahi kuazimwa shamba hilo kutoka kwa wamiliki wake (Bwana Juma Mzee, marehemu), (Bwana Muhijazi Mzee, marehemu) na (Bwana Juma Zaharani, marehemu) wa Kengeja kwa shughuli za kilimo ikiwemo kilimo cha ushirika kwa wananchi wa Mwambe na maeneo jirani na shughuli za utafiti wa minazi). Hata hivyo, shughuli hizo katika shamba hilo baadae hazikuweza kuendelea zaidi na hivyo kwa kipindi kirefu shamba hilo lilikuwa halitumiki.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 1992 Bwana Saleh Mohammed Bajuni (mtoto wa miongoni mwa warithi wa wamiliki wa shamba hilo) kwa niaba ya warithi wenzake aliandika barua ya kuomba kurejeshewa shamba lao hilo kwa lengo la kuendeleza kilimo, shughuli ambazo hadi sasa zinaendelea.

Kwa wakati huo mwaka 1993 lilikuwa na eka 20 na ndani yake imo minazi 380. Kufuatia maombi hayo wizara iliamua kukubali ombi la wahusika. Hivyo, mnamo mwaka 1993 ililikabidhi rasmi shamba hilo kwa Bwana Saleh Mohammed Bajuni barua zenye kumbukumbu nambari WKM/32/92/93 ya tarehe 6/5/1993 (kutoka kwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na

Maliasili kwa wakati huo) na ile WKM/P/29/5/13/518 ya tarehe 8/11/1993) (kutoka kwa Ofisa Mdhamini, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili kwa wakati huo) zinathibitisha kukabidhiwa shamba hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri yaliyojaa mikwaju mingi naomba kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu a na b.

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shamba hili tunavyoamini wananchi wa Jimbo la Kiwani lilikuwa ni mali ya serikali ambalo limefanyiwa kazi tangu baada ya Mapinduzi, na kwa kuwa leo Mhe. Naibu Waziri anasema kuwa shamba hili lilikuwa si la serikali. je, anaweza kutuonesha kumbukumbu amabazo zinathibitisha kuwa shamba lile halikuwa la serikali na lilikuwa la hiyo familia aliyoitaja.

(b) Kama shamba hili lilikuwa si la serikali kwa nini serikali ikawachukua wananchi wa Kengeja, Mwambe, Kiwani na vitongoji vyake kuwatumikisha katika shamba la watu binafsi na hakuna fidia yoyote. Je, kuna fidia watayopewa wananchi wa Jimbo langu la Kengeja.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo kwamba shamba liliazimwa. Sasa wakati shamba liliazimwa na kuazima ni kitu ambacho unaweza kuazima halafu ukakirejesha. Liliazimwa shamba lakini liliwekwa kwa mujibu wa kuwasaidia wananchi katika kilimo cha ushirika, mimi nadhani baadae shamba walipoamua wenyewe hawa walioazimwa na kwa mujibu wa *document* kuwa zipo za kurejeshewa lile shamba moja ni kurejeshewa kwa huyu Bwana Saleh Mohammed Bajuni, ni *document* ambayo WKM/32/92/93 ya tarehe 8 kwa hivyo moja kwa moja inaonesha kuwa hili shamba liliazimwa na kurejeshwa. Sasa kama kuna uhakika kwamba shamba hili lilikuwa la serikali hilo wizara yangu haijui.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, dokezo ambalo Mhe. Naibu Waziri anatoa ni la mwaka 1993, shamba hili limechukuliwa tangu baada ya Mapinduzi na mzee wetu, Mzee Karume kwa ajili ya kufanya kilimo cha minazi na mambo mengine na waliotumika katika shughuli hizo ambao ni wazee sana bado wako hai. Wanaridhika vipi na dokezo la mwaka 1993 wasiwafuatilie wale watu waliokuwepo na Mzee Karume kwa ajili ya kazi hiyo na ndio maana nikasema jee zipo *document* za halali za tangu mwanzo za Mzee Karume walizoazima au munaridhika na hizo za 1993 ambapo mimi nimeshazaliwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji, na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Tarehe aliyoitaja yeye ni tarehe ya kurejeshwa kwa shamba, lakini tarehe iliyoanza kuandikwa katika jibu la msingi ni kwamba shamba liliazimwa mwaka 1970 na sio mwaka 1993 kama alivyouliza Mhe. Mwakilishi.

Kwa sababu jibu limetaja wenyewe shamba hilo kwa majina na ni wenyeji wa hapo Kengeja, kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, inathibitisha kwamba lile shamba hawa waliotajwa ndio waliokuwa wenyewe na bila shaka itakuwa zipo *document* mahala zinazoonesha kuwa hilo

shamba ni hao wenyewe na hao wakakubali kuliazima likatumiwa kwa ajili ya ushirika, nahisi jibu lilikuwa sahihi.

Sasa kama kuna suala la kufanya utafiti zaidi ni vizuri Mhe. Mwakilishi akashirikiana na Wizara ya Kilimo akapatiwa hizo *documents* za kuthibitisha kwamba hilo shamba halikuwa la serikali, lilikuwa ni la watu na majina yametajwa katika lile jibu la msingi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi amesema kwamba shamba hili lililoulizwa hapa liliazimwa na kwa wakati huo aliyekuwa Mkuu wa Mkoa kwa ajili ya kilimo, na kwa kuwa Mhe. Waziri ametaja kwamba ndani ya shamba hilo kuna minazi isiyopungua mia tatu.

Kwa kuwa waliokuwa wakiliendeleza shamba hilo sio wenye shamba na kwa kuwa hao wanaoambiwa wenye shamba wamesharejeshewa hilo shamba, sasa ninataka kufahamu Mhe. Naibu Spika, shamba hili lilipoazimwa tayari lilikuwa na hii minazi au minazi hii imepandwa wakati wa uendelezaji na kama imepandwa wakati wa uendelezaji itakuwaje shamba hili warejeshewe wale ambao waliokuwa sio waliopanda minazi ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Ahsante sana Mhe. Naibu, ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, shamba liliporejeshwa lilikuwa na minazi mia tatu na thamanini. Wakati huo lilipoazimwa Mhe. Mwakilishi swali hili nitakuletea kwa maandishi kama wakati lilipoazimwa kama lilikuwa na minazi au lilikuwa halina minazi.

Kwa hivyo suala ninalolifahamu kuwa lililoporejeshwa shamba hili lina minazi mia tatu thamanini. Hivyo swali lako nitakuletea kwa maandishi.

Nam. 4

Tatizo la Kutoweka Mikarafuu

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Zao la karafuu Zanzibar ni sehemu ya kitega uchumi cha Zanzibar, zao hili linategemewa sana katika maisha ya mwananchi na bei ya karafuu ilipoongezwa kwa kiwango kizuri wananchi waliongeza mavuno yakawa makubwa kuliko yale ya miaka ya awali. Lakini matatizo makubwa ya mashamba yao ya mikarafuu ni kutoweka kwa mikarafuu yenyewe siku hadi siku.

(a) Je, Mhe. Waziri jitihada gani zimefanywa kuhakikisha kwamba kila wilaya pana idadi kubwa ya miche iliyo tayari kwa ajili ya kipindi cha msimu wa mvua.

(b) Je, serikali imejipanga kiasi gani kuwasaidia wakulima wa mikarafuu, mikopo ili waendeleze mashamba yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 4 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, serikali inayo mkakati maalum wa kupanda miche ya mikarafuu kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili serikali imepanga kila mwaka kutoa miche laki tano na kuigawa kwa wakulima bure.

Utaratibu unaotumika kwa kuigawa miche hiyo Mhe. Naibu Spika ni kupitia wilayani na inategemea na mahitaji ya kila wilaya. Hivyo serikali inawaomba wananchi wawasiliane na Wizara hii ya Kilimo na Maliasili kwa ajili ya kupatiwa miche ya mikarafuu.

b) Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa mikopo kwa wakulima ili waweze kuendeleza mashamba yao ya mikarafuu, serikali haijatenga fedha maalum kwa ajili hiyo, lakini kwa ajili ya kuendeleza mashamba, kwa kuwa ni suala la uwekezaji utekelezaji wake utafanyika baada ya kupitishwa sheria ya maendeleo ya karafuu ambayo ina lengo la kuanzishwa mfuko wa maendeleo ya karafuu.

Sheria hiyo inatarajiwa kuwasilishwa kwenye Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni. Hata hivyo, kwa sasa ZSTC hutenga fedha kidogo kwa ajili ya mikopo ya muda mfupi kwa wakulima wakati wa uvunaji wa karafuu ambapo fedha hizo huwasaidia wakulima kuanzisha kambi na kununua vifaa vya kuvunia karafuu kama majamvi, pishi, karabai na vyenginevyo.

Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, katika msimu wa karafuu wa mwaka 2011/2012, ZSTC ilitenga kiasi cha shilingi milioni mia mbili ili kuwakopesha wakulima kwa ajili ya uchumaji wa karafuu.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ameeleza katika maelezo yake kulikuwa na mgao wa miche ya mikarafuu katika kila wilaya, ningelipenda kujua kutoka kwa Mhe. Naibu Waziri kwa Wilaya ya Micheweni kiasi gani cha mgao wa miche yake, kwa sababu katika wilaya ambayo mikarafuu mingi imekufa ni katika sehemu ya Wilaya ya Micheweni.

Sasa nataka kujua ni kiasi gani ya mgao wa miche mipya ambayo imepelekwa katika wilaya hiyo kwa mwaka huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, nimesema katika jibu la swali la awali kwamba suala la kuotesha miche na kuigawa kwa wakulima lipo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, na kwa hivyo ningemuomba Mhe. Mwakilishi awasiliane na wizara hii inayohusika na suala hilo ili kujua basi katika Wilaya ya Micheweni ni miche mingapi imepelekwa ya mikarafuu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninapenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba hii miche inayotolewa inasemekana kwamba baada ya miaka miwili miche hii huoteshwa na kuchuma karafuu zake ni mara moja tu huwa inakufa.

Lakini jee, Mhe. Naibu Spika, na wewe umesema kwamba miche hivi sasa imetolewa kwa kila wilaya, hebu nikuulize katika hii miche inayotolewa imefanyiwa tathmini gani inayoota na mingapi isiyoota. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, nimesema na ninasema tena kwamba suala la kuandaa miche ya mikarafuu ipo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Sasa masuala ya utafiti bila shaka Mhe. Naibu Spika, itakuwa pia chini ya wizara hiyo hiyo ya Kilimo na Maliasili.

Kazi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaanzia kwenye uchumaji wa karafuu, kuwasaidia wakulima kwenye kuchuma, kununua karafuu zao na wakati wa kuchuma kuwasaidia uchumaji usiokuwa na matatizo kwa kuwakopesha pesa kuwarahisishia kazi hiyo waweze kuzifikisha kwenye vituo vya kuuzia karafuu.

TAARIFA

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, Katiba ya Zanzibar 1984 ibara ya 43 (5) inasema na naomba ninukuu, “Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Raia ndio itayokuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za serikali kwa ujumla na Mawaziri chini na uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar”.

Mhe. Naibu Spika, muongozo nnaouomba ni kwamba tumezoea katika mabunge takriban yote ya Jumuiya ya Madola na hata uzoefu wangu mfupi nilipokuwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kwamba linapoulizwa swali la mwakilishi linaelekezwa kwa serikali.

Sasa anapojibu Waziri au Naibu Waziri wa wizara moja, ikiwa kuna maelezo ambayo yanayotakikana kutoka kwa wizara nyengine, hiyo ni mgawanyo wa majukumu ambayo serikali umeufanya.

Kwa hivyo ni utaratibu tumeuzoea katika mabunge yote ya Jumuiya ya Madola kwamba ikiwa Waziri au Naibu Waziri wa wizara fulani anaona shughuli ile haipo kwake bado inapaswa

mwengine katika serikali, ikiwa Waziri au Naibu Waziri anyanyuke kutoa majibu ya swali ambalo limeulizwa na Mhe. Mwakilishi.

Lakini sasa imekuwa ni utaratibu wa kawaida tumeuzoea mara nyingi, tukiuliza swali anakwambia hilo halipo katika wizara yangu. Sasa ninasema nataka muongozo wako utwambie kwamba jee, hii tafsiri ya kujibu kwa moja hapa katika kujibu maswali ya Wawakilishi inatakiwa itafsiriwe vipi Mhe. Naibu Spika.

Naomba muongozo wako.

Mhe. Naibu Spika: Mimi nadhani serikali imesikia na majibu utayapata.

Nam. 2

Ujenzi wa Daraja la Mkia wa N'gombe

Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Aliuliza**:-**

Wanakijiji wa Mkia wa Ng'ombe wana matumaini ya ujenzi wa Daraja kwa kutumia *Culvert* na kifusi kwenye kivuko cha mto wa maji ya chumvi kwa muda mrefu. Daraja hili lingewasaidia wanakijiji kwa ajili ya kuvushia bidhaa na vifaa mbali mbali lakini ujenzi huo hadi leo haujafanyika.

Je, ni lini daraja hili litajengwa ili kuwaondoshea usumbufu wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 2 kama hivi ifuatavyo:-

Wizara ya Miundo Mbinu na Mawasiliano inatambua umuhimu wa daraja hilo ikiwa kama kiungo muhimu kwa shughuli za kijamii na kiuchumi kwa watu wa Mkia Ng'ombe.

Aidha kwa mnasaba huo, jitihada maalum zimechukuliwa ili kuondoa usumbufu wa matatizo yanayo sababishwa na kukosekana kwa huduma hiyo. Kwa hivi sasa tayari zabuni zimeshatangazwa na Mkandarasi mzalendo ameshapatikana ambapo Kampuni ya *Pemba Building Construction* ndio itakayojenga kwa gharama ya shilingi milioni hamsini na mbili na matarajio yetu katika kipndi cha miezi kumi na minane kazi hiyo itakuwa imeshakamilika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja tu la nyongeza.

Nimefurahi sana kwa majibu haya kwamba hili daraja tayari limeshakubalika kujengwa lakini napenda angalau unipe ni lini hasa daraja litaanza, kwa sababu hiki kipindi kizuri cha kiangazi mbele yake tunakabiliwa na msimu wa mvua kubwa sana.

Sasa angalau niweze kupata *at rough idea* ni lini hasa mutaanza hii shughuli kabla ya mvua.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, katika majibu mama tumeeleza kwamba mkandarasi ameshapatikana, gharama itakayotumika tumeshaieleza na hatua tuliopo hivi sasa tupo katika hatua za mwisho za kuingia mkataba na mkandarasi huyu ili aanze kazi.

Matarajio yetu kabla ya mwezi wa Machi kazi hii itakuwa imeshaanza katika utekekelezaji wake.

Nam. 7

Uchakavu wa Barabara Mkarafuu Mmoja – Kiuyu

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza**:-**

Barabara ya Mkarafuu Mmoja – Kiuyu ni barabara muhimu sana inayounganisha barabara mbili kuu za Mkoa wa Kaskazini zinazotumika kwa usafiri wa Chake – Wete.

(a) Serikali ina mpango gani wa kuwaondoshea wananchi usumbufu wa usafiri kwa kuwatengenezea barabara yao (*feeder road*) ya Mkarafuu mmoja – Kiuyu ambayo imeunganisha barabara mbili kuu za Mkoa wa Kaskazini Pemba zinazotumika kwa safari za Wete – Chake ili kuwaondoshea usumbufu wana vijiji na wananchi wanaotumia barabara hiyo uganishi.

(b) Kwa vile daraja liliyopo Shangafu lipo katika hali mbaya na ni eenye kuhatarisha maisha, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea wananchi daraja jengine. Kwa kuwa liliopo lishatumika sana na kwa sasa halifai.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake namba 7 kama hivi ifuatavyo:-

Azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwaondoshea wananchi wake matatizo yote yanayowakabili likiwemo suala la Miundombinu ya barabara. Hata hivyo, kikwazo kikubwa ni upatikanaji wa fedha kwa serikali.

Aidha kwa upande wa barabara hiyo ya Mkarafuu mmoja hadi Kiuyu pamoja na daraja la Shangafu kwa kuzingatia umuhimu wake kama kiungo cha barabara Kuu kwa wananchi wetu, tayari Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeshaanza kuchukua hatua muhimu za kuliondoa tatizo hilo. Hivi sasa Zabuni zimeshatangazwa na utaratibu wa kumpata mkandarasi unaendelea kwa ajili ya ujenzi wa daraja liliopo Shangafu, matarajio yetu ni kuona tukimaliza

kujenga daraja hilo harakati za kutandaza kifusi kwa maeneo mengine zitaendelea ili kurejesha huduma hiyo muhimu kwa wananchi wa maeneo husika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na napongeza majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri.

Lakini ningetaka kujua tu wizara imejipanga kutumia kiasi gani kwa kwa ujenzi wa lile daraja na kiasi kwa kifusi. Na kama Mhe. Naibu Waziri ana kumbukumbu kutoka pale Mkarafuu mmoja mpaka Kiuyu kiasi ni kilomita ngapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, barabara anayoiulizia ni barabara ambayo ni kiungo muhimu kwa barabara inayotoka Chake-Chake hadi Konde pamoja na ile barabara ya pili inayotoka Chake-Cheka hadi Wete.

Barabara hii ni kiungo kutoka barabara moja hadi nyengine yenye urefu wa kilomita sita nukta tano.

Matarajio yetu kwamba daraja tunalotaka kulijenga la Shangafu litakuwa na gharama ya shilingi milioni thalathini na saba. Azma ya serikali ni kwamba tukikamilisha daraja hili utaratibu wa upatikanaji na uwekaji wa kifusi bado gharama hazijafanywa, msingi wetu ni kulijenga daraja ambalo litakuwa na urefu na upana wa mita tano litakaloweza kunyanyua ili kukidhi matumizi ya upitaji wa maji wa chini usiweze kuathiri ujenzi huo tunaoutarajia.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya 2005

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuna wachangiaji sita wamesalia katika mswada huu, kwa hivyo naomba muda tulionao tuutumie vizuri.
Kwa hivyo mchangiaji wa mwanzo ni Mhe. Mshimba Makame Mbarouk, wa pili Dr. Sira na wa tatu Mhe. Asha Bakari, halafu wataendelea na wengine.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi hii chache na mimi nitazitumia kama ulivyoeleza na hasa ilivyokuwa mswada wenyewe ni mdogo na unataka fikra na mawazo mengi sana.

Mhe.Naibu Spika, nimefarijika sana sasa tunakwenda katika mamlaka. Nikiendelea kwenye historia kidogo huko nyuma tulipitisha mamlaka ya uwanja wa ndege na tunaona jinsi gani ambavyo utaratibu wake unavyoendeshwa.

Lakini Mhe. Naibu Spika, katika sheria zetu, lengo hasa na madhumuni ni kutafuta ufanisi wa hali ya juu wa kuweza kuendesha hizi mamlaka zetu. Mhe. Naibu Spika, kuna mambo ambayo mara nyingi sana tunasahau sana kuyatia kwenye sheria ambayo hayo mambo yanakuwa ni muhimu sana.

Nitatoa mfano Mhe. Naibu Spika, tukiangalia hasa mswada huu kuna mambo ambayo hatujaoneshwa humu jinsi gani ya uokozi na hilo halimo ambalo ni muhimu zaidi wala vikundi ambavyo vitaweza kutiwa kwa mujibu wa sheria ya uokozi ambapo kwa jina jengine, tunaita *diver* na vikundi hivyo vipo Mhe. Naibu Spika, lakini bado hatujavitendea haki kwa mujibu wa sheria.

Lakini tunatunga sheria ambayo tunayoiona sisi itakuwa ni sheria, kumbe ndani yake ukitizama mbele kutakuwa na athari yake. Mimi ningeomba sana jamani serikali tunapoamua kutunga sheria basi tuangalie uzuri na ubaya wake, isijekuwa leo sisi tumo kwenye vyombo hapa tukatunga sheria tu, baadae na sisi tutarudi nyuma sheria ile tunataka kuitekeleza itatushinda wakati sasa hivi upo nje.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo ambayo ni muhimu sana lakini sisi tumezingatia ukurasa huu wa 86 kuhusu umri tu wa vyombo lakini kuna mambo ambayo ni muhimu zaidi kuliko umri wa vyombo na hayo mambo hamna.

Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, tukiangalia hasa wataalamu hatuna na hii ndio *source* lakini watu hawaioni ni sawa sawa kuwa unataka kujenga lazima uwe na ramani, ndipo unapoweza kuijenga nyumba, ukira na ramani halafu unakwenda na *foundation* mpaka unafika pahala nyumba kamili na watu wanaingia ndani.

Mhe. Naibu Spika, vitu vile vinatumiwa na *engineer* ambaye anakuwa ni *especial* amesomea masuala yale kwa kufanya *study* ya kuweza kujenga nyumba. Lakini sisi Mhe. Naibu Spika, sheria hatuoni na tumepiga kelele mara nyingi sana kuwa lazima wataalamu waajiriwe, lakini bado *still* humu hatujaona kitu kama hicho, tuna wataalamu wachache sana.

Mhe. Naibu Spika, kuna *survey* za aina nyingi ambazo hizo ndizo zinazofanya hata hizo meli iweze kupewa ruksa ya kufanya kazi yake kwa uangalifu. Leo utakuta mtaalamu mmoja tu na mtaalamu huyo tunampa pesa ndogo. Hebu tuangalie mtaalamu tunamlipa pesa kidogo lakini akiondoka hapa akenda Tanzania Bara analipwa pesa chungu nzima, ndio maana nikasema sheria tunazozitunga tuangalie faida na hasara zake. Tatizo lipo wapi. Tatizo hatulijui.

Mhe. Naibu Spika, tulipokwenda kule SUMATRA, mimi niliwauliza swali. Hebu naomba niambeni idadi kubwa ya watu wanaokufa kwenye nchi kavu na baharini ni wapi. Wakaniambia nchi kavu wanakufa watu wengi. Ukiangalia mabasi yapo mengi ambayo ni *old model*, yana muda mrefu.

Sasa hapa ndio kichwa kinaniuma Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tunazungumzia umri au tunazungumzia kuwa gari hazifanyiwi *service* au meli hazifanyiwi *service*. Sasa survey Mhe. Naibu Spika, hapa Zanzibar kwa kweli inakuwa ni mtu mmoja anatakiwa aweze ku-*survey* meli

chungu nzima zimefanyiwa *registered*, hebu tuone hapo watakuwa ni mmoja au wawili au mkurugenzi yule ambaye ni mmoja huyo huyo, *survey* awe ndiye huyo huyo.Mhe. Naibu Spika, nalo hili tuliangalie.

Lakini Mhe. Naibu Spika, ukenda kwenye sheria mama ningeomba tumrudishie mamlaka yule yule mkurugenzi, ndiye mwenye kujua hiki kifungu cha umri wa miaka kumi na tano kwa meli kiondoke, tumrudishie mamlaka huyu mkurugenzi kwa sababu mkurugenzii ndiye anayejua kutokana na wataalamu wake.

Nitasema kidogo Mhe. Naibu Spika, kuhusu *survey*. Kuna *survey* ya ku-*survey*, lakni kuna *survey* ya kuhakikisha hasa, kuna mambo ya *engineer* yakoje na mambo chungu nzima, vipi *balance* yake meli na kila kitu. Lakini kuna *survey* nyengine anatakiwa mtu lazima zile *plate* nazo zina-*link* kwenye bahari. Sasa inaangaliwa *marking* yake ikoje na kila kitu. Hizi ndizo *survey* zinazotakiwa lakini hatufanyi *survey* hizo kutokana na uchache wa vyombo na wataalamu.

Sasa mimi nafikiria Mhe. Naibu Spika, hapa tungekaa na tukazingatia kabisa suala hili, kuwa tusione umri wa kusema miaka kumi na tano tu. Mhe. Naibu Spika, tunasema kuna meli ambayo hii ni *Lake Tanganyika*, mimi ninakubaliana nayo kama ni *Lake Tanganyika* lakini nayo hii ina-*rotate*, inazunguka ndio maana yake *Lake Tanganyika* inakuwa inazunguruka.

Kuna mambo ya lake na mambo ya bahari ni kitu cha jiografia, lakini sasa jee hebu tuangalie ina miaka mingapi. Ina miaka mia na still inachukua watu na historia nzima katika nchi za Afrika ya Mashariki kuwa bado ina-*survive*. Sasa hebu tujiulize hapa kitu gani kinachotakiwa kuwa ni muhimu, pengine hii inafanyiwa *service* kwa wakati, kila leo inachunguliwa na kila kitu, wataalamu wanaiangalia na ndio maana inaruhusu ikafanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, ninafikiria tuzingatie masuala hayo. Lakini kwa kuendelea kifungu hiki hiki meli mpya itakuja leo. Lakini tukiangalia Mhe. Naibu Spika, kama *survey* hazikufanyika kwa kuwa meli mpya imekuja leo ina umri wa miaka kumi na tano, hatuoni kama ni vichekesho pengine kama maboya hamna na mambo mengine muhimu hamna mule ndani yake, tumefanya nini, ndio yale yale yanayoturudisha nyuma.

Mimi ninaona kutokana na hali ya nchi yetu Mhe. Naibu Spika, lakini isitoshe hii ni moja katika njia ambayo tuiangalie kwa makini pengine huko mbele tunaweza tukakosa mafao yetu. Sisi leo tumekuwa wakala wa meli na wakala wa meli tume-*register* meli za nchi za nje nyingi na wenzetu hivi sasa wanatia pesa nyingi sana.

Sasa mimi hapa nina wasi wasi isije kuwa kuna kitu hapa Mhe. Naibu Spika, na sisi kama tumeingizwa mtego na tumeingia kwenye mtego huo, hatimaye tukaja tukakosa soko. Kwa sababu meli ambazo zimefanyiwa *registration* na shirika letu hapa au wakala wetu ni meli ambazo zinawezekana zikawa na umri mkubwa. Lakini tukipitisha sheria hii tutakuja kukosa faida ile.

Mhe. Naibu Spika, itakuwa ina faida gani, hebu tuangalie mheshimiwa. Sasa mimi naomba sheria hii tuangalie. Mimi naomba miaka kumi na tano kuwa ni nafasi ndogo sana kuvipa vyombo vyetu hapa.

Mhe. Naibu Spika, tutakuja kuleta zogo kubwa sana la wafanyabiashara hapa. Angalieni nyuma tulipokuwa tunahangaika, tulikuwa na meli moja tu MV. Mapinduzi, halafu MV. Maendeleo na Maendeleo yenyewe ipo wapi. Ikawa msongamano hapa wa usafiri. Sasa leo Mhe. Naibu Spika, itakuwa ndio yale yale. Atakuwa tajiri mmoja anaweza kumiliki vyombo wengine tena *forever* wamekwenda na maji.

Mhe. Naibu Spika, tunaondoa lipi tunafanya lipi. Tiketi za ulanguzi zitakuja hapa hapa, ajali tunazozikiuka tutarudi pale pale. Mhe. Spika, mimi nasema kwamba tusifanye hasira tukaking'ang'ania hiki kifungu kuwa lazima miaka 15, hapana. Tuangalie kwa uangalifu zaidi.

Lakini kwa kuongeza na kuweza kumalizia, tuangalie zaidi katika umri ambao kwa mfano tunasema kuwa tunakwenda na wakati, tunakwenda katika umoja wa mataifa. Zanzibar hatujafikia *standard* hiyo, hilo tuseme ukweli. Kwa sababu kuna mambo mengi yanatakiwa umoja wa mataifa na hatuwezi kuyapata. Tusiweke hiyo ngao ya kusema kuwa tunakwenda na wakati mambo mengi sana. Hata huko nchi za nje. Mimi mwenyewe nina umri wa miaka 48 basi bado ina miaka 50 zaidi na vyombo vinakwenda.

Mhe. Naibu Spika, Uingereza wamesema kuwa wanasheria ya 15, Uingereza ndio Zanzibar. Hebu tuangalie kwa nini vile vyombo vya kule vinakuja kufanya usajili hapa Zanzibar, kuona kuwa hiyo hali inakidhi haja ya miaka 15, wanakuja kusajili huku kwetu. Lakini mimi nasema bado tufanye kitu hiki twende kwenye sheria mama ambayo inasema kuwa bado yule yule Mkurugenzi anastahiki kuweza kuwa yeye ndiye mwenye kujua ubora wa vyombo ili aweze kusajili kitu kama hivyo.

Lakini leo Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, alisema jambo ambalo mimi nilijaribu kumchokoza, ndio maana tunasema tunaandaa sheria lakini bado hatujawa tayari. Amesema kuwa bado serikali yetu changa ya kupata vitu vya kisasa vya vya uokozi. Sasa hili suala mimi ningeomba kwamba bado mimi sijakubaliana nalo kusema kwamba serikali yangu changa, haijawa *serious* tu, niseme ukweli Mhe. Naibu Spika, hili suala hatujawa *serious.* Tunaandaa sheria hii lakini uokozi hatuna, hatuna vifaa vya uokozi, lakini sisi tumeng'ang'ania tu miaka 15. Vile vyombo vilivyokuwa muhimu vya uokozi na vikundi vinavyojulikana kwa mujibu wa sheria vyenye wataalamu hatujaonesha kabisa humu Mhe. Naibu Spika. Hili ni suala ambalo linatia uchungu na linasikitisha sana. Mhe. Naibu Spika, mimi sikubali suala hili na wala sitounga mkono mswada huu kama hiki kifungu ambacho hakijarekebishwa ili kikaeleweka, angalau kwa sababu kuna hii Tume ambayo aliyoiasisi Mhe. Rais, tume ile ya meli ya mwanzo iliyozama Mv. Spice. Tume ile ilisema moja katika tatizo iliyogundua ilisema angalau meli isizidi umri wa miaka 21, iwe katika umri wa miaka 20. Sasa kwa nini tusitumie hivyo. Basi kama 20 hamtaki basi wekeni 19 mpaka 18, lakini 15 Mhe. Naibu Spika, hilo ni suala ambalo halitoeleweka.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea tena kwa kumalizia, nije katika masuala ya ma-*engineer*. Kuhusu mabaharia tulikubaliana Mhe. Naibu Spika, kuwa chuo kiwepo, lakini mpaka leo chuo hicho

hakipo, tunasema tu tutaunda. Nakubaliana nalo kifungu kwa mabaharia wataliunda haki zao na kwa kupitia mamlaka haya, hilo mimi sikatai, nakubaliana nao sana. Lakini tulitoa ushauri na wao mamlaka haya iwe karibu na kile chombo cha mabaharia ili kuweza kusaidiana nao wale mabaharia ambao wana uwezo ili kuweza kuajiriwa katika meli husika. Kifungu hiki Mhe. Naibu Spika, mimi sina tatizo nacho.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwamba serikali yetu ilitambue suala hilo, na iseme ni kwa sababu gani, Waziri aje kunipa sababu *concrete* ya kung'ang'ania lazima kifungu hiki cha 15 kiwepo, mimi sijaona sababu kubwa. Hata kwenye sheria mama haioneshi, kwa sababu ingekuwa ipo sababu kubwa, basi kwenye sheria mama ingeonesha, lakini kwenye sheria mama haioneshi. Basi Waziri aje kunipa ili niweze kum-*support* anipe suala ambalo lililokuwa la msingi kabisa, ili mimi niridhike na niweze kukubaliana naye na kumuunga mkono kwa kifungu hicho cha 15. lakini vyengine vyovyote, mimi nina-*suggestion* kuwa 20 inatosha kusajiliwa vyombo vyetu hapa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia kidogo kuhusu suala hili tunalolizungumza la sheria ambayo imeletwa hapa ili kuweza kuichangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza napenda nimpongeze Waziri, Naibu waziri na wizara yao kwa ujumla, kwa kuweza kuleta sheria hii haraka iwezekanavyo, ili tuweze kuichangia, kuijadili na hatimaye kuipitisha na iweze kuwa sheria kwa maslahi ya wananchi wetu ambao wanapoteza roho zao.

Mhe. Naibu Spika, nimeamua kusimama hapa kwa sababu kama kuna watu wanaathirika na kuna watu ambao wanapata shida inapotokea ajali basi ni wafanyakazi wa wizara ya afya, tukisaidiwa na wenzetu wa vikosi. Hizo wizara mbili kukitokea majanga yoyote, basi tujue kwamba sisi ndio tunaokuwa waathirika wakubwa, kwa sababu tunakuwa hatuna tena nafasi ya maisha ya kawaida, tunashughulikia matatizo yaliyojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, mara ya kwanza ilipotokea ajali ya meli, zaidi ya robo tatu ya Baraza tulikuwa Arusha. Lilipotokea tatizo lile, saa 8:00 za usiku tulipopata taarifa sote tulimahanika, waliolia walilia, lakini sisi wengine tulilia mara mbili zaidi, tukifikiri kwamba watu wetu, lakini tukifikiri na kazi ambayo inatukabili. Tumerudi Unguja kama siku tano mfululizo hakuna aliyerudi nyumbani, wafanyakazi wa afya hao ambao ninawakusudia. Hakuna aliyerudi nyumbani usiku na mchana, hatujui tunachokila, tunashughulikia majeruhi na waliokufa. Wenzetu wa vikosi wanashughulikia kuchimba makaburi na kuzika. Sio kazi nyepesi.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu mlikuja poleni poleni, mkaondoka mkenda zenu. Lakini sisi kwa kweli huwa tunapata mzigo. Haukwisha mwaka mmoja tulipata tatizo jengine. Mimi nilikuwa ofisini nilipopigiwa simu kuambiwa kuna meli imezama, sikuamini masikio yangu. Niliganda juu ya kiti kama gundi, nikaifikiri siku ile na nikaifikiri na kazi inayokuja. Nikampigia simu daktari mkuu kuhakikisha kama hilo lililosemwa ni kweli, maana sikutaka kuamini. Nikaambiwa kweli daktari taarifa imeshakuja na hapa tunajipanga. Nakupenda kwangu kuvaa michuchumio lakini nilitoka na viatu vya kutawazia nikaenda hospitali. Nilikuja kuvuliwa na wafanyakazi wangu wakanipa viatu vyengine, kwamba ni kitu kinachotisha.

Mhe. Naibu Spika, Barazani hapa yalipotokea hayo hakuna aliyebakia kimya hapa. Rudieni *hansard* zenu za nyuma muende mkazitizame. Nyie nyie mnaokataa leo, rudieni *hansard* zenu za nyuma mkaangalie mliyoyasema. Leo hii kwa maslahi na uhai wa watu tunakataa maelekezo tunayopewa na serikali kwa ajili ya kuhakikisha kwamba roho za watu zinalindwa. Hivi na waniambie Wawakilishi, ni nani hakuguswa na misiba ile, kama si ndugu yako, au ndugu yako, au jirani yako au mwanao na kama si nchi yako, tutizame basi kwa mtazamo huo kama hukufiwa na mtu. Sisi wengine tumefiwa na majirani, tumefiwa na ndugu na wamekufa wafanyakazi wa Wizara ya Afya ambao walikuwemo katika meli zile. Tunataka tuathirike kiasi gani watu wa Wizara ya Afya mpaka tusimame hapa kusema.

Lakini sio hilo tu, yakishatokea hayo na tukishafanya kazi hizo zote, tunasema kwamba tunatumikia wito. Hapa leo suala la mwanzo linadaiwa watu waliojitolea. Sisi Wizara ya Afya tulisema kwamba, waliuliza maswali, hao hao wenye vyombo, bado kesi hazijesha, lakini wanauliza maswali kuwa watu mtawalipa vipi. Tutawalipa vipi wakati na nyinyi ndio mnaosababisha hamtaki kukubali. Tusifanye hivyo, uhai wa binadamu ni mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, asubuhi hapa tunaapa kwamba ooh! Tuepuke tamaa mbaya, tusifanye hayo. Kwenye kiapo ndio ilivyo hivyo, tuepuke ubinafsi. Lakini hatuangalii maisha ya binadamu, kama mngejua kifo cha majini ni kibaya na maiti wanapoletwa pale wanakuwa na hali mbaya basi tusingekaa tukatetea hiyo miaka 5, tungetetea uhai wa watu. Sisi ni Wawakilishi wa watu na tunatakiwa tutetee maisha ya watu, tusitetee maslahi yetu binafsi.

Mhe. Naibu Spika, kweli ajali haina kinga wanasema, lakini nyengine kinga zinazo. Chombo kikiwa kipya na ikiwa kutatokea mengine, hayo ni mengine. Lakini kikiwa kikuukuu tunategemea kwamba ajali itakuwa karibu zaidi. Watu wanazungumzia kuhusu MV. Ilemba, sidhani kama kuna aliyeipanda MV. Ilemba hao wanaozungumza hapa, mimi nasema kwa sababu nimeipanda. Nilikuwa nafanya kazi katika Kitengo cha Ukoma na watu wa ukoma walemavu wanakaa kwenye visiwa, nimepanda meli hiyo. Sio kwamba ndio meli ya fahari watu wana raha sana, hawana jinsi tu kule na sisi ikiwa tutapitisha sheria hii watatushukuru maana na wao watapata meli nyengine mpya na yenye usalama. Kwa hivyo, hatuwezi kujilinganisha kwa jambo baya eti tunataka hapa kwetu tufaidike, hapana. Meli mimi nafikiri miaka 15, hata kama Tume ilipendekeza miaka 20 ni mapendekezo tu, serikali imeamua na sisi ndio waamuzi wa mwisho, miaka 15 mimi nafikiri ni ya maana zaidi kuliko hayo wanayoyataka wao.

Mhe. Naibu Spika, unajua kama wangekuwa wanafahamu msongo wa mawazo unaowapata wafanyakazi wa Wizara ya Afya yanapotokea yale. Kwa sababu wakati ule tunakuwa hatukujipanga, tuna dawa zetu tunazozitumia inabidi zote tuzitumie kwa ajili ya ajali, kitengo cha maafa kinakuwa hakina pesa, serikali inakusanyika na watu wanakusanya pesa hapa na pale ili waweze kutusaidia sisi waweze kuchimba makaburi na waweze kufanya hayo yote. Wakati huo huo mchango ndio ule wa serikali, wakati huo huo mwisho wa mwezi wanangojea pesa tulipwe, wakati huo huo wanakuja watu wanasema kwa nini hatuwapi dawa hospitali wakati serikali wamesema watatoa dawa bure. Hivi hayo yote yatatokea wapi kama ajali zitaendelea kutokea na kutokea.

Mhe. Naibu Spika, mimi sijakiona bado kinacholindwa kwa ajili ya maisha ya watu, yote zungumzeni, lakini tunapozungumza maisha ya watu ni kitu chengine, kwa sababu mimi ni mfanyakazi na ninayehusika na maisha ya watu. Sasa kama nyinyi mnaona raha kwa sababu ya mapesa au kwa sababu ya nini, hayo mengine mimi sidhani kama yana maslahi na maisha ya watu, na hao watu tulionao ndio hao hao Wawakilishi wenu wanaokaa wakakupigieni kura. Yalindeni maisha yao kwa kupitisha mswada huu, sio kubadilisha maneno hapa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri badala ya kukaa tukalinda hayo, tuone jinsi gani tutakavyojipanga tuweze kuupitisha mswada, tukishaupitisha mswada tuangalie hayo ya vyombo vya uokozi, tuangalie hizo pesa zitakazopatikana wafundishwe watu. Badala ya kukaa hapa tunakaa tunahudumia mazishi, tunahudumia kambi na mambo mengine, halafu tunakuja kuulizana maswali ambayo hayana majibu. Hao wanaodai vyombo vichakavu vipitishwe mimi naona kwa kweli hawatupendi wananchi wa Zanzibar, kwa sababu wao wana uwezo wanasafiri kwa ndege, asubuhi na mchana wanachagua ndege wanayoitaka, lakini hawawapendi wananchi wao maskini wanaovitegemea vyombo katika maisha yao. Tunasema lakini wangapi tunapanda nao ndege hapa. Mimi sijawaona wanapanda boti, siku zote tunapishana uwanja wa ndege pale. Lakini kama wanataka wananchi wao waishi, basi vyombo viwe salama.

Maamuzi yote yatakayotolewa hapa Mhe. Naibu Spika, mimi nasema kwanza yazingatie uhai wa watu na maslahi ya watu binafsi baadae. Baada ya kusema hayo, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi hii asubuhi ya leo, nikushukuru sana. Lakini kwanza kabla ya yote niipongeze serikali kwa kuleta marekebisho ya mswada huu ambao ni muhimu, ili kuweza kutumika katika taratibu za kisheria.

Lakini nitakuwa mwizi wa fadhila Mhe. Naibu Spika, kama sikumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake kwa jumla, kwa jinsi walivyotuainishia vile vifungu ambavyo vinahitajika katika kuimarisha mswada huu na baadae kuwa sheria.

Niseme tu Mhe. Naibu Spika, kwamba leo sitokuwa na mengi, kwa sababu jana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, mfano wake alinifilisi kwa maelezo ambayo ameyatoa, lakini sio vibaya na mimi nikachangia hapa na pale.

Kwanza nije katika kuongezwa kifungu kipya cha 10(a), lakini kikawa kifungu cha 10(a) (1). Kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, naomba nikinukuu kidogo.

Kifungu cha 10(a) (1)

> “Hakuna mtu au taasisi atakayeingia katika shughuli zozote zinazohusiana na usafiri wa baharini bila ya leseni au kibali kinachotolewa katika namna itakavyoelekezwa na mamlaka”.

Mimi hapa kidogo Mhe. Naibu Spika, najua kuna vibali vinatoka katika sehemu mbali mbali, lakini hapa mimi kwa sababu hili ni suala nyeti, mimi hapa kidogo nitakuwa mbishi, kwa sababu hapa tunaweza tukakaribisha rushwa, kwa sababu vibali tunatoa katika sehemu mbali mbali. Lakini hivyo vibali Mhe. Naibu Spika, ndio vinageuka rushwa, sasa suala hili hapa ni nyeti.

Mhe. Waziri naomba uje unieleze vizuri na suala hili sitokubaliana nalo, kama ni shughuli ambayo taasisi hii mwenye mamlaka basi atoe yule mwenye mamlaka tu, sio baadae apewe mtu ambaye baadae ije igeuzwe rushwa. Yule mwenye mamlaka kama ni Mkurugenzi, Katibu Mkuu au kama ni nani, lakini mimi hapa sitokubaliana naye. Hilo moja.

Lakini jengine mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni mswada nyeti katika nchi, kwa sababu ni mswada ambao utasaidia serikali pamoja na wananchi wake kuhakikisha kwamba hakutotokea tena madhara ya makusudi, haidhuru Mwenyezi Mungu anaandika, lile ambalo analiandika Mwenyezi Mungu halifutiki, lakini unaambiwa "*tahadhar kablal athar".* Sasa tuache utashi wa mtu kwamba ana biashara yake ya meli kama yumo ndani au nje. Hapa tunatunga sheria ambayo tulifoka sana katika Baraza lako tukufu hili Mhe. Naibu Spika, kutokana na uzembe ambao unafanywa na watu wetu wafanyabiashara wa boti.
Kwa hivyo, mimi nakubaliana na serikali, kwamba chombo kwa sababu hatujui chombo kile kule kwao kimetumika miaka mingapi na hapa kinaletwa tuseme miaka 20. Mimi hapa sikubaliani kabisa, nakubaliana kwamba miaka 15 ndio iwe kigezo, kwa sababu matatizo yaliyojitokeza Mhe. Naibu Spika, ni kutokana na kuchukua vyombo wenzetu wakavileta hapa vimechakaa, kwanza vyengine vimeshatumika miaka na miaka, halafu baadae kinakuja hapa kwa kukokotwa hivyo hivyo kufika Zanzibar tukakifanya kuwa chombo kile ni kipya. Kwa hapa mimi nakubaliana na serikali kuwa ni miaka 15.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitompa sifa yake Bakhressa. Kwanza nimsifu sana mfanyabiashara Bakhressa, pamoja na yote anapoleta vyombo analeta vyombo vya uhakika, lakini matengenezo kwake ni muhimu na ndio tukaona kwamba vyombo vya Bakharessa vingi viko katika *standard* ambayo inastahiki. Kwa hivyo, nimpongeze na nasema kwamba kwa kweli anastahiki kwa biashara yake ambayo anaifanya.

Lakini sio vibaya nikatumia nafasi hii hapa kupongeza jinsi alivyoweza kutengeneza pale bandarini napo kupaweka pahala ambapo panavutia kwa kivutio. Mhe. Naibu Spika, niungane mkono na mambo ya uokozi, nitagusia kidogo, Mhe. Ismail Jussa jana aliyazungumza sana. Kwa kweli uokozi ni kitu muhimu na bila ya uokozi hakuna linalokuwa katika mambo ya baharini, wataalamu. Sisi tumeshaagizia meli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa hivyo ni vyema tukaanza kufunza watu wetu, kama mtu ana kijicheti tukamuendeleza na wengine tukawapa mafunzo ili wasiwe watu wawili au watatu, hawawezi kuokoa watu wawili au watatu na jambo la bahari ni bahari Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, naiomba serikali kwamba tuhakikishe sasa hivi tunabadilika katika mambo yetu tusibakie pale pale.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nimelizungumzia kuhusu rushwa. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wizara yake iepukane na mambo ya rushwa. Siku nyengine sio miongoni mwa viongozi au wakurugenzi au makatibu wakuu, lakini kuna baadhi ya watu ambao wanajifanya wao ndio wenye bandari na kila kitu ni rushwa. Naomba sana hili Mhe. Waziri alichunguze na alikemee.

Mwisho niseme tu kwamba naupongeza sana mswada huu na mimi niseme kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi hii kuchangia mswada wa sheria ya marekebisho ya sheria ya usafiri wa baharini nambari 5 ya mwaka 2006.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchangia katika kifungu nambari 12 cha mswada ambacho kimeongeza marekebisho ya kifungu cha 17(a), ambacho kinasomeka, naomba kunukuu;

Kifungu cha 17(a)

> "Hakuna meli ambayo itazidi umri wa miaka 15 tokea tarehe ya kutumika kwake, itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa ajili ya kuchukua abiria na mizigo Zanzibar"

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana nacho kifungu hiki, ila namuomba Mhe. Waziri mambo yafuatayo ayazingatie. Kwanza Mhe. Naibu Spika, uaminifu na uadilifu kwa watendaji, watendaji wakiwa waaminifu na waadilifu katika kutekeleza majukumu yao, wanakuwa hawayumbi, hawarubuniwi na wanajiamini katika kutekeleza majukumu yao.

La pili Mhe. Naibu Spika, kuwepo na wataalamu wenye uzoefu na ujuzi na hasa hapa nasisitiza kwa wale wapasishaji wa meli na wakaguzi. Nasema hivyo kwa sababu hawa ni watu muhimu sana na waangaliwe kimaslahi. Natoa mfano kuna taasisi nyengine kama TRA, Mahakama na taasisi nyengine wanapata maslahi mazuri, basi na hawa wapasishaji na wakaguzi wa meli waangaliwe kimaslahi ili watende kazi kwa uadilifu na haki katika kutoa huduma.

Jambo la tatu Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu ukarabati na ukaguzi wa meli, kuwepo na utaratibu maalum ambao meli zetu zinakaguliwa na zinafanyiwa ukarabati. Hii itasaidia kuondosha zile dosari ambazo zinajitokeza na kuweza kuzichukulia hatua za haraka.

Mhe. Naibu Spika, katika hili naomba nitoe ushauri kwa Mhe. Waziri, kuhusu kuweka kanuni katika sheria hii ambayo itaiwezesha mamlaka ya usafiri ZMA kujua uhalisia wa meli tokea huko ilikonunuliwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee kuchangia kifungu cha 13 cha mswada ambacho kinazungumzia kuongezwa kwa kifungu 18(a) kipya ambacho kinasomeka, naomba kunukuu;
Kifungu cha 18(a)

> "Waziri anaweza kutunga kanuni zitakazoelekeza ukomo wa umri wa meli zisizokuwa za abiria kusajiliwa au kupata leseni Zanzibar"

Kifungu hiki nashauri kibaki kama kilivyo, kwa sababu sio vifungu vyote ambavyo vinatungiwa kanuni. Kifungu hiki kinajitosheleza na itamlazimu au ikibidi iko haja ya kutunga kanuni katika kifungu chochote basi apewe uwezo huo, kuliko kusema Waziri atunge kanuni, kama tunamlazimisha, wakati kuna vifungu vyengine Mhe. Naibu Spika, havihitaji kutungwa kanuni.

Mhe. Naibu Spika, sheria mama nambari 5 ya mwaka 2006 inampa uwezo waziri kutunga kanuni ili sheria itekelezeke vizuri. Sasa hapa naomba nimuulize Mhe. Waziri

1) Je, ni kanuni ngapi ambazo zinahitajika kutungwa katika sheria hii mama.
2) Mpaka hivi sasa ni ngapi zimetungwa.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 9 ambacho kinaongeza kifungu kipya cha 10(a) ambacho kinasomeka, naomba kunukuu;

Kifungu cha 10(a)

> "Hakuna mtu au taasisi inayoingia katika shughuli zozote zinazohusiana na usafiri wa baharini bila ya leseni au kibali kinachotolewa katika namna inayotekelezwa na mamlaka"

Mhe. Naibu Spika, hapa naomba iwekwe wazi ni mamlaka gani ambayo itatoa kibali hicho na ushauri nautoa katika kipengele hiki. Kwa sababu mamlaka zipo nyingi zinazoshughulikia mambo ya usafiri baharini. Kuna bandari, Shirika la Meli, ZMA na kuna Waziri mwenyewe pia ni mamlaka. Kwa hivyo, nashauri neno "mamlaka" kwanza liwekwe kwenye tafsiri, halafu kifungu hapa kieleze hasa ni mamlaka gani husika ambayo itakayotoa kibali hicho.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nilikuwa na pendekezo kuhusu uokozi. Naomba Mhe. Waziri kuwepo na utaratibu maalum wa shughuli nzima za uokozi. Kwa mfano vifaa vya kutosha na wataalamu, hii itasaidia Mwenyezi Mungu aepushie mbali, hatuombei litokee, likitokea ina maana tutakuwa tunalikabili kutokana na vifaa ambavyo tunavyo.

Mhe. Naibu Spika, pia ninashauri kupitia Mhe. Waziri na serikali kwa jumla kwamba kuwe na chombo cha *DNA*, kwa sababu matukio mawili ya ajali za meli yaliyotokea maiti nyingi zimeharibika na wala hazikuweza kutambuliwa na jamaa zao.

Kwa hivyo, kitakapokuwepo chombo hichi basi maiti hata kama imeharibika ikichunguzwa kwa mfano atakapokuja mtu atasema huyu jamaa yangu itachunguzwa damu yake na yule maiti na inaweza akatambulika maiti yule ni wa nani. Mhe. Naibu Spika, chombo hichi kitaweza kusaidia sana kutambua zile maiti ambazo zimeharibika.
Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Mswada wa Marekebisho Sheria ya Usafiri Baharini Nam. 5 mwaka 2006.

Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo mbele ya Baraza lako hili tukufu na kuweza kuchangia mswada huu.

Pili nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuamua kwa makusudi kutuletea Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Usafiri Baharini, tukizingatia madhumuni na sababu ya mswada huu unapendekeza kwamba kuweka mazingira mazuri mamlaka hii yaliyo bora ya usimamizi na masuala ya usafiri wa baharini, ili kuhakikisha yanatekelezwa ipasavyo kwa mujibu wa uwezo aliopewa.

Nianze mchango wangu kwa kusema kwamba sote ni mashuhuda wa matukio yaliyotokea hapo nyuma, ambapo tulishuhudia malalamiko mbali mbali yaliyotolewa na wananchi wetu pamoja na sisi Waheshimiwa kwa matukio yaliyotokea ya ajali za meli zetu tatu kama sikosei nadhani zilizotokea kwa muda wa kipindi kifupi.

Kwa kuzingatia hayo, Mhe. Naibu Spika serikali kwa makusudi iliamua kuunda Tume ya kuchunguza na kulifuatilia suala hili. Miongoni mwa mambo tume iliyayogundua ni pamoja na kasoro ya uchakavu wa meli hizi ambazo zinaingizwa nchini kwetu zikiwa zimeshatumika sana huko zinakotoka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa na karne hii ya sayansi na teknolojia tunayokwenda nayo kuna haja ya kufanya mabadiliko makubwa ya usimamizi wa vyombo vya baharini na kuweka mikakati madhubuti, ili kusimamia utekelezaji wake kwa lengo la kupunguza ajali zinazotokea, kwa maana zisiendelee kutokea na tukaonekana kwamba serikali inafanya mambo haya kwa makusudi.

Wakati huu wa sasa ni kusema kwamba vyombo chakavu katika nchi yetu viwe basi, visipokelewe kutokana na usimamizi mzuri wa mamlaka hii.

Nikiendelea na mchango wangu niende moja kwa moja kwenye kifungu cha 17A kuhusu umri wa vyombo ambavyo vinaingizwa katika nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja ya serikali na pia nasisitiza maamuzi ya Kamati yangu kwamba umri wa miaka 15 wa vyombo kusajiliwa katika nchi yetu ubakie hapo hapo.

Kwa kweli serikali ililiona suala hili na kamati ile ambayo iliundwa kwa ajili ya kuchunguza masuala yale ililiona hili, kwamba vyombo vingi ambavyo vinakuja katika nchi yetu vinakuwa vimeshatumika sana huko vinakotoka na vyengine vinakuwa vinabadilishwa maumbile yake.

Kwa mfano, kwao huko vinakotoka vina maumbile mengine lakini vinapokuja hapa vinabadilishwa na kubeba abiria na matokeo yake vinasababisha ajali mbali mbali ambapo inakuwa ni mzigo mkubwa kwa nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, ifike wakati tuseme sasa vyombo chakavu katika nchi yetu iwe basi.

Mhe. Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu mimi naomba umri huu ambao umewekwa wa miaka 15 tuukubali na tuupitishe mswada huu, ili iwe sheria na iweze kutumika.

Mhe. Naibu Spika, wananchi chombo chochote ambacho kitaletwa hapa katika nchi yetu kikeshasajiliwa hata kama kule kwao kimeshatumika muda mkubwa vipi. Lakini wananchi kwa vile wanakuwa na shida ya usafiri watakipanda na aghalabu vyombo vile vinakuwa ni vya bei nafuu, kwa hiyo lazima wananchi watapanda bila ya kuzingatia, kwa sababu wao wanakuwa hawafahamu kwamba chombo kile kimetumika huko kwao kwa muda gani.

Kwa hivyo, nadhani serikali imeamua hivi kwa makusudi, ili kuweza kunusuru matokeo mbali mbali ambayo yanayoweza kutokea katika nchi yetu. Kwa kweli mimi nasisitiza kwamba muda wa umri wa miaka 15 utoshe kusajili vyombo ambavyo vinaingia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Vile vile naiomba serikali iweke mkakati maalum tena madhubuti wa kulisimamia hili, kwa maana chombo chochote ambacho kitakachokuja hapa kama nilivyosema kwamba wananchi wakiekewa wao watapanda tu kwa sababu hawajui hasa kimetumika muda gani na kimetengenezwa muda gani.

Mhe. Naibu Spika, mimi zaidi ilikuwa ni kulitilia nguvu hilo moja ambalo nilipanga kulitilia nguvu. Kwa hiyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa asubuhi hii ya leo kuchangia mswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini, ambao kwa kiasi fulani Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia mswada huu.
Mhe. Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa maana hiyo mswada huu nimepata fursa ya kuupitia mara nyingi sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu muhimu wa Mamlaka ya Usafiri Baharini, ili kuifanya iwe bora zaidi mamlaka yetu pamoja na kuweka sawa usafiri wa baharini.

Pili Mhe. Naibu Spika, nilipongeze Baraza letu la Wawakilishi kwa kuandaa utaratibu mzuri wa kukutana na wadau, kwa ajili ya kutoa maoni yao kwa suala liliopo muhimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa kweli mswada ni mzuri lakini hata hivyo kila kizuri si kwamba kiachiwe na uzuri pale pale, isipokuwa kinahitaji kurekebishwa zaidi pamoja na kuwekwa sawa.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya kuwaita wadau ni kupata maoni yao na wao wanahitaji wakati wanapotoa maoni yao kusikilizwa na kuona kwamba hili kama linafaa, basi ni wajibu kulitunza na kulifuata. Mhe. Naibu Spika, tuliwaita wadau wa mswada huu na kuupitia kwa kina kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kuboresha vyombo vyetu vya baharini kwanza naiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ione kwamba hii Mamlaka ya Usafiri Baharini ni vyombo muhimu katika nchi yetu hasa ukizingatia kwamba Zanzibar ni visiwa. Kwa maana hiyo, baada ya kuwa ni visiwa basi lazima tutatumia vyombo vya baharini tukitaka tusitake.

Kutokana na hali hiyo, naiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ione kwamba mamlaka hii ni muhimu na iboreshwe kwa ajili ya kupatiwa wataalamu, ili kile tunachokifanya kiwe kinafanya kazi kwa vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu nakubaliana nao tena vipengele vipi, isipokuwa lazima tuangalie na nchi yetu ilivyo. Kwa mfano, baada ya kutokea matatizo Mhe. Rais wa Zanzibar aliunda tume maalum kwa ajili ya kuchunguza na kuangalia utaratibu wa nchi yetu. Lakini tume iwe inao wataalamu ambao wameteuliwa na Rais. Sasa yale mapendekezo yao wanayoyatoa wanatoa mapendekezo ya kitaalamu.

Sasa kipengele hichi cha 12 ambacho kuwa kinarekebisha kifungu cha 17 Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 12 kinarekebisha kifungu cha 17 kinaeleza hivi:-

> “Hakuna meli itakayosajiliwa katika nchi yetu ikiwa imefikia umri wa 15 isisajiliwe tena”

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wataalamu pale walipendekeza kama angalau kufikia miaka 20, yaani Mhe. Naibu Spika hii kwa uchache wa nchi yetu ilivyo basi hapa angalau ndio kiwango cha miaka 20 lakini miaka 15 ni kidogo mno.

Kwa maana hiyo, narudia tena kusema na mimi nilisema kwenye Kamati na leo nasema hapa kwenye Baraza kwamba miaka 15 ni kidogo mno, basi angalau hiyo miaka 20, kwa sababu lazima tuangalie na nchi yetu ilivyo, kwani tusije kuondoa matatizo tukaweka matatizo, na tutakapoona hakuna vyombo na hapa hatuna basi tutakuja kupunguza na watu watapata matatizo ya usafiri.

Kwa hivyo, lazima tuangalie na kiwango tunachoweka kwani hichi kiwango ni kidogo mno, miaka 15 ni kidogo na wataalamu walipendekeza miaka 20 na sisi humu Waheshimiwa Wajumbe wengi wanaosimama wanapendekeza angalau miaka 20.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika pamoja na kwamba sheria hii ni nzuri sana, lakini lazima tuangalie na utaratibu wa nchi yetu ulivyo na wala tusije tukajibana mpaka tukabanika kweli kweli. Kwa hiyo, lazima tujibane lakini tuangalie kidogo na utaratibu ulivyo, kwa sababu wadau wamelia na kusema kama wapatiwe angalau miaka hiyo na humu Wajumbe wengi wamesema hivyo.

Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba aliangalie hili pamoja na watendaji wake kama miaka 15 ni kidogo mno, basi angalau miaka 20.

Jambo jengine ambalo nataka niliseme kwa sababu watu wengi wanasema kama tulipata majanga basi sababu ni hiyo. Kwa kweli sababu si hiyo chombo kiangaliwe je kimetimiza yale masharti, kikaguliwe kila mara, je chombo hichi kiko imara kutokana na masharti yaliyomo yote.

Lakini kama hatuna wataalamu na wala chombo hakikaguliwi basi hata chombo kipya yaani meli mpya ikija leo, ikiwa haiangaliwi au haikaguliwi basi nayo itakuwa mbovu nayo na meli mpya inaweza kuzama pia na kongwe inaweza kuzama.

Kwa maana hiyo, jambo la msingi ni kuwa na wataalamu wa ukaguzi wa meli na kuweza kukagua mara kwa mara na wakatimiza masharti yanayotakiwa. Lakini kuwa meli ni mpya na kuna wenzangu waliotangulia walisema kwamba kuna meli inakaribia miaka 100 na ukiiona utafikiri ni mpya, kama meli kuzama basi duniani inatajwa hiyo tu na ilizama na wala si sababu hiyo na ilikuwa bado ni mpya.

Mhe. Naibu Spika, suala la msingi ni kuwa na wataalamu wakakagua meli kitaalamu, ikafanywa iwe bora na kutizama masharti wamekamilisha, basi meli hizo zifanye kazi.

Jambo jengine ni kifungu chengine nakubaliana nacho, ambapo meli yoyote iliyokuja ikawa haikutayarishwa tangu kwao kama hii ni meli ya kuchukulia abiria na mizigo, basi kweli meli hiyo haina haki ya kuchukua.

Vile vile ikiwa meli itakuja na kubadilishwa umbo lake la zamani, mimi naungana nacho kifungu hichi kama hiyo meli izuiliwe. Lakini ikiwa meli imeundwa tokea kwao ya abiria na mizigo, basi meli hizo zichukue abiria na mizigo baada ya kutimiza masharti tena kuna haja gani ya kuzizuia, nadhani zikaguliwe na ikiwa zimetimiza masharti basi zifanye kazi.

Mhe. Naibu Spika, jambo la msingi ni wataalamu na kutimiza masharti hili ndilo jambo muhimu katika nchi yetu.

Nikiendelea na mchango wangu naomba nipongeze wale wataalamu waliotoa ushauri wao kama kuna haja ya meli zetu kuwa na bima, kwa sababu bima inasaidia pale inapotokezea matatizo, lakini meli ikiwa inakwenda tu haina bima basi hiyo itakuwa haikutimiza hayo masharti. Kwa hivyo, moja ya masharti basi na bima iwe ni masharti na hilo naungana nalo.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mswada huu nimeuogelea mara nyingi basi sitaki nichukue muda wako mkubwa, basi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, ambaye ni msikivu aangalie Waheshimiwa Wajumbe wanavyochangia mswada huu, ili pasiwepo na kupingana na tuendelee kujenga nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii kwa ajili ya kuchangia machache katika mswada huu uliopo juu ya meza yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwenye marekebisho ya vifungu niseme kwamba sina wasi wasi kwa sababu nimeiamini Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa maoni yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli na mimi naomba niseme machache kuhusu utunzaji wa vyombo na siku zote watu wanasema kwamba ukitunze kidumu. Matatizo yanayojitokeza kwenye vyombo vyetu ni kwamba havifanyiwi ukaguzi na hali hiyo ndiyo husababisha maafa katika vyombo hivyo.

Ukaguzi kama walivyosema wenzangu ni lazima vyombo hivi vifanyiwe ukaguzi wa mara kwa mara. Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamesema tokea jana kwamba sisi si masikini wa kutunga sheria, kwa kweli sheria nyingi tunatunga lakini utekelezaji wake ndio unakua mdogo. Mimi niseme kwamba kweli utekelezaji wa zile sheria zenyewe unakuwa ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mswada huu naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha mbele yetu na kwa sababu hii ndio kazi ambayo tumeingia kwenye Baraza hili kwa ajili ya kupitisha miswada na ile ambayo imepitwa na wakati kuifuta.

Kwa kweli niseme kwamba nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu mbele yetu, kwa mnasaba ule ule wa kujadili na baadaye kuupitisha, ili kuiwezesha serikali yetu kufanya mambo yake vizuri. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye vifungu kama wenzangu walivyokwisha kuvichangia kuhusu kuongezwa kwa kifungu kipya cha 10A Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 10A (i) kinaeleza hivi:-

> "Hakuna mtu au taasisi itakayoingia kwenye shughuli zozote zinazohusiana na usafiri wa baharini bila ya leseni au kibali kinachotolewa na namna itakavyoelezwa na mamlaka".

Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi sina wasi wasi nacho. Lakini kuna kifungu chengine ambacho naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 10A (ii) kinaeleza hivi:-

> "Mtu yeyote atakayevunja masharti ya kifungu kidogo cha kifungu hichi atakuwa ametenda kosa na atahukumiwa kwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua dola elfu 5000".

Vile vile mimi naona labda kingeongezwa iwapo hatolipa hizo dola elfu 5000 basi kama kwa mujibu wa vifungu vyengine ipo adhabu nyengine ambayo ni kifungo na kiainishwe kwamba ni kifungo cha miaka mingapi.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye kifungu chengine cha sheria hii ambacho ni kifungu 17 ambapo Waheshimiwa Wajumbe wengi wameshakizungumza ni kuhusu umri. Kwa kweli mimi niseme huu umri ni kweli labda aidha tuainishe kwamba umri wenyewe, kwa sababu kuna vyombo vyengine vinaingia hapa vinakuwa tayari vimeshatumika muda mwingi ambavyo vinaingia katika visiwa vyetu.

Lakini kwa meli ile ambayo itakuwa ni mpya kwa miaka 15 kwa kweli ni kidogo na kwa sababu kama mwenzangu aliyemaliza kuchangia hivi sasa, kutokana na hali ya nchi yetu basi ni njema tutizame umri huu na hasa tukisema kwamba na siku zote watu wanasema kuwa ukimuelekezea kidogo mwenzio basi nyengine vinarudi kwako.

Kwa hivyo, kwa kuwa serikali yetu nayo inawajibika nayo kutafuta meli na tukiweka umri huu hasa ninavyojua kwamba taasisi za serikali mara nyingi zinakuwa kwa utendaji hakuna uwajibikaji wa hivyo na hata tukasema, kwa sababu unapofanya biashara huwa unategemea siku zote kuingiza.

Hata hivyo, tunaona kwamba kwa upande wa serikali ikianzisha chochote kile kinakuwa hakiko endelevu na hapa nina wasi wasi kwamba ya kuja kuvuja mapato, kwa sababu kila unachokifanya kwa sababu unapofanya biashara unataka urejeshe, ili kile unachokirejesha uweze kutafuta kitu chengine.

Sasa kwa upande wa serikali kwa miaka 15 bado ni kidogo na hata kile chombo chenyewe kikawa kipya ndio kabisa na haijambo labda kiwe hicho ambacho kimeshatumika kwa muda mrefu na mimi nina wasi wasi huo.

Vile vile naomba nitoe kumbukumbu ya meli zetu za serikali ambazo tulikuwa nazo hapa na nafikiri mpaka leo bado zinaendelea. Kwa mfano, nakumbuka meli ya MV. Mapinduzi nadhani mwaka 73 mpaka leo inakaribia miaka 40. Lakini kinachotizamwa kwamba zile ajali hazisababishwi na uchakavu, isipokuwa meli hizi zilizopata ajali ni kuwa uzembe wa kupakia abiria na mizigo bila ya mpango, kwa hiyo ni lazima kuwe na ukaguzi kabla chombo hakijaondoka basi kuwe na ukaguzi.

Pia wamiliki wa vyombo wahakikishe kwamba abiria walioingia mule ni sawa, lakini utaona hata hivi sasa bado pamoja na kutokea majanga mengi, lakini bado unakuta tiketi haziko kwenye umiliki wa wenyewe, yaani tiketi unazikuta ziko mikono mwa watu na haya ndiyo yale yanayosababisha kutokea majanga na kupotea kwa watu wetu wengi sana.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba umri wa hizi meli kwa kweli tuzingatie labda kama imeshatumika kwa hiyo tunaweza kuweka muda maalum.
Baada ya hayo, Mhe. Naibu Spika mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani mswada huu nauona ni mzuri na bila ya kupitishwa miswada na sheria serikali haiwezi kufanya mambo yake kwa vizuri na kufanikiwa. Kwa hivyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kusema machache na kwa vile leo siku ya Ijumaa sitaki niwe na mengi nitasema machache kwa wakati huu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla sijaenda mbele ningependa labda nikamtaka Mhe. Waziri akaangalia marekebisho aliyoyafanya, yaani marekebisho ya karatasi aliyotupa, ambapo mamlaka inaweza kushirikiana na Mamlaka inayosimamia mambo ya baharini Tanzania Bara.

Nadhani hapa ameacha neno muhimu sana, kwa sababu lengo ni usafiri. Kwa hiyo, ningependa kuongeza neno usafiri wa baharini Tanzania Bara na tukiacha hivi tu, mambo ya baharini ni mengi. Kwa maana hiyo, inaweza kutumika fursa njema na kuleta dhana nyengine, kwa mfano baharini kuna uvuvi na mengineyo. Kwa hiyo, labda neno usafiri katika kifungu cha 6(3) tungeongeza, ili kuleta maana zaidi ya mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho haya yamekuja baada ya kutokea yaliyotokea katika nchi yetu na mara nyingi tunapokuwa tunaleta marekebisho, basi huwa tunakusudia kulenga zaidi na kutaka yale ambayo tunahisi yana mapungufu, basi tuyarekebishe kwa sheria mpya inayokuja au tunayotarajia kuiunda.

Mhe. Naibu Spika, kila nikiangalia nahisi kwamba sheria hii ni nzuri, lakini bado ina mapungufu mengi sana, kwa sababu imekuja kama vile kurekebisha jambo moja tu na lile la uchakavu wa meli, kwamba sasa tunataka meli ziwe na aina fulani na mengine mengi na ambayo labda yamependekezwa na zile tume zilizoundwa nahisi yamesahauliwa.

Katika kuepusha mengi na hasa yale yaliyotokea hii moja peke yake haitoshelezi na sisi zaidi tumezingatia ubora wa meli tu, lakini tumeyaacha mengi ambayo yangetusaidia.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wanakuwa na vyombo vinavyotembea katika maji ya bahari ya chumvi na labda vyengine vinatembea kwenye maji ya kawaida, yaani maji ya mto na hili ndilo linalotokea. Lakini sijaona humu katika marekebisho haya na vyombo vinavyokuja hapa kwetu, nina imani kwamba vyengine vinakuwa vinatokea katika mito huko kwa wenzetu *Red Sea*. Lakini baadaye zinakuja ku- *operate* katika bahari ambazo uwezo wake nina imani ni mdogo. Nahisi sheria hii pia izingatie mambo kama hayo ya kuangalia miaka tu kwamba iwe na umri si zaidi ya miaka 15 si kigezo. Kuna upandaji wa meli, kuna upakiaji wa mizigo, pia yote yalitakiwa yawe na utaratibu wake na ingepangiwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mwanzo nilisema kwamba sheria hii ina mapungufu. Nasema hivi kwa sababu moja au mbili. Ninachokijua mimi kwa miongo mingi sasa, karibu miwili na kuendelea nchi yetu ilikaribisha watu kuja kuwekeza katika sekta ya baharini. Wananchi wetu wengi walijitokeza wazalendo wakasema sisi kwa vile serikali kwa wakati huu ina majukumu mengi ya kufanya basi tutajitokeza na tutaingiza mapato yetu katika kuleta meli ambazo zitasaidia usafiri wa hapa na pale. Sisi tuliokuwepo katika mwambao huu wa Afrika Mashariki tuna sukumwa na tunapangiwa na baadhi ya misemo ambayo hutusaidia kuzingatia baadhi ya mambo.

Tunachokifanya ni kama vile ule msemo wa Kiswahili unaosema **"**Lishalovusha ni gogo**"** Leo kwa muda wote wananchi hawa wameingiza pesa zao, wame-*invest* katika usafiri, lakini tunakuja na sheria ambayo wao hawakuzingatiwa hata kidogo kwamba fedha zao zimetumika na wengine wana madeni, tukaleta sheria ambayo nina imani kwamba itakapotiwa saini wengi watakufa. Hawatakufa kwa sababu ya meli zao kwamba zitazama lakini watakufa kwa sababu pesa zao zitakuwa haziwezi kufanya kazi tena zikawapatia manufaa ya kuendesha maisha yao.

Baada ya kutokea matokeo haya Mhe. Spika, na serikali kuona umuhimu lakini umuhimu wa kuleta meli na umuhimu huo tuna imani pengine utachukua zaidi ya mwaka mmoja. Wengi walijitokeza wakaona kwamba sasa ipo haja ya kuwa hili lilokwisha kutokea ili lisitokee tena wakasema walete vyombo. Hivi sasa vimetia nanga bandarini, vyombo vile havipewi ruhusa ya kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyengine.

Mimi ningelipenda kuiomba serikali kwamba haya tuliyoyafanya yazingatie kwamba tuna wazalendo katika nchi hii waliojitolea kwa hali na mali kuhakikisha tatizo la usafiri katika nchi yetu limeondoka. Kwa sheria hii inayokuja nina wasi wasi kwamba hawa wenzetu watarudi nyuma sana kwani wamefungika. Hasa tukiangalia Mhe. Naibu Spika, hichi kipengele cha 17 kinachosema kwamba ili meli isajiliwe basi isizidi umri wa miaka 15.
Mhe. Naibu Spika, hichi ni kipengele kizito, nina imani hatakama hiyo meli iliyopangwa kuja ya serikali itakuja, basi haitotatua tatizo la usafiri ni lazima washirikiane na wadau wa sekta nyengine ili kuondoa tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa yako hivi sasa hasa tunapokuwa katika mwezi wa Disemba inakuwa kuna usumbufu mkubwa wa usafiri baina ya Unguja na Pemba na Unguja na Dar-es-Salaam. Ninaimani hilo serikali hailiwezi. Ningeomba ingeangalia kwa makini kwa nini leo tulete sheria ya miaka 15. Je, hivyo hii meli ikiwa ni nzima ina umri wa miaka 5 haiwezi kutokea yaliyotokea. Jawabu mimi nasema yanaweza yakatokea. Kuweka kigezo cha umri wa kuwa iwe ni miaka 15 si sababu ya kuepuesha hayo, kuna mengi ya kufanywa.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachokifahamu katika karne hii ya leo sayansi ndio inayotumika zaidi kuliko uelewa wa mtu wa kubahatisha. Hivyo tujiulize hivi vyombo vinavyoingia vinavyotengenezwa vinakuwa haviwekewi *life span* ukajua kwamba meli hii au boti hii imetengenezwa mwaka gani na itamaliza muda wake kipindi fulani, havifanyiwi hivyo na hawa wanaovitengeneza. Kiasi kwamba leo tufike sisi tupange tu miaka 15 iwe mwisho na wao wanavigezo vyao vinavyotambulika na wana vigezo zinavyokubaliaka kwa sababu ni vya kisayansi. Nafikiti ni vyema tuelekee huko zaidi, tuende katika vigezo vya kisayansi kuliko kuweka sisi.

Mhe. Naibu Spika, leo kwa sheria hii imeshazua mengi, wengine wanaona kuna wengine wanataka kuja hivi. Bi Asha Bakari alisema hapa kwamba kutatokea rushwa ndani yake kwamba huyu atakuwa hivi, huyu atakuwa vile. Hebu tuondokane na haya tuende katika mfumo wa kileo kabisa, sayansi itumike. Kama chombo kinakuja hapa hakina *life span* moja kwa moja kitakataliwa na ikiwa chombo kama *life span* yake miaka 7 basi kiruhusike kutumika miaka 7 tu, sio miaka 15 na kama *life span* yake miaka 30 basi kitumike kwa muda wa miaka 30. Hiyo *inspection* ya kila leo ya mara kwa mara itaendelea kutumika. Lakini tukiweka moja kwa moja kwamba leo tuwe na kikomo cha miaka 15 hawa wenzetu waliotusaidia katika kuboresha sekta hii ya usafiri wa baharini baina ya visiwa vyetu watarudi nyuma.

Nina imani sasa tutakuwa hatuna uwezo tena kwa sababu wao hawatoweza kujitokeza. Mimi sijui gharama za chombo kimoja kinagharimu kiasi gani. Lakini ukimwambia wewe lete chombo ndani ya miaka 15 basi faida yake pengine isiweze kufikia akawa yeye keshalipa faida yake, kweli Mhe. Naibu Spika, atakuja huyo awekeze katika nchi yetu tena. Naomba Mhe. Waziri kipengele hichi akiangalie tena kwamba kuweka umri wa miaka 15, haitotusaidia sisi chochote, lakini kuna taratibu nyengine zaidi, zinazotaka ziangaliwe ili kuhakikisha kwamba hayo yanayotokea hayatokeo.

Mhe. Naibu Spika, humu niliona katika Mswada wetu tumetaja neno SUMATRA lakini tukalifuta au tumesema tutumie chombo cha usafiri wa baharini chenye mamlaka ya kusimamia usafiri wa baharini Tanzania Bara, wengi wamependekeza chombo hichi kisiwepo. Kwa kumbukumbu zangu mwaka wa 1997 wakati Baraza hili linapitisha Mswada huu chombo hichi kiliondoshwa na kilitakiwa kisiwepo. Lakini pia hata kama kitakuwepo mimi ninaesema ni mmoja sijui wenzangu wataunga mkono kiasi gani. Nina wasi wasi kwamba kama tutaondosha neno SUMATRA hapo baadae tunapokwenda mbele inawezekana katika Tanzania Bara kikatokea chombo chengine ambacho hakitaitwa SUMATRA nacho kitasimamia usafiri wa Baharini. Je, nacho kilikotokea katika hali kama hiyo pengine ni sekta binafsi wakajiingiza katika kusimamia usafiri bahari, hivyo nacho kitakuwa na mamlaka ya kusimamia mambo ya usafiri wa vyombo vyetu, au tulichokusudia hapa ni hii SUMATRA tu. Kama tumeikusudia SUMATRA kwa nini tuiyondoe.

Mhe. Naibu Spika, hizi lugha napenda tungezitumia vizuri. Kwa sababu ukisema mdudu huyu anaonekana usiku macho yake makubwa anakuwa moja kwa moja ni bundi. Sasa wewe ukisema chombo kinachosimamia Usafiri wa Baharini Tanzania Bara moja kwa moja ni SUMATRA. Sasa leo unataka eti tusiiseme, *automatically* inakuwa ni hiyo, kwa hiyo kutaja kwake inatupa faida na itaipa faida hii sheria. Kwa sababu anaweza akaja akatokea mwengine akasimamia suala

hilo asiyekuwa SUMATRA, je, na yeye atakuwa na mamlaka. Ningependa hili pia Mhe. Waziri nalo akaliangalia kwa kina.
Mhe. Naibu Spika, leo Ijumaa, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwamba wachangiaji wetu wamemaliza sasa hivi na tunategemea jioni tumwite Naibu Waziri na Waziri kufanya majumuisho. Ninaloomba kwenu tuje mapema. Mtu aje asikilize hoja zake alizouliza ili apate majibu. Vyenginevyo akijakuuliza mtu wakati wa kupitisha vifungu na hakuwepo, hatuwezi kumsikiliza.

Baada ya hayo nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuwa muda wetu wa kumalizia haujatimia, atoe hoja ili tuweze kuakhirisha Baraza hili hadi jioni.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa vile muda uliobaki hautotosha kumuwezesha Mhe. Waziri kufanya majumuisho na kwa vile muda haujatimia wa kukamilisha Kikao cha asubuhi cha Baraza, naomba kutoa hoja na kuliomba Baraza lako Tukufu itengue kanuni ya muda ili kuliakhirisha Baraza kabla ya muda wake kwa ajili ya kujitayarisha kwa Kikao cha jioni.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Naakhirisha kikao hichi hadi Saa 11 za jioni.

(Saa 5:35 Asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi Saa 11:00 Jioni leo)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, na mimi ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kuchangia machache tu juu ya mswada huu wa sheria ya marekebisho ya sheria ya usafiri wa baharini namba 5 ya mwaka 2006.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano na kwa kuleta fikra hii ya kuifanyia marekebisho sheria mama. Ninafikiri kimsingi Waheshimiwa sote tumeona umuhimu wa kufanya marekebisho ya sheria mama hasa baada ya matukio yale mawili ambayo yameliathiri taifa letu kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hivyo mimi niipongeze Wizara baada ya kuona mapungufu katika sheria mama ile ya mwaka 2006 na kuja na marekebisho, na ni imani yangu kwamba marekebisho haya yatatusaidia sana katika utendaji, katika ununuzi na suala zima la safari za meli kwenye bahari ile.

Mhe. Naibu Spika, kuna Waheshimiwa walichangia suala zima la uokozi na hilo nataka mimi nilitolee maelezo machache zile juhudi za serikali mbali ya Wizara yenyewe lakini katika vikosi vyetu vya ulinzi na usalama hasa katika masuala haya ya uokozi. Lakini moja naomba nilitamke na pengine baadae mwenyewe Mhe. Waziri atakuja kulitamka kwa kirefu ni suala la kinga, niseme na kinga yenyewe kwamba kila chombo kinatakiwa kwa sheria kiwe na *life jackets* yale makoti ya uokozi kama kwenye ndege au kwenye meli lazima wenye boti zile wanatuelekeza jinsi ya kuzitumia wakati wa ajali na wanatuhimiza japo unajua kutumia lakini uchukue yale mambo ya hadhari ujue hata kwenye ndege wanaelekeza japo unajua ushasafiri sana lakini usikilize yale maelezo ikitokea dharura ufanye nini, hili suala la msingi sana. Na yale yanasaidia sana wakati wa ajali katika suala zima la uokozi.

Mhe. Naibu Spika, katika kikosi chetu cha KMKM au kwanza niseme kwa ujumla kwamba baada ya lile tukio la mwanzo la ajali ile ya Spice Islander One basi tuliagizwa tutafute vyombo au uwezekano wa kupata vyombo ambavyo vitafika kwenye lile tukio la ajali kwa haraka sana, na sio kufika tu lakini wakishafika waweze kuokoa wale watu ambao bado hawajazama au wale waliozama lakini hawajafa. Sasa tukio hilo sasa tumelichukua Wizara na tuliwatuma wataalamu wetu wawili kwenda India kuangalia uwezekano wa kupata boti kule wana kiwanda katika jimbo la Kirala kinatengeneza boti tumewatuma kule na wakaja na mapendekezo mazuri tu kule wameona kuna kiwanda kinajenga boti ambazo kwa lugha ya siku hizi ni *faster* zinakwenda kwa *speed* 45 la kukimbia kwa haraka sana. Kwa hivyo inasaidia kufika katika tukio la ajali kwa haraka sana, lakini pia zina uwezo wa kukaa baharini bila ya kujaza mafuta na maji kwa zaidi ya wiki mbili. Pia boti hizo zina uwezo wa kuhimili mawimbi makubwa.Tutakumbuka ajali ya pili ile ya MV Skagit pale tukio la ajali palikuwa na mawimbi mazito, kwa hivyo vyombo vyetu vilipata tabu katika suala zima la uokozi.

Kwa hivyo vyombo hivi tulivyoelekezwa vina uwezo wa kufika kwa haraka sana katika eneo lile lakini pia zinaweza kukaa zikatulia pale na ziko chini zikaweza kufanya suala zima la uokozi. Sasa tumezingatia kama alivyoeleza Mhe. Mohammed Aboud asubuhi, kwa kipindi hiki tuna matatizo ya fedha lakini tutakaa kama serikali na Wizara ya Fedha kuona kwamba hebu tuanze kupata alau boti moja kwenye sifa hizi azma yetu tupate boti mbili, moja ikae Unguja na moja iende Pemba. Lakini kwa kuanzia tuone ile moja itafanya kazi vipi na ufanisi wake na ninaamini itatusaidia mbali suala la ulinzi lakini katika suala zima la uokozi, hili suala la uokozi ni suala la msingi sana na tutalitilia maanani sana.

Mhe. Naibu Spika, juhudi nyengine ambayo serikali imefanya ni suala zima la mafunzo kwa askari wetu, mafunzo haya hasa ya kuzamia. Mhe. Naibu Spika, hivi juzi tu tulitoa mafunzo kwa vijana wapatao kama 30, 22 wamehitimu na 8 kidogo mafunzo yao hayakukamilika tunasubiri kidogo kama mwezi mmoja hivi waje wakamilishe. Na katika hao 22 basi wanawake 8 kwa makusudi tumewaweka hao 8 kwa sababu yakitokea majanga kama haya kusiwe na matatizo ya kuwasaidia kinamama. Tunajua kinamama wanataka *handling* ya aina yake. Kwa hivyo tumeona *handling* kama ile vizuri na wao kinamama tukawafunza. Kwa hivyo tunao vijana shababi, wazuri tu wa kike wanaweza kuzamia kwa ukakamavu, kwa hivyo hao Mhe. Naibu Spika, wameshapatiwa mafunzo na ni imani yetu kwamba wana uwezo au watakuwa na uwezo wa kuokoa watu waliozama, Pia watakuwa na uwezo kwa kuokoa watu walionasa katika meli. Lakini vile vile watakuwa na uwezo wa kuzamia hata wakati wa usiku mbali ya mchana

wataweza kuzamia hadi kina cha mita 25. Kwa kweli hayo ni mafanikio makubwa sana na pia watakuwa na uwezo wa kutoa huduma ya kwanza.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo haya tunayafanya au tumeyafanya kwa kushirikiana na wenzetu wa *red cross* tumeshirikiana pamoja kuweza kusaidiana nao. Lakini Mhe. Mwenyekiti mafunzo haya yatakuwa yakiendelea na kwa kipindi kilichopita walitusaidia kampuni ile inaitwa LNW kutoka Uingereza, tumeekeana mikataba watakuwa wanakuja mara kwa mara kuweza kutoa mafunzo kama haya.

Sasa suala hili la uokozi si kama la vikosi tu peke yao inapotokea ajali, ajali ni kitu hakitarajiwi wakati wowote inaweza ikatokea. Kwa hivyo ni suala la msingi kwamba sote tuna wajibu kwamba inapotokea ajali basi tuweze kuacha unachokifanya ili tuweze kuhami roho za watu. Na tunashukuru sana kwa ajali zile mbili za meli zilizotokea mbali ya serikali lakini watu binafsi; Nungwi kule na hata hapa Malindi walisaidia sana na wao katika kukimbilia katika matukio ya ajali huu ni mfano mzuri sana na walitusaidia sana tunawashukuru sana. Kwa hivyo pale hakuna suala la hakuna mafuta hakuna nini, kilichopo wewe kamata ukimbilie kwenye ajali, hii ndio utaifa pale kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri wa Afya ni kuhami maisha. Kwa hivyo ni imani yangu kabisa Mhe. Naibu Spika, kwamba sheria tutasaidiana nayo na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuona kwamba maisha yetu au tunakinga ajali kama hizi.

Lakini zaidi juhudi nyengine Mhe. Naibu Spika, ni lile suala la msaada wa wenzetu wa EU katika kuisaidia KMKM, wamejitokeza wenzetu wa EU wamekuja kuna mtaalamu wao mmoja kutoka *European Naval Forces Liaison Office* yupo Dar es Salaam pale anaitwa kamanda John Kelly yeye amekuja na ametuuliza nini mahitajio yenu katika suala hili mbali la ulinzi lakini hata uokozi. Kwa hivyo tunafanya kazi nae kwa karibu, kubadilishana mawazo na tunazingatia suala zima la usalama wa baharini yaani *maritime Safe measures*. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nilitaka kusema tu kwamba serikali ina mipango kabambe au madhubuti ya kuona kwamba mbali ya kurekebisha sheria lakini tunaimarisha hata masuala mazima ya uokozi na mawasiliano ya vyombo vyetu, ili tuone wakati wapo baharini basi wanawasiliana na wenzao walioko nchi kavu kama suala la ndege vile kuona kama kutatokea chochote basi wanataarifiana mara moja na watu wana-*rush* kwenye tukio la ajali mara inapotokezea.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli sina mengi nilisema nichangie kidogo mawili matatu haya kuonesha juhudi za serikali ilizozifanya katika masuala mazima ya kuimarisha masuala ya uokozi.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma yeye ndie ambaye ametuwezesha sisi kuwa hapa kufanya yetu tunayoyafanya kwa msingi wa kutaka kuwasaidia wazanzibari katika hatima yao njema hasa hasa kwa jambo hili ambalo tuko nalo leo la usalama wao katika harakati za usafiri kwa vyombo vya baharini.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya hilo naomba nitamke wazi kwamba mimi naunga mkono marekebisho haya ya sheria kwa asilimia 100 mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka.

Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi nitoe mchango wangu, mchango wangu mimi unaweza ukatofautiana kidogo kwani mchango wangu utalenga katika kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wameuliza katika mnasaba wa marekebisho haya ya sheria husika.

Mhe. Naibu Spika, kuna maeneo mengi ambayo wameomba na wamehitaji ufafanuzi na naomba nichukue nafasi hii kwa kuanza bila ya kuwataja majina kwa mnasaba huo wa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo.

Mhe. Naibu Spika, limezungumziwa eneo moja muhimu na namna ya chombo chetu cha ZMA kiasi gani na kwa namna gani kitaweza kutekeleza, kusimamia sheria iliyopo lakini pia kwa namna gani au kwa kiasi gani kitaweza kujiimarisha katika shughuli zake za ukaguzi wa vyombo vya baharini.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya mabadiliko haya sheria iko wazi nguvu walizokuwa nazo, wajibu waliokuwa nao ZMA na kazi ambazo wako nazo ZMA. Naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wawakilishi kwamba dhamira ya mabadiliko haya itakuwa ni chachu katika kusimamia na kutekeleza yale maeneo ya ufanisi katika harakati zote likiwepo suala la usimamizi pamoja na kuimarisha huduma za ukaguzi. Natambua katika suala la ukaguzi limezungumziwa suala la kuboresha mafao au maslahi ya wafanyakazi wetu. Hili tumelipokea na tunaamini kwamba pamoja na uchanga wa chombo hiki cha ZMA kwa kutambua tu kwamba chombo hiki kimezaliwa rasmi mwaka 2011, tunaamini kwamba haja hiyo, umuhimu huo wa kuimarisha kwa kuwaboreshea maslahi yao wafanyakazi hawa yanaonekana wazi. Na sisi kama wizara tutahakikisha kwamba ZMA wanaangaliwa kwa jicho la karibu sana hasa hasa wakaguzi hawa wa vyombo ili kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi na kuleta tija kama ilivyolengwa.

Mhe. Naibu Spika, suala la pili lililozungumziwa ni kuhusiana na idadi ya kanuni ambazo ZMA wamepaswa kutunga, kwa mujibu wa sheria ile namba 5 ya mwaka 2006 ZMA ilitakiwa iwe na kanuni zisizopungua 42. Lakini kwa kutambua changamoto ziliopo, hadi muda huu ZMA wameweza kutunga kanuni 5 na matarajio yetu kwamba kanuni zilizosalia zitaweza kutungwa haraka kwa kutambua tu kwamba chombo hicho sasa kimeanza kupata nguvu baada ya kuweza kupatiwa fedha kutoka katika mfuko mkuu wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna eneo jengine lililouliziwa kuhusiana na adhabu pale pindi kama mtu atashindwa kutekeleza matakwa ya sheria hii ukiangalia kifungu cha 464 kifungu kidogo cha tatu kimeeleza wazi utaratibu wa mtu ambaye atashindwa kutekeleza maelekezo ya sheria hii kwa kuadhibiwa kwa kifungo kisichopungua miezi mitatu lakini pia kwa kifungo kisichozidi miaka mitatu.

Aidha tunakubaliana na ushauri uliotolewa katika mapungufu ya neno usafiri katika kifungu nambari 3 *sub section* 3 baada ya neno baharini kulikuwa kuna neno usafiri ushauri huo tumeuchukua na tunakubali kuufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, limezungumziwa suala jengine lilikuwa suala la minara, maboya pamoja na vyombo vyengine vinavyoongoza katika harakati za shughuli za usafiri baharini. Naomba nilijulishe Baraza lako tukufu kwamba chombo chetu cha Shirika la Bandari linafanya kazi kubwa ya kuimarisha huduma hii muhimu ya minara, maboya kwa kubadilisha mfumo uliopo wa taa zile ambazo zilikuwa zikitumia gesi kama tunavyojua kwamba teknolojia hiyo kwa kipindi hiki imeshaondoka duniani, hivyo kuendelea kuwa na teknolojia hiyo kunapelekea kuwa na gharama kubwa katika uendelezaji na uimarishaji wa huduma hiyo. Utaratibu uliopo hivi sasa wa kuweka taa za *solar* tunaamini utakuwa ni wenye tija na faraja lakini pia ufanisi na matarajio yetu ni kwamba utaratibu huu utakuwa katika kipindi kifupi utakuwa umekamilika kwa maeneo yote.

Hivyo basi, kwa yale maeneo ambayo bado utaratibu huo haujafika tunawahakikishia Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wananchi kwamba tuko katika hatua za mwisho ili kukamilisha, shirika letu hili limeingia mkataba na kampuni ya UAE ili kuweza kufanikisha jambo hilo.

Mhe. Naibu Spika, pia limezungumziwa suala la bima, mabadiliko yetu haya ya sheria naomba tuungwe mkono ili kuweza kufanya biashara hii ya usafirishaji wanadamu katika vyombo basi wale wanaohusika wakate bima na kiwango hicho cha milioni kumi kama tulivyolenga ili tuweze kuwafikia wenzetu pale wanapotokewa na majanga.

Lakini pia limezungumziwa suala la ID ikiwa ni pamoja na suala zima la uuzwaji wa tiketi kiholela. Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kidogo namna ya kuweza kukabiliana na changamoto hii ya tatizo la uuzaji wa tiketi kiholela. Jambo hili ni suala Mtambuka, sisi kama Wizara moja hatuwezi kulifanya kwa ufanisi tukaweza kufanikiwa. Linahitaji wadau na tunaamini kwamba serikali kwa pamoja tunaweza kulichukulia hatua. Jambo hili ni jambo la kusikitisha wadau muhimu ambao ni wananchi wanaokwenda kununua bidhaa hizi hawajawa tayari kuunga mkono azma na jitihada za serikali katika kupiga vita biashara hii ya magendo au biashara ya ulanguzi. Jambo liliopo ni kwamba wanafanya biashara hawana leseni, wanafanya biashara hawatozwi kodi. Lakini katika hali ya kushangaza pamoja na ku-*introduce* utaratibu mpya wa kuuza tiketi kwa njia ya *electronic* ili kuhakikisha kwamba yule msafiri aliyelengwa ndie mwenye kuuziwa tiketi, jambo hili nalo pia kwa bahati mbaya wenye kampuni za shughuli za usafiri wamekuwa hawatuungi mkono kama vile matarajio ya serikali. Ninachokuhakikishia kwamba tutarudi tena wizarani kwa kushirikiana na serikali pamoja na vyombo husika ili tuone kwa nguvu zetu zote tunakwenda kulisimamia hili na kuona tija kama ilivyolengwa.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine limezungumziwa suala la usajili wa nje. Usajili wa nje katika utaratibu wa usajili wa meli kuna taratibu mbili ile tunayoita *domestic registry* na *open registry*. *Open registry* maana yake ni usajili ule wa kimataifa na sisi ZMA tuna kampuni ambayo imeingia mkataba na serikali kwa ajili ya kufanya shughuli za usajili wa meli kwa madhumuni au kwa malengo au kwa niaba ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya chombo cha *Zanzibar Maritime Authority*. Kampuni hii ni Filtex na ni kampuni ambayo inafanya kazi zake vizuri, tija na mapato tumeyaona na tunaamini kwamba itakuwa ni miongoni mwa chachu ya kuimarisha taasisi yetu ya ZMA kama zilivyo nchi nyengine kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine lililozungumziwa ilikuwa ni suala la *signal tower,* kwa malalamiko kwamba kazi za *signal tower* zinafanywa kwa *radio* ambayo inatolewa mkobani mwa mfanyakazi anapiga baadae inarejeshwa mkobani, jambo hili Mhe. Naibu Spika, si jambo la ukweli. Kituo cha *signal* kilikuwa kipo katika jumba la Beit El Ajaib na sote ni mashahidi kwamba jumba lile sasa hivi limepata tatizo ya hofu la kuporomoka, hivyo tumeona kwamba ni busara na hekima ya kuondoa mitambo yetu ile kwa kutambua tu kwamba mitambo iliyopo pale ni mitambo ya gharama kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, katika eneo hilo la *signal tower* kuna mtambo ambao ni muhimu, mtambo wa kisasa mtambo wa GMDSS mtambo ambao una uwezo wa kugundua au ku-*allocate* chombo katika *diameter* ya kilomita 75 ambayo inayo uwezo wa kuona karibu ya Msumbiji na zaidi ya Pemba ukiwa upo Zanzibar. Chombo hiki tumeona ni vyema na busara kukiondoa pale kwa kutambua kwamba chombo hiki kingepata maji kingeweza kuathirika.

Aidha mbali ya chombo hiki kuna chombo chengine cha AIB chombo ambacho tumepata msaada kutoka katika serikali ya Ufaransa, chombo ambacho kina uwezo nacho wa kusaidia namna ya kuweza kujua na kujilinda masuala ya kiharamia kwa kutambua chombo namna gani kilipo, mwendo gani kinakwenda, kimepakia mzigo gani na kina muelekeo gani. Katika jitihada hizi Shirika la Bandari limeingia katika harakati za kutafuta eneo jengine la kuweza kuweka mitambo hii katika maeneo ya juu. Na tunashukuru wapo katika hatua ya mwisho ya kuingia mkataba na Shirika la ZSTC kwa ajili ya kutumia jengo la ZSTC liliopo eneo la Kinazini ili kuweza kutoa huduma hii muhimu kama tulivyoitaja hapo kabla.

Mhe. Naibu Spika, naomba niongezee katika eneo ambalo limechangiwa na wengi hasa hasa suala la umri wa meli. Mimi naomba niseme kidogo sana Mhe. Naibu Spika. Naomba tutambue kwamba madhumuni makubwa ya chombo hiki ni kuwatetea wananchi ambao wako wengi, ambao kwa namna yoyote haki ya kusafiri kutoka eneo moja kwenda jengine ni hali ya kikatiba. Kama hivyo ndivyo naomba sana tutumie busara, hekima na uzalendo ule ule wa kuwalinda wananchi wetu kubaki katika eneo salama.

Dhamira ya serikali ni kuona kwamba kiasi hiki cha miaka 15 kinakidhi kwa chombo kuweza kutoa huduma za usafiri kwa kutambua tu kwamba kuna vyombo vingi hasa meli ukiangalia *life span* yake si muda zaidi unaozidi miaka 25 ama 30. Sasa madhumuni ya serikali ni kuona kwamba miaka 15 ili kumpa nafasi ya miaka 10 kuweza kufanya biashara na kurejesha gharama yake. Sasa malengo ya serikali ni kuwalinda wananchi wake na watumiaji wengine wa huduma za usafiri kusafiri katika vyombo vilivyo salama vitakavyowaokolea maisha yao. Kinyume ya hapo naomba niseme kwamba suala la biashara anafanya mwenye uwezo. Suala la biashara ni ushindani, na ushindani siku zote anashindana mwenye uwezo wa kushindana. Sasa chombo hiki kisije kikajielekeza katika kutaka kutenda jambo la kuashiria kwamba ushindani wa kibiashara uwe haupo kwa msingi wa kuweka vigezo vitakavyoashiria kila mmoja aweze kufanya jambo hilo.

Msingi mkubwa nadhani tumeelekeza katika kuhakikisha usalama wa maisha ya wananchi wetu tunaowalinda na kuwakinga na majanga. Kinyume ya hapo tutakuwa hatuwatendei haki wala hatuwatendei jambo jema. Madhumuni ya serikali ni kuona kwamba wananchi hawa walio

wanyonge walio wengi waweze kusafiri katika vyombo vilivyo salama wakitoka eneo moja kwenda eneo jengine.

Serikali imezingatia kwa makini sana na kutambua na kufanya tathmini kwa hali ya juu kuona kwamba umri huu wa miaka 15 ni umri ambao ungekidhi kwa ajili ya kutaka kutoa huduma. Na ile azma ya kutaka kwamba wafanyabiashara wenye uwezo, wafanye biashara hii kwa kutambua na wale wafanyabiashara wadogo wadogo wanayo nafasi ya kujikusanya kutengeneza ushirika utakaoweza kufanya kazi hiyo kwa kutambua ule umuhimu na usalama na watakuwa wamewapa kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, naomba niliseme hili kwa kutambua tu kwamba lengo la serikali maisha yote ni kuhakikisha usalama wa wananchi wake ndio kipaumbele nambari moja. Bila ya kutoa usalama kwa wananchi unaowaongoza sidhani kama serikali hiyo itakuwa serikali makini yenye kuwajali wananchi inaowaongoza. Ninaamini serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni serikali makini yenye malengo na madhumuni ya kutaka kuwasaidia wananchi wake kwa kuwalinda kuhakikisha bidhaa na huduma wanazozipata ziko salama na ziko endelevu.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine lililozungumziwa ni suala la *diversion* kwa maana ya kubadilisha maumbile ya chombo, limezungumziwa suala la jenereta Mjumbe alitaka kujua kwa sababu gani jenereta likawa ni miongoni mwa mambo yaliyoainishwa katika vile vipengele ambavyo vinaashiria vifaa ambavyo vitakuwa vimebadilisha maumbile ya chombo husika. Dhamira ya hapa ni kuonesha tu kwamba inawezekana meli ina jenereta zake ina uwezo wa kutengeneza umeme pengine megawatt 5 ukibadilisha jenereta likutane na jenereta linalozalisha megawatt 2 chombo hiki kitakuwa kimepoteza sifa yake na tutakizuia hatutokipa usajili.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lililozungumziwa ni ubadilishaji wa maneno neno *may* na neno *shall* haya tumeyapokea kwa maeneo maalum. Katika yale maeneo maalum tunatakiwa kufanya *regulation* kwa ajili ya usimamizi maalum neno *shall* bila shaka litatumika. Lakini katika yale maeneo ambayo yataendelea kuwa ya ujumlajumla tunaomba neno *may* liendelee kutumika.
Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache pamoja na ufafanuzi huo mdogo nilioutoa naomba nirejee tena kusema kama ninaunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza niamshukuru *Allah* kutupa uhai uzima na taufiki ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu na kupata nafasi ya kutoa mchango wa wizara na serikali kwa jumla kuhusiana na hoja mbali mbali za Wajumbe wa Baraza hili.

Kwanza napenda niwataje wale ambao wamechangia katika Mswada wetu wa Marekebisho ya Sheria wa Mamlaka ya Usafiri Baharini kama ifuatavyo:-

Tukianza na Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa niaba ya Mwenyekiti

1. Mhe. Hassan Hamad Omar
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma

4. Mhe. Saleh Nassor Juma
5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
8. Mhe. Hamza Hassan Juma
9. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
10. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais
11. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
12. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
13. Mhe. Asha Bakari Makame
14. Mhe. Marina Joel Thomas
15. Mhe. Salma Mussa Bilal
16. Mhe. Subeit Khamis Faki
17. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
18. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
19. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Kwanza napenda nichukue fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa wajumbe hawa na wale ambao wamebaki kwa kutoa michango yao ya kina na kuweza kuuchangia mswada huu ili kuweza kufikia mustakabali mzuri.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na vile vifungu 29 vilivyotajwa katika Gazeti Rasmi la Serikali naomba pia kuwasilisha vifungu vyengine vitatu ambavyo viliridhiwa na kamati yako ya Mawasiliano na Ujenzi ili kutilia mkazo juu ya udhibiti wa usafiri wa baharini viende pamoja na mswada wa mwanzo.

Vifungu vyenyewe vinaonekana katika mswada uliogaiwa sasa hivi kifungu cha marekebisho nambari 11 kinachorekebisha kifungu nambari 12, kifungu cha marekebisho nambari 31 kinarekebisha kifungu cha 122 na kifungu nambari 20 kinachorekebisha kifungu cha 57 cha sheria mama.
Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye hoja za Wajumbe. Mhe. Naibu Spika, hoja ambayo ilichangiwa sana na wajumbe wengi ni marekebisho yaliyofanywa katika kifungu nambari 17a. Kifungu hiki kiliweka umri wa kusajiliwa meli naomba nikinukuu halafu nitoe maelezo yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki kinasema, “Hakuna meli ambayo itazidi umri wa miaka 15 tokea tarehe ya kutumika kwake itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa ajili ya kuchukua abiria na mizigo Zanzibar”. Kwanza naomba niseme kwamba wajumbe wengi ambao walikuwa wakichangia walikuwa wakiondoka katika ile maudhui yenyewe. Kwa hivyo, napenda nitoe ufafanuzi ufuatao ili ifahamike vizuri zaidi ni nini kilichokusudiwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, la mwanzo ni kwamba meli hizi zinazokusudiwa kupewa *category* hii ni zile ambazo zitakuja sasa hapa Zanzibar, sio zile ambazo tayari zimeshaingia. Kwa hivyo, zile meli ambazo zimeshaingia zinaendelea kufanya kazi yake zile zitafanyiwa utaratibu kama ambavyo sheria inavyosema ya ukaguzi na kuendelea kuzipa leseni kadiri itakavyoweza kukidhi mahitaji

ya usalama na ubora wa chombo chenyewe. Lakini meli yoyote itakayoingia kuanzia sasa ndio itabidi ifuate mkondo huu.

La pili, wengi walikuwa wakizungumza kuhusiana na labda wafanyabiashara wengine watatengwa. Hili Mhe. Naibu Spika, sio la kweli, kwa sababu sisi katika uchunguzi wetu wa kina tumeona kwamba chombo ambacho ni kikongwe kina gharama zaidi kukiendesha kuliko chombo ambacho kina umri mdogo. Hivi sasa mimi ni shahidi kwamba Meli ya Maendeleo ambayo imo katika shirika letu inatubebesha mzigo mzito sana wa kuendesha, kwa sababu *maintenance cost* ni kubwa kuliko hata ile *import* ile inayotia. Kwa hivyo, ili kuwaokoa hata hawa wafanyabiashara wasiweze kupata *maintenance cost* kubwa basi ni afadhali kuwawekea hii kwa huruma zao.

Lakini la tatu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba vyombo hivi vinatarajiwa viende *dry-dock* kila baada ya miezi 18 vinavyochukua abiria. Tumeona hapa vyombo vyetu vingi vinakaa hapo hapo bandarini na kufanyiwa matengenezo bila ya kwenda *dry-dock* kwa sababu vyombo vyenyewe ni chakavu, fedha ni nyingi zinazohitajika kupeleka *dry-dock* na hawana uwezo huo. Sasa ili kuwapunguzia gharama zote hizo serikali imeona kuwa tuwaokoe tokea mwanzo wachukue chombo kizuri. Lakini wale walioiuliza ni kitu gani kilichokusudiwa hasa miaka 15 ni tokea ile meli ilipomaliza kuundwa na itaanza kufanya kazi huko. Kwa hivyo, ule umri wa meli ulivyokuwa unaifanyia kazi ndani ya bahari.

Jengine Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa ufafanuzi wale ambao walikuwa wakiipigia debe ile meli iliyoko katika Ziwa Nyasa Waheshimiwa wawili bahati hapa wameshapanda ile meli na wameizungumza vizuri, mmoja nampongeza sana Naibu Waziri wa Afya jinsi alivyoeleza. Meli yenyewe imeshazama mara tatu halafu inazamuliwa inakuja inachukua tena abiria. Sasa tujiulize hizi zetu sisi ziko wapi? Mbili zimezama zimepatikana wapi? Sasa safari za kwenye ziwa na safari za baharini ni vitu viwili tofauti. Pia tuna safari za maji chumvi ambapo maji chumvi yenyewe yanakula chum asana kuliko maji ya baridi. Sasa tumeangalia mantiki yote hiyo.

Lakini jambo jengine Mhe. Naibu Spika, zilipotokea ajali mbili hizi sisi Waheshimiwa Wajumbe nikiwemo mmoja mimi mwenyewe binafsi tulikuwa tunapiga kelele sana kuhusu kuimarisha usalama wa vyombo vya baharini. Sasa inaonekana kwamba moja katika kuimarisha huu usalama wa baharini ni kuiwekea huu umri kwa sababu ya uzoefu uliopatikana.

Angalia MV. Skagit ambazo mwanzo zilipokuja hapa zilikuwa zinaitwa Kalama zilikwenda kununuliwa ndani ya umri wa miaka 23, sasa mtu anakwenda kununua chombo tayari kwa dola laki nne sasa dola laki nne wewe unakwenda kununua chombo ili kije kibebe abiria katika nchi hii. Kwa hivyo sasa, haya mambo ndio yaliyopelekea tukaona kwamba lazima sasa tuweke utaratibu ili watakaoingia katika biashara hii waweze kuwa waaminifu, waweze kuleta yale maslahi ya wananchi na usalama wao.

Mhe. Naibu Spika, hakuna mwananchi ambaye anasafiri baina ya Unguja na Pemba akawa hataki usalama wake, au baina ya Unguja na Dar es Salaam, lakini kwa sababu kuna bahari katikati huwa hana budi kupanda lolote litakalokuwepo. Sasa ni juu ya serikali pamoja na Wawakilishi nawaomba sana kuangalia kwamba je, watu wetu hatutaki tena waendelee katika

hali ya usalama? Ni lazima ajali zile mbili kubwa zitupe mafunzo maalum ili tuweze kuimarisha usalama wa watu wetu katika siku za baadae.

Kwa hivyo, kwa kumalizia na suala hili nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane kuiweka hii miaka 15 iwe ndio kigezo cha kuingiza meli mpya inayokuja, sio zile ambazo zipo nchini. Kwa sababu usajili unatolewa mara moja tu kikiingia chombo, leseni ndio inayotolewa kila baada ya muda, lakini hii haisemi leseni kifungu hiki kinasema kusajiliwa haitosajiliwa. Kwa hivyo, ni ile meli inayokuja mpya na uzoefu wa wafanyabiashara wetu tumeona tokea tulipoanzisha wanakwenda kuchukua vyombo ambavyo haviko katika *standard*, haikufanya maamuzi hayo kwa sababu ya upendeleo fulani.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie hapo ili niwaachie Wajumbe waangalie na wapime ndani ya nyoyo zao ni nini hasa mustakabali wetu. Hatuwezi tena Zanzibar kuweza kuwamaliza watu wetu ndani ya bahari. Mimi jambo hili linaniuma sana kwa sababu mimi nimeshuhudia mambo mengine ambayo nyinyi pengine pia mmeshuhudia. Wale waliokufa kwenye ajali zile meli mbili kuna watu wengine wanaendelea kufa kwa vihoro hawakuweza kumeza tena, mtu ana mkewe na watoto wake watatu, ana ndugu zake watano hawakuweza kumeza wengine hawakuchanganya tena unawaona baada ya muda mdogo na wao wanakwenda. Sasa hili ni jambo la kuzingatia sana, wizara haikukaa kabisa kabisa katika nafasi yoyote ile kutizama maslahi labda ya mtu mmoja au wawili au kumpendelea mmoja au wawili, imetizama maslahi ya watu wetu na usalama wao ndani ya usafiri.

Kwa hivyo, naomba sana tukubaliane katika hili jambo, nimechukua muda kulizungumza kwa sababu ya uzito wake hatujui sisi chombo gani kimeundwa wapi wala wapi hiyo sio kazi ya wizara atakakokwenda angalia basi serikali ilivyokuwa imeamua. Serikali pamoja na kwamba bado tunasema hivi hivi lakini imeamua kuchukua mtoto mchanga mwaka *zero* inaanza kutengenezwa ndio italetwa hapa tukijaaliwa. Sasa kwa wananchi na wafanyabiashara tunawapa *span* ya miaka 15, serikali inachukua *zero* inaunda mpya lakini wananchi tumewapa miaka 15 kwa hizo sababu zenu tunazikubali kwamba wako watu wetu hawana uwezo wa kununua mpya na ndio maana ikawekwa miaka 15 tokea ilivyoundwa meli ile inafanya kazi.

Baada ya hayo naomba Mhe. Naibu Spika, niendelee na kipengele chengine ambacho kilizungumzwa sana na Wajumbe wengi kipengele nambari 18a. Hiki kilizungumza kuhusu, waziri anaweza kutunga kanuni zitakazoeleza ukomo wa umri. Hapa tunakubaliana na Wajumbe waliochangia na tunakubaliana kukibadilisha kwamba sasa isomeke, waziri atatunga kanuni badala ya waziri anaweza kutunga kanuni.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo lilitiliwa mkazo sana na kutengenezwa na wajumbe ni hili la kifungu cha 10a. “Hakuna mtu au taasisi atakayeingia katika shughuli zozote zinazohusiana na usafiri wa baharini bila ya leseni au kibali kinachotolewa katika namna itakavyoelezwa na mamlaka”. Kwanza nawashukuru wote ambao wamekiunga mkono hiki kifungu, lakini wale waliotahadharisha kwamba pasipite rushwa katika hapa pia nawapongeza. Mimi katika kipindi changu hiki chini ya ZMA nahakikisha kwamba leseni haitotolewa kwa rushwa kwa njia yoyote ile, atakayekuwa ametimiza masharti ndiye atakayepewa leseni na chombo chochote kikionekana kwamba hakiendi kwa utaratibu au hakifuati masharti basi leseni haitatolewa.

Mhe. Naibu Spika, hayo ndio mambo makubwa ambayo yamezungumzwa na wajumbe wengi. Sasa naomba niingie kwa mchangiaji mmoja mmoja kwanza nianze na Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mwakilishi wa Jimbo la Chonga.

Kwanza tunampongeza sana kwa michango yake kwa kutaja kwamba mswada huu umekuja katika wakati muwafaka. Pili napenda nieleze kwamba sisi katika wizara hii pamoja na ZMA tunaloshughulikia ni viwango na kwa hivyo kutokana na mchango wake sisi tumechukua na tunaiagiza ZMA ifanye uchunguzi wa kina kuhusu Meli ya Serengeti na hali yake ambayo ilitajwa.

Mheshimiwa alitaka kwamba kuna wasi wasi kuwa Meli ya Serengeti inazibwa kwa saruji. Kwa hivyo, sisi tunaiagiza ZMA kupitia wakaguzi wetu ifanye uchunguzi wa kina na ukaguzi ili kubaini hali hiyo.

Halafu mchango wake mwengine ulikuwa vile vile ni kuhusu meli ambazo hazina mkuku na meli ambazo zina lango la kufunga na kufunguka. Meli hizi Mhe. Naibu Spika, bila ya kuchanganya ziko aina mbili, kuna meli ambazo tokea mwanzo zinatengenezwa kwa ajili ya kuchukua abiria na hizi zinapewa jina roro chipsi (*roll on, roll of*). Hizi zinaruhusiwa kuchukua abiria kwa sababu muundo wake na usalama wake tokea mwanzo zimetengenezwa kwa kuchukua abiria. Lakini kuna meli nyengine ambazo zinaitwa *land crafts* ambazo huwa hazina mkuku zinaweza kukaa mpaka kwenye mchanga na zile ambazo hazikutengenezwa kuchukua abiria utaziona muundo wake, kuna *cabin* nyuma halafu sehemu kubwa iko wazi haina chochote.

Sasa wafanyabiashara wetu huchukua ile *cabin* wakaiongezea juu wakachukua abiria, sasa jambo hili ndilo lililokatazwa vile vile. Kwa hivyo, sheria inakataza kuchukua *land craft* ambazo zimetengenezwa kwa kuchukua mizigo ukapachika *cabin* ili uchukue abiria hili sheria imelikataza. Hivyo tunasema wazi hapendelewi mtu yeyote wawekezaji sasa watakuwa na nafasi ya kuangalia ni wapi wataleta uwekezaji wao, wanataka meli ya mizigo, wanataka meli ya abiria, tumeshachoka tena abiria wetu kulazwa juu ya nondo. Kwa hivyo, tunaomba sana wawekezaji waweze kuchagua kama mtu anataka kuchukua abiria na mizigo basi atenge pahala pa mizigo maalum kwa kuweka mizigo na abiria wawe na viti vyao vya kukaa, lakini watu kwenda kuwekwa juu ya nondo hali inavyokwenda vile basi tena, huu ndio msimamo wa usafiri baharini sasa hivi.

Mimi nilisema katika maelezo yangu ya mwanzo Mhe. Naibu Spika, tunataka *safety and comfortability***,** abiria asafiri awe hajulikani kwamba katoka safari. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hatukukusudia kukomoa mfanyabiashara yoyote wala mwekezaji yoyote, tunakusudia kubagua baina ya chombo cha kuchukua abiria na chombo ambacho kitachukua mizigo na chombo ambacho kitachukua abiria na mizigo kilichotengenezwa makusudi kwa ajili hiyo.

Mhe. Mgeni Hassan Juma tunamshukuru kwa michango yake na tunapokea pongezi alizotupa na sisi vile vile tuko katika huzuni mpaka hivi leo juu ya kusikitikia matokeo yaliyotokea. Ndio maana tukawa tunasisitiza msimamo wetu wa kuwa na utaratibu mzuri wa usafiri kwa usalama.

Kama alivyosema Mhe. Mgeni ni kweli kwamba sisi hapa vyombo vyetu vinasafirisha abiria wa ndani na wa nje. Mimi mwenyewe binafsi nimeshashuhudia vikao vingi tunavyofanya hapa sasa hivi na wageni mpaka kupenda namna gani sisi vyombo vyetu vinavyotoa matangazo ya kiusalama, abiria anapoingia tu anatangaziwa. Hivi sasa hivi vyombo vya baharini vinatumiwa na watu ambao wana ngazi mpaka ya Ubalozi na wewe huwezi kuwajua mle, wana ngazi kubwa kubwa. Sasa hatuwezi tena kwamba sisi tuwe *branded* kwamba ni watu ambao hatuna mpango lazima vyombo vyetu viende kiutaratibu.

Kwa hivyo, vile vile katika kuimarisha biashara ya utalii tumeona katika matokeo yote, hata juzi hayo ya *MV Skagit* watalii walikuwemo sasa ile ni pigo kwa biashara ya utalii ambayo inaingiza mapato ya nchi. Kwa hivyo, ili kudhibiti hayo tunaendelea kudhibiti usafiri na hivyo tunakushukuru Mhe. Mgeni. Isipokuwa suala lako hili limeshazungumzwa kama mtu amefanya kosa na amepewa faini lakini hakulipa basi kiko kifungu katika sheria mama 464(3) kinachozungumza kwamba, mtu yule atathibitishiwa na adhabu ya kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miaka mitatu.

Mheshimiwa pia aliuliza kuhusu meli kukamatwa ikiwa imegonga mwamba imekwama au imezama. Meli ile ikiwa inadaiwa itauzwa kama ni *scrapes*, kwa hivyo bado itakuwa na thamani ya kuuzwa.

La mwisho alizungumza usimamizi wa sheria nadhani katika matokeo mawili yale ya ajali ya *Spice Islanders* na *Skagit* serikali iliunda tume ambayo ile ile ilifanya kazi ya kwanza na ya pili na mapendekezo yake mengi yapo na ndio tunayafanyia kazi katika kuhakikisha kwamba sheria zinasimamiwa. Hivi sasa tumefikia kiwango hata cha kuzizuia meli zisiende kwa sababu ya hali ya hewa. Kwa hivyo, usimamizi tunaufanya katika ngazi ya juu kidogo. Hali ya hewa ikichafuka tunawasiliana na vituo vya utabiri wa hali ya hewa na tukiona kwamba hairuhusiwi vyombo vile vinazuwiwa kwa masaa mpaka hali ya hewa itakapotulia ndio vinaruhusiwa kwenda. Kwa hivyo, hiyo ndio *stage* ambayo tumefikia.

Mhe. Saleh Nassor Juma tunashukuru kwa michango yako ni kweli kwamba watu wengi kwa sababu sisi ni visiwa tunategemea usafiri wa baharini. Usafiri wa baharini kama tulivyosema hauna *alternative*, kwa sababu chombo kinachokwenda ndio hicho kwa hivyo usalama wake ndio tunaojitahidi hivi kuuchunga.

Suala la *ID* ni kweli katika udhibiti wa uuzaji wa *ticket* tumeweka utaratibu huu kwamba watu wende na vitambulisho vyao ili iwe ni rahisi. Kwa hivyo, hapa kwa niaba ya serikali mimi nitalichukua hili nilipeleke hasa kwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi watu ambao hawajapata vitambulisho waweze kuwapatia ili na wao waweze kupata *comfort* ile tunayosema katika usafiri. Kwa sababu anapokwenda ikiwa hana kitambulisho akazuwiwa ni sehemu moja ya kukosa haki yake. Kwa hivyo, hili tunalichukua na *Inshaallah* serikali ipo imetusikia na tutakwenda nalo.

Mhe. Naibu Spika, aliendelea kuchangia kuhusu chombo kufanyiwa *service*. Hili nimeshalizungumza sasa hivi hapa, kuna *regular service* ambazo zinafanywa na kuna muda ule wa miezi 18 ikifika chombo kile kiende *dry-dock*, ndio nikasema kwamba vombo vyetu baadhi yake huwa havyendi kwa sababu ya ukosefu wa mtaji na ndio maana ikawa ni muhimu sasa hivi

kubadilisha hizi sheria ili kuwafanya wale wawekezaji wawe *serious* katika hii *business.* Kwa hivyo tunawataka waweze ku-*comply* na mambo yote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub namshukuru sana kwa michango yake kama ambavyo tulielezwa kwamba *signal tower* ni muhimu isipokuwa ni chombo ambacho kinaendeshwa na Shirika la Bandari na tunakuhakikishia kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tumo katika mashughuliko makubwa na *vision* yetu hasa ni kuwa na *signal tower* yetu wenyewe kama ambavyo ipo Dar es Salaam pale.

Kwa hivyo, nakushukuru sana kwa michango yako. Kwanza niseme jambo moja, hii sheria ambayo tunaisoma leo ni sheria ya usafiri baharini ya mwaka 2006. Hii mamlaka tunayoita ZMA sheria yake ilipitishwa mwaka 2009 na yenyewe ikaundwa mwaka 2011. Kwa hivyo hii ZMA ni chombo kichanga sana kina umri kama wa miaka miwili tu sasa hivi. Hivyo hii sheria tunapoisoma inawachanganya watu wengine kuona kwamba labda ni chombo cha zamani. Sheria ilifanywa ya usafiri baharini halafu mwaka 2009 ikapitishwa sheria ya mamlaka ya usafiri baharini lakini chombo chenyewe kilianza kufanya kazi mwaka 2011.

Sasa kwa njia hiyo yote mambo mawili, kwanza utendaji wake wa kazi lakini la pili kanuni ambazo zilitakiwa zitungwe usifikirie kwamba zimechelewa sana, lakini la tatu ni kwamba kanuni za ZMA zimeambatana na sheria za kimataifa zinazoitwa *International Meritime Organization.* Kwa hivyo, ni vitu ambavyo lazima uvi-*magic* yale mambo yetu wenyewe na zile sheria za kimataifa au kanuni zinazotokana na *International Meritime Organization*.

Lakini pamoja na hayo sikatai kwamba zimechelewa, kwa hivyo kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na kwa niaba ya ZMA nakuhakikishia Mhe. Jaku pamoja na Wajumbe wote waliochangia kuhusu kuchelewa kwa kanuni kwamba tutahakikisha kuwa ndani ya muda mfupi ujao kanuni tutazitengeneza ili ziweze kutumika, sidhani kama utavuuka mwaka huu kama kanuni hizo zitakuwa hazitumiki na hiyo ni kwa urefu sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub uliuliza kuhusu suala la *Filtex* Hii ni kampuni ambayo imetiliana mkataba na serikali kuhusiana na daftari la kusajili meli za kigeni ambalo makao makuu yake yapo Dubai. Fedha zake zinakuwa kwenye mfuko wa serikali moja kwa moja, hazipitii ZMA zinaingia katika mfuko mkuu wa serikali. Kwa hivyo hata hesabu yake ipo Wizara ya Fedha.

Mgao baina ya kampuni na serikali ni asilimia 65 kwa serikali na 35 kwa kampuni. Hili ndio swali lako la mwisho.

Swali lako la mwisho kabisa lilikuwa nini hatma ya wawekezaji wadogo wadogo katika usafiri baharini. Mimi nasema kwamba nchi inaendelea, hata dunia ukitizama ilikuwa hapa Tanzania bajeti ya miaka ya nyuma ilikuwa ikizungumzwa *billion*, sasa inazungumzwa *trillion*, ina maana nchi inakua.

Sasa sisi wawekezaji wetu wadogo wadogo hatuwezi kubaki *stagnant* ni lazima wakue. Kwa hivyo hao tunaowaita wadogo wadogo tunataka wanyanyuke. Sisi Zanzibar hapa tulikuwa tukitumia milioni bajeti za nyuma, miaka kumi iliyopita, sasa tunatumia bilioni. Bajeti yetu ya

mwaka huu ilikuwa bilioni mia sita na kama arobaini. Kwa hivyo hawa wawekezaji wadogo wadogo sisi tunawahitaji nao wawepo, lakini nao wakue ili waweze kukua.

Mhe. Mohamed Aboud leo asubuhi alipokuwa anazungumza alitoa ushauri mzuri kwamba wajikusanye pamoja. Kwa hivyo wale wafanyabiashara wadogo wadogo katika sekta hii ya usafiri ambao wanahisi hawana mitaji mikubwa wajikusanye pamoja ili kupata mtaji ambao ni mzuri wa kuendesha biashara zao katika hali ya ushindani.

Madhali tumekubali kiujumla kufanya hali ya ushindani inabidi ni lazima tuende vile vile, hatuwezi kupiga breki halafu tukasema aah! Wengine hawawezi kwenda *speed* hii, ni lazima tuende vile vile.

Mhe. Hija Hassan Hija nashukuru sana kwa michango yako. Mimi sidhani kama hoja ya majanga ni dhaifu, kwa sababu hakuna *cost* ya maisha ya mtu. Isipokuwa lishatokea. Kwa hivyo sisi mabadiliko ya sheria hii kuyajengea katika majanga yaliyotutokezea ilikuwa ni haki kwamba sisi tumeona lakini ni haki kwamba mapendekezo mengi haya yanatokana na Tume iliyoundwa kwa ajili ya kuchunguza chanzo na mambo yanayotokana na ajali hiyo.

Kwa hivyo watu ambao tumepoteza ni wengi mno na pengine si rahisi kujua idadi yake kama ambavyo ilivyokuwa. Hivyo sisi kujenga hoja hii ni sahihi kabisa.

Jambo ambalo ulilichangia na mimi nakubaliana nalo ni kwamba tuwe na umakini katika kuangalia usalama wa vyombo baharini. Hata mimi nitalisimamia jambo hili na napenda niwaaambie watendaji wote kwamba hatutomvumilia mtendani yeyote ambaye hatokuwa na umakini katika kusimamia usalama wa baharini akenda akatafuta maslahi yake mwenyewe. Hilo hatutovumilia. Mimi nitakuwa wa mwanzo kumtolea karata mbele ya serikali. Kwa hivyo hilo ni jengine.

Yapo mambo yamebainika ni sahihi kwamba hakukuwa na umakini na ndio maana hapa liliulizwa swali kuhusu wafanyakazi wangapi wakaguzi. Wapo ambao walisimamishwa kazi na hivi sasa kesi yao ipo Mahakamani, kwa sababu na huu umakini wa kuona kwamba linafuatiliwa. Kwa hivyo wale ambao walibainika kwa njia moja au nyengine walihusika katika habari ile ndio wakasimamishwa kazi na wakapelekwa katika vyombo vya kisheria. Kwa hivyo umakini upo.

Ulizunguma kuhusu sheria za kukopia. Labda Mwanasheria Mkuu yupo hapa lakini nasikia sisi tunatumia sheria za Uingereza tokea mwaka gani sijui. Kwa hivyo mimi naambiwa na wanasheria wenyewe kwamba sio vibaya kukopia sheria, lakini wewe unayekopia usiwe unakopia ukawa hujui, yaani *blind copy*, uwe unajua kwamba hii ina-*effect* hivi na vile.

Kwa nini nchi zetu zinaingia katika mashirikiano kwa sababu yale mambo yao yanakwenda kwa pamoja, movement za watu ni nchi na nchi au sehemu na sehemu na sisi ndio tunaoshughulikia. Usafiri baharini unashughulikia na *movement* za watu. Kwa hivyo madhali inashughulikia nyendo za watu, watu watakwenda kila pahala. Sasa ili kuweza kuoana na utaratibu huo ni lazima mambo mengine tuchukue yale ambayo wanayo wenzetu na tunayaona kwamba yanafaida kwetu sisi tuyachukue, yale yaliyokuwa hayana tutawaachia wenyewe.

Mhe. Hija nakuhakikishia kwamba katika mamlaka hii wataalamu wetu wanatumika lakini tuna ukosefu kweli kweli wa wataalamu wa aina hii. Ikiwa utawashawishi vijana wanaomaliza *form six* na wapi waende wakasomee hii fani basi watapata ajira ya mara moja.

Wakaguzi ambao wanaoitwa *surveyors* hatuna. Kwa hivyo hii ni fani ambao inayohitajika sana na wale pengine waliopo wanaona kuna maslahi zaidi kwengine. Kwa hivyo sisi hatumuweki mtaalamu wetu ikawa hatukumtumia.
Ndio hilo suala lako la surveyors kama nilivyokwambia na sio kwamba hawatumiki, hapana hawa wa kuwaajiri. Ndio maana hivi sasa baada ya mtikisiko huu ZMA inaingia mkataba na kampuni ambayo kampuni hiyo hiyo itaingia mkataba na SUMATRA ili nini, kwamba huyu mkaguzi atakayekaa hapa Tanzania, sisi tutakuwa na *access* naye kwa kumtumia kwa pesa zetu na kwa kazi zetu na kule watakuwa wanamtumia. Kwa hivyo itakuwa ni *cost affective* hiyo.

Tofauti karibu hapa ilikuwa anachukuliwa mkaguzi kutoka Dar es Salaama anafikiri ni wa SUMATRA; yule si wa SUMATRA. Ile ni kampuni ambayo iliajiwa na SUMATRA, sisi tunafanya mazungumzo nayo. Lakini hivi sasa tunaingia katika mkataba hasa na ile kampuni ambayo sisi tutamtumia na wao watamtumia kila mmoja kwa wakati wake.

Kuhusiana na magendo ya tiketi. Sisi tulifanya utafiti. Moja katika tuliyogundua mbali ya matatizo ya vyombo vyenyewe vilikuwa havitoshi kwa muda huo, lakini kuna baadhi ya wamiliki wa meli hawajaingia katika ile *electronic tickets*. Kwa hivyo ili kuweza kuweka mtandao wa pamoja wameshapewa agizo la ZMA waweke mtandao wa kompyuta ili waweze kutoa *electronic ticket*. Sasa hapo tukishakuwa mashirika yote yana *electronic tickets*, sisi tutafanya *system* za kuweza kumjua nani anayeuza tiketi za magendo na nani hauzi, kwa sababu zipo njia hizo. Ikishakuwa ule mtandao upo utajua kwa sababu hawezi ku-*cheat* lakini mpaka hivi sasa kuna wauzaji wengine wa tiketi wanauza tiketi zilizoandikwa kwa mkono, kwa hivyo zile huwezi kuzifuatilia kwa kina.

Kwa hivyo nakuhakikishia kwamba hili suala tunakwenda nalo. Mimi nasema uondoe wasi wasi hapa wizarani hapana kitu, hapana kitu chochote kilichofichika, kipo kitu kipo sawa. Kwa sababu wewe uliuliza kuna nini huko wizarani? Hakuna kitu, zaidi ya sisi tunataka usalama wa wasafiri wetu. Hilo lipo kweli lakini jengine hakuna.

Mhe. Mahmoud suala lako na ninakushukuru kwa mchango wako, lakini nililijibu pale kwamba ni kuanzia pale ilipoanza kufanya kazi ile meli na kuendelea, ndio huo umri wa ile meli ilipomalizwa kutengenezwa.
Tunamshukuru Mhe. Waziri Mohamed Aboud kwa *intervention* yake na kutoa nasaha zake.

Mhe. Hamza Hassan Juma tunakushukuru sana kwa michango yako. Pongezi zako tumezipokea. Vile vile tunakushukuru kwa kutushtua sheria inatakia kufuatiliwa na kusimamiwa utekelezaji wake. Ni kweli kuwa na mbiu ya sheria hakumaanishi kwamba ile shughuli inafanyika, sheria ni lazima isimamiwe, ni sahihi. Sitokuwa mkali lakini nitakuwa *serious* katika kusimamia sheria.

Sasa hii ya mwaka, si tulisoma huu mswada kwa mara ya mwanzo 2012. Kwa hivyo huu mswada umeshakuwa table tokea 2012, mpaka iwe *otherwise* lakini 2012, hapa unasomwa kwa mara ya pili.

Kuhusu Mamlaka ya Usafiri Baharini tumeshasema kwamba tumebadilisha lile na tumeeka mamlaka yoyote ya usafirini baharini iliopo kwa sababu lile ni jina ambalo kwanza linashughulikia taasisi mbili ya usafiri wa nchi kavu na sisi tuna-*deal* usafiri baharini tu, na hata kikiondoka hiyo taasisi hiyo tutakwenda na ushirikiano na hiyo taasisi iliopo kwa wakati huo hata zikiwa mbili. Sisi tutakwenda na ushirikiano na zile taasisi ziliopo kwa mujibu wa usafiri baharini.

Lile suala la shilingi limetajwa katika sheria lilikosewa katika pale tu, lakini katika sheria limetaja kwamba dola elfu tano zitakazolipwa katika shilingi za Tanzania. Kipengele nambari (a) nafikiri tumekizungumza sana, 17 (a) nimekizungumza sana nafikiri, kwa hivyo nimeshakujibu. Kama ulivyosema usimamizi.

Kuhusu kipengele cha mashine za umeme, nilisema pale ni zile ambazo sio za asili yake kwa sababu kuna wengine mashine ya umeme ipo chini kule kwenye chumba ambacho kinachoitwa *engine room*. Atakujakuchukua jenereta aweke juu kwenye watu, watu wanapita hapo hapo, jenereta hapo hapo, moshi moshi hapo, sasa ile *modification* ile haitakiwi, anatakiwa a-*replace* aondoke ile aweke nyengine pahali pale pale. Sio kwamba afanya *modification* jenereta aweke huko anakotaka yeye kwa sababu ya ule muundo wa jenereta. Kwa sababu zile jenereta za melini zina muundo wake na mwahali mwake.

Sasa kama kamalizikiwa ile jenereta imemaliza muda wake, anunue nyengine lakini itakayokuwa na muundo wa kwenda kupachikwa mule mule, lakini akiamua kuweka juu huko kwenye watu, moshi huko huko, hiyo itakuwa ndio kafanya mabadiliko. Crane ilikuwepo ndogo kaona sasa mizigo mikubwa kapachika kubwa ili apate faida zaidi, meli inazama chini. Sasa ndio hayo *crane* ya tani tano a-*replace* ile ile ya tani tano asitie ya tani kumi, ndio ilivyokusudiwa hapa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu tunakushukuru kwa michango yako mingi na tunapokea pongezi zako. Tunakuhakikishia kwamba marekebisho haya yamefanyika baada ya majanga yale na zile tume mbili ambazo zimeundwa pamoja na kuangalia ni wapi ambapo tumejikwaa.
Kuhusu SUMATRA kama tulivyosema kama tumeiondoa, tunaweka Mamlaka ya Usafiri Baharini. Kama ulivyosema ni sahihi kwamba ajali zote mbili ilianzia Dar es Salaam lakini hilo ndilo lililotufanya tukasema kwamba tupate ushirikiano, kwa sababu safari zetu za baharini zinakwenda Unguja, Pemba, Tanga au Unguja, Dar es Salaam pengine na Mtwara.

Sasa lazima kwa sababu *code* tunazozi-*code* ni ndani na zina ushirikiano ni lazima tuweze kuwa na ushirikiano na kile chombo katika *port* hizo ili kuondoa migongano.

ZMA kama mulivyoambiwa ina *volume* ya vifungu mia nne na sabini. Kwa hivyo si rahisi kwamba ZMA itafutika kwa marekebisho haya. ZMA ipo na lakini kitu kipo.

Suala kama tulivyolijibu mwanzo kama tumekubali kwamba waziri atatunga sheria, sio anaweza. Tumekubali na tumeshai-*cooperate*. Vifungu vile ulivyoviuliza nimesoma hapa katika mada yangu nilipoihudhurisha, uliuliza kuhusu ziada ya vile vifungu ambavyo havikutokeza lakini mswada ulioletwa sasa hivi umeshatiwa.

Kanuni nimeshasema kwamba ZMA ndogo lakini sasa tutaisimamia kwa sababu imeshakuwa na nini. Open Registry nimeshalieleza na *Filtex* nimeshaeleza kwamba fedha zake zinakwenda katika mfuko mkuu wa serikali.

Sisi tunasimamia sehemu ya uokozi kwa wenye boti wenyewe. Kwa hivyo tumeona kwamba kwanza kunakuwepo yale maboya ya kujiokolea maisha. Hilo ndio la mwanzo ndani ya boti. Lakini wengi huwa hawawafundishi abiria wala hawawaoneshi isipokuwa labda hizi boti zinazokwenda kwa kasi.

Lakini sisi tutasimamia hata hizo meli ambazo haziendi kwa kasi ambazo abiria wake wanakaa sehemu mbali mbali ziweze kuwepo karibu na kuweza kufamishwa wale abiria. Kuna wenzetu ni kweli kuwa wanafanya mpaka mazoezi maalum ya vile kuvaa yote, hata kama hakuingia mule baharini lakini kila mmoja anapewa katika ile safari avae. Kwa hivyo sisi tutasimamia hilo uokozi ndani ya ile boti yenyewe.
Sasa uokozi kwa jumla wa nchi kama ulivyoelezwa na Waheshimiwa Mawaziri wawili na sisi tutahakikisha kwamba hayo mambo yanatokezea, kwa sababu inapotokezea ajali ya boti au meli ni sisi ambao tunahusika zaidi katika vile vyombo.

Mimi nakubaliana na usemi wako uliousema na mimi nimeuchukua na hivyo nimo katika ku-*transform* watu wangu, kwamba vipi *what we need is not new laws or new institution but good people with good intention.* Kwa hivyo mimi nakuhakikishia kwamba nimeuchukua na nitaufanyia kazi kwamba tunawa-*transform* watu wetu kuangalia maslahi ya wananchi zaidi, maslahi ya nchi zaidi na kutoangalia maslahi ya binafsi.

Mhe. Naibu Spika, wengine ambao wamechangia kwa jioni baadae ni Mhe. Makame Mshimba. Yeye masuala yako yote tumeshayajibu isipokuwa tunakubali kuwa tuna wataalamu wachache na ndio kama nilivyosema tunatafuta wataalamu.

Chuo cha Mabaharia hakipo hapa lakini meli imeshafika hivi sasa tungojea kama mambo yake yatakuwa mazuri karibuni hivi tutapata Chuo cha Mabaharia. Wengine tumeshawakaribisha ili waje kuanzisha chuo cha mabaharia. Kwa hivyo si muda mrefu inshaalla Zanzibar itakuwa tunaanza na vyuo vya mabaharia ili tuweze kuwa na *sponsor* wa kimataifa.

Mhe. Asha Bakari Makame tunashukuru kwa mchango, tunakuhakikishia kwamba leseni zinazotolewa na vyombo zitatengwa mbali na rushwa, na yeyote tutakayem-baini kwamba kacheza mchezo mchafu basi tutapambana naye tukijaaliwa. Tunakushukuru kwa kutuunga mkono katika umri wa chombo miaka kumi na tano.

Mhe. Marina Joe Thomas tunakushukuru kwa mchango wako na kutuunga mkono na nakuhakikishia kwamba kanuni waziri atatunga sio mbali. Mamlaka imetajwa kwamba neno lolote litakalokuwa linatajwa katika sheria mamlaka; maana yake ni mamlaka ya usafiri baharini Zanzibar (ZMA). Kwa hivyo hili limetajwa katika tafsiri na lipo.

Mhe. Salma Bilali tunakushukuru kwa mchango wako na kutuunga mkono kwamba umri wa meli uwe miaka kumi na tano. Mhe. Subeit Khamis Faki nakuomba uweze kubadilisha msimamo wako na kuweza kuridhia hali hii.

Mimi najua kwamba unatetea maslahi lakini mazuri zaidi ni yale ya wananchi wengi ambao naamini kwamba utatufahamu. Suala la Bima limeingizwa ni muhimu na ndio maana tukaliingiza katika mswada huu. Tunakushukuru kwa mchango wako.

Mhe. Fatma Mohamed Said tunakushukuru kwa michango yako ingawa ulizungumza kwa ufupi lakini yote uliyoyazungumza tumeyafahamu, tunakuomba sana utuunge mkono ili mambo yetu yaende mazuri. Kifungu kama ulivyosema cha 464 tumekitaja kwamba mtu ambaye adhabu yake haikutajwa ikiwa faini hakuwahi kulipa basi moja kwa moja kifungu cha 464 (3) kinamthibitishia adhabu ya kufungwa jela chini ya miezi mitatu au si zaidi ya miaka mitatu.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali tunakushukuru kwa mchango wako isipokuwa ulikuwa ukichanganya tu baina ya umri na kuwepo kwa meli. Kama nilivyofafanua pale mwanzo, meli hizi ziliopo zinaendelea kuwepo na kanuni zake zitatungiwa pale hali itakayokwenda na kuonekana hali yao inayokwenda. Zile zinazokwenda vizuri zitaendelea kwenda na zile zinazodorora zitafika wakati wataambiwa watusamehe nenda kauze *scraper* yako.

Lakini hakuna mfanyabiashara yeyote au mwekezaji yeyote aliyependelewa wala ambaye ameekewa kiwango fulani na huyu hakuekewa. Hivi ni viwango vilivyoekwa kwa mujibu wa utaratibu na kila kitu.

Mhe. Dr. Mwinyihaji nakushukuru sana kwa kufafanua juu ya uokozi ambao ulitaja kwamba na vikosi na sehemu nyengine bado zinaendelea, sisi tutafuatilia kwa kina kwa sababu sisi ndio wenye mamlaka ya usafiri baharini kwamba hayo mambo kweli yanakwenda na tutafanya utafiti na wenzetu wanafanya nini katika vyombo hivi.

Kwa hivyo wakati wa bajeti Waheshimiwa Wajumbe ya mwaka huu, mimi nitakuja na maelezo mazuri namna gani uokozi ulipo na sisi tupo *position* gani. Kwa hivyo tupeni huo muda na mimi nizungumze na hao kwa sababu na mimi nahusika sana na uokozi kwa sababu meli tunazoziruhusu kwenda na kurudi, lazima ziweze kuwa na aina fulani ya sehemu ya uokozi, nakubaliana nayo.

Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa michango yako ya ufafanuzi na nafikiri Wajumbe wametufahamu. Kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano nawaomba sana Wajumbe watuunge mkono katika mswada wetu huu ili wananchi wetu waweze kwenda katika safari zao kwa salama na bila ya wasi wasi na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatufikisha.
Kwa hayo machache nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba niko tayari sasa kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe hivi sasa. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2012

SEHEMU YA KWANZA

Masharti ya Awali

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika

Kifungu 2 Kusomwa

SEHEMU YA PILI

Marekebisho

Kifungu 3 Marekebisho ya kifungu cha 2

Kifungu 4 Marekebisho ya Kifungu cha 3

Kifungu 5 Marekebisho ya Kifungu cha 6 pamoja na marekebisho yake

Kifungu 6 Marekebisho ya Kifungu cha 7

Kifungu 7 Marekebisho ya Kifungu cha 8

Kifungu 8 Marekebisho ya Kifungu cha 9

Kifungu 9 Kuongezwa kwa Kifungu Kipya cha 10(a) pamoja na marekebisho yake

Kifungu 10 Kurekebishwa kwa Kifungu cha 11

Kifungu 11

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na kwa sababu ndio kwanza nasimama naomba nitumie fursa hii kwanza kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa usikivu wake na kukubali marekebisho mengi ambayo tumeyapendekeza kufanya katika mswada huu, likiwemo lile la kufuta neno "*SUMATRA*". Ni imani yangu kwamba yale mambo yaliyojitokeza mwaka jana kwamba tunafanya marekebisho, lakini baadae miswada ikijakutoka inakuwa inaachwa kama mwanzo, basi hayatojitokeza tena *Inshaallah* katika mwaka huu na miaka inayokuja.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 11 nilikuwa naomba marekebisho madogo tu, nilitanabahisha mapema wakati ninachangia kuhusu vifungu hivi ambavyo vilikuwa viko katika ile karatasi ya ziada ambavyo havikuwemo katika mswada, sasa nashukuru vimeletwa,

lakini katika lugha tu kidogo. Kijifungu cha (2) kinachoongezwa yaani kifungu cha (b) pale kinasema, kuingizwa kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo. Sasa kuna maneno pale mwisho naona Kiswahili kidogo hakijakaa sawa na kwa sababu lugha ya Kiswahili inayotumika Baraza la Wawakilishi, ndiyo itakayoeleza dhamira ya watunga sheria.

Nini ninachokusudia Mhe. Mwenyekiti, kinasomeka hivi;

Kijifungu kipya cha (2)

> "Mtaji ulioekezwa na Kampuni ya Meli ambayo itasajiliwa kwa ajili ya kuendesha shughuli za kibiashara ya usafiri Zanzibar, isipungue chini ya shilingi bilioni 3".

Sasa Kiswahili isipunguwe chini ya shilingi hiyo hakuna Mhe. Mwenyekiti, ama iandikwe isipunguwe shilingi bilioni 3, au isiwe chini ya bilioni 3. Lakini haiwezekani isipunguwe chini, itakuwa tunafanya maneno mawili ambayo maana yake ni moja. Kwa hivyo, mimi ningeomba isomeke vizuri kwamba isipungue shilingi bilioni 3, itakuwa imekidhi haja. Naomba ifanywe marekebisho hayo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tunakubali litoke neno "chini", libakie isipungue shilingi bilioni 3.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, tuendelee ahsante.

Kifungu 11 Marekebisho ya Kifungu cha 12 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri, pamoja na kutueleza kwamba tukubali umri huu wa kuwa meli ikifika umri wa miaka 15 isiweze kusajiliwa tena. Sijui ndipo hapa kifungu cha 12 chini (a) 17(a)?

Mhe. Mwenyekiti: Bado hatujafika hapo.

Kifungu 12 Marekebisho ya Kifungu cha 15
Kifungu 13

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilimuelewa sana Mhe. Waziri alipokuwa anatoa hoja kuhusu umri wa meli na alisisitiza kwamba kwa kila aliyekuwa makini ni lazima atetee uhai wa Wazanzibari na mimi naunga mkono katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana Wawakilishi hawa wakaishauri serikali mwaka jana kwamba ni lazima wanunue meli mpya, kwa kujali maslahi ya Wazanzibari wote. Lakini hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, nilisema jana kwamba ukiangalia sheria mama, kifungu cha 16 na 17, vilieleza wazi ni vipi meli itakubalika kufanya kazi hapa, kwa maana kwamba kuna masharti ndani ya sheria mama yaliyoelezwa wazi wazi kwamba meli itafanya kazi ikiwa masharti yafuatayo yatasimamiwa. Nilieleza jana kwamba hata Meli ya *Titanic* ya Uingereza, ilizama siku ya kwanza tu ya kufanya kazi, kwa sababu walikataa masharti ya kitaalamu ya meli ile. Kwa hivyo, ndio nikasema kwamba umri sio hoja.

Mhe. Mwenyekiti, unaweza kuwa na meli mpya lakini mukakiuka masharti ya meli ile, basi siku hiyo hiyo ikazama. Inawezekana kukawa na meli kongwe lakini ukafuata taratibu na ikapasishwa na meli ikaenda. Ndio nikasema kwamba umri sio hoja, ila masharti ya sheria yangesimamiwa kama ilivyo sheria mama, basi kungekuwa hakuna tatizo. Hizo meli ambazo zimezama hapa, wala sio kwa umri ni kwamba watendaji na serikali haikusimamia masharti ya meli yenyewe. Ni nani aliyemruhusu aongeze meli kwa urefu kama sio watendaji waliovunja masharti. Kwa hivyo, umri sio hoja, bado nasisitiza kwamba tuwawezeshe Wazanzibari wengi maskini, tuwaongezee umri angalau miaka 20 badala ya 15.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilieleza kwamba hili suala la umri linatokana na uzoefu uliopatikana katika kipindi hiki ambacho biashara iliruhusiwa, halikuja wenyewe. Hawa wafanyabiashara wetu walivyopewa ile nafasi ya kwenda kufanya ile biashara, wao wenyewe ndio waliokuwa wakienda kuchukua vyombo vichakavu, ndio suala lililojitokeza. Haidhuru katika hiyo aliyosema kuwa umri sio hoja, lakini wenyewe wafanyabiashara ndio waliokwenda kuchukua vyombo vichakavu ambavyo vina umri mkubwa. Kwa hivyo, ikaonekana kwamba hapana. Sasa kutokana na uzoefu uliopo hapa, ukiachia hivi hivi hali itakwenda vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikatoa mfano Skagit amekwenda kuchukua chombo miaka 23 ambapo ndio karibu na ku-*expire*. Kwa hivyo, suala la umri pale lilikuja kwa uzoefu uliopo hapa wa hao hao wafanyabiashara wetu. Tukaweka miaka 15 na meli itakapoundwa mpaka ikafikia miaka 15 imeshatumika, ndio nikatoa mfano kwamba serikali inafanya umri wa sifuri, kwamba inachukua meli mpya. Lakini haikuweka kwamba kila mmoja aende akaagizie meli mpya, imewawekea miaka 15. Kwa hivyo ugumu uko wapi, mimi siujui uko wapi ugumu, kwa sababu vyombo vilivyopo vinaendelea na safari zake. Sasa mfanyabiashara atachagua mwenyewe. Hilo ndio jibu ambalo ninalitoa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kama umri ndio kigezo cha kuzama meli, basi ingezama mwanzo Mv. Maendeleo, Mv. Serengeti ingezama mwanzo na Mv. Mapinduzi pia ingezama mwanzo, kwa sababu ni meli kongwe sana. Lakini zimetunzwa, zimeshughulikiwa na zimelindwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mv. Maendeleo ni hivi sasa tu, lakini ilikuwa na *life jacket* nyingi, Mv. Maendeleo ilikuwa na *engine* nzima, Mv. Maendeleo ilikuwa ikifanya *service*. Zimelindwa, zimeshughulikiwa na zimesimamiwa sio tatizo la umri. Kwa hivyo, kifungu cha 16 na 17 cha sheria mama, vimetoa masharti ya kutosha kwamba kama meli itafuata utaratibu huu, Msajili akaridhika kwa utaratibu huu, basi hiyo meli itaruhusiwa kufanya kazi na haikusema kwamba ni lazima miaka 3 au miaka 4. Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukaweka meli miaka 3 au miaka 4, lakini watendaji wakawa wazembe wakasababisha mauaji makubwa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tufuate sheria mama, sheria nambari 16 na 17 ambayo imeweka wazi kwamba Mhe. Waziri akisimamia, basi hapana matatizo yoyote yatakayotokezea na hata tukiweka siku moja ya meli, kama Waziri atakuwa Ofisini hafuatilii watendaji wake, siku moja ya meli itazama na watu wataumia. Sio tatizo la umri Mhe. Mwenyekiti, ni *commitment* ya usimamizi wa majukumu yetu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, napenda niseme kwamba hizo meli 2 alizosema kwamba sio umri, lakini Mv. Spice Islanders ni zaidi ya miaka 25 umri wake imezama, Skagit ni zaidi ya miaka 23 imezama. Sasa wakitetea huko kwamba hizi zipo, hizo zilizozama umri wake ni huo. Kwa hivyo, hakuna meli mpya ambayo hapa kwetu imezama na hiyo Titanic iliyozama wakati huo, ilikuwa ni masuala ambayo mbali mpaka leo huu ulimwengu unashuku. Kwa hivyo, hayakuwa ni masuala ya kawaida. Sisi tunatizama mazingira yetu na bahari yetu tuliyonayo.

Pia nilisema kwamba meli zetu tunazozichukua hapa ni meli zinazosafiri baharini, kwa hivyo, kile chuma chake ambacho kimeshakaa muda ndani ya bahari miaka hiyo inalipa na hiyo ndio imebainika kwamba watumiaji wetu hapa wenye vyombo, hawana matengenezo makubwa na ndio maana hivyo vyombo vikienda Pemba asubuhi basi jioni unaambiwa kimezima moto njiani. Kwa hivyo, ule uzoefu uliopo ndio uliofanya tuweke hivyo. Hata kiufundi, sisi tumepitia kwenye utafiti wa kiufundi, meli ambayo ina umri mkubwa gharama yake ya matengenezo ni kubwa mno, kiasi inawafanya hawa wenye meli wasipende kwenda *dry-dock* kuzitengeneza meli zao. Sasa sisi vile vile tuna-*protect* hiyo, kwamba tulete meli ambazo zitaweza kufanyiwa matengenezo. Kwa hivyo, tukiagiza meli kongwe sana zitakuwa hata huo uwezo wa wale wenyewe wamiliki, kuzifanyia matengenezo hawawezi. *(Makofi).*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, namuelewa sana Mhe. Waziri na sitaki nibishane naye, lakini unapotaja tatizo la chuma, ukataja pia tatizo la matengenezo, ndio pale ambapo watendaji hawasimamii majukumu yao. Kwa nini utoe kibali wakati hakuna matengenezo, ndio hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kwamba hata hiyo mpya kama hujakagua chuma, hujakagua matengenezo yale basi maana yake hakuna usimamizi na sheria mama imeeleza wazi kwamba kama kuna usimamizi hakuna tatizo. Bado hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, sio tatizo la umri. Mhe. Waziri amekiri hapa kwamba imejulikana kuwa walikuwa hawafanyi *service*, wanatubeba tu kwa sababu ya mshahara na mapato. Kwa hivyo, hapa nalenga kwenye wizara katika usimamizi, ndio nikasema kwamba kifungu mama na hiyo kanuni yake asisitize kwamba kifungu nambari 16, kanuni iseme wazi kwamba kuwe na matengenezo na kufanya *service* angalau kila mwezi au miezi miwili. Hiyo ndio hoja ya msingi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hoja yake nimeifahamu. Sasa labda tumuulize swali, kama umri sio tatizo kwa nini wao wakapendekeza 20, wasiseme ije tu, inaonesha na wao wanaona umri ni tatizo. Kwa hivyo

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe Waziri alisema kwa nini nyinyi mkapendekeza miaka 20. Hoja hapa inakuja meli haikuzama kwa kutoboka, meli imezama kwa kupakia abiria zaidi ya uwezo wake. Leo hata hizo meli mpya, si tunazo meli mpya. Leo meli yenye uwezo wa kupakia abiria 250, kesho hebu tukapakie abiria 1,000 pale tutizame itarudi. Sisi hapa kitu tunachokisema, hoja ambayo ilitolewa na serikali bado kwetu sisi haijawa hoja ya msingi. Ndio maana tukarudia, sisi tunarudi mpaka kwenye Kamati aliyoiunda Mhe. Rais, ndio mapendekezo yake, sisi ndio tumeyachukulia yale na kama meli zitashughulikiwa vizuri na abiria watapakiwa kama kawaida, Mhe. Mwenyekiti, hilo halina tatizo. Sasa kama alikuwa

anataka ufafanuzi kwa hilo, basi ufafanuzi ndio huo. Hoja ni kwamba meli zinapakia kupita kiasi.

Kwa mfano, hata meli iletwe siku hiyo hiyo ndio imetengenezwa, kwa mfano hii ya serikali, mfano tunakuja kuambiwa idadi ya abiria ni 1,000 na tani ni 1,000 basi wacha tuibebeshe tani 4,000 na abiria 4,000, basi haifiki hata Chumbe itakuwa imeshazama. Kwa hivyo, mimi nadhani usimamizi ni kitu muhimu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichangia.

Mhe. Mwenyekiti: Hii hatujamaliza bado.

Mhe. Abdalla Juma Abadalla: Haijesha.

Mhe. Mwenyekiti: Unataka kutoa taarifa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Hapana. Unajua Mhe. Hamza kazungumza hoja kwa mawazo yangu nahisi ni tofauti kidogo. Sasa nilitaka nitoe ufafanuzi zaidi kabla Waziri hajaanza kujibu.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani wacha tumalize halafu tutakuja huko.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Haya.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri amenifahamu. Jana tulikuwa tunazungumza hapa, sasa akiniambia kwa nini nitaje miaka 20. Basi pia nilitaka kujua kwa nini yeye asiseme mwaka mmoja. Maana yake ni muda tu. Hoja ni kwamba atukubalie tuongeze umri ili kutoa uwanja kwa wale wafanyabiashara wadogo wadogo, chini ya masharti ya serikali ya sheria. Maana sio tuwape ruhusa tu wafanye, lakini chini ya usimamizi wa sheria, ambapo sheria mama tayari imeeleza wazi wazi, kwamba Waziri kama atakaa ofisini akawasimamia watendaji wake, basi matatizo yataondoka hapa. Lakini kama meli itakuja leo kutoka ndani ya uzi wa hariri wakajisahau kuwasimamia, yatakuja kuliko haya.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri atakubali kuwa tuongeze umri wa meli kusajiliwa na baada ya hapo sasa awasimamie watendaji wake wawajibike, sio tukae ofisini halafu tutegemee kwamba meli haitazama. Itazama meli na ndege itaanguka kama hatuwajibiki.

Mhe. Mwenyekiti: Labda nikuhoji Mhe. Mjumbe, una msimamo wa miaka mingapi wewe?

Mhe. Hija Hassan Hija: Angalau miaka 18. Mimi nipunguze na yeye apunguze tukubaliane miaka 18 angalau.

Mhe. Mwenyekiti: Yaani utoke miaka 15 mpaka 18.

Mhe. Hija Hassan Hija: Angalau.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, sisi tulivyofanya ni miaka 15. Sasa maamuzi yako kwako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa labda uamuzi wa Baraza zima, tutumie kura. Naomba tusikilizane. Imekuja hoja ya miaka 18 kwa miaka 15.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwa sababu suala la kura ni hatua ya mwisho katika chombo kama hiki. Najua siku hizi mara nyingi tumejenga ushabiki huo, jambo kidogo tunakwenda kwenye kura sio utaratibu mzuri kwa chombo kama hiki ambacho msingi wake unatakiwa ujengwe kwa *consensus* zaidi, yaani kwa maelewano baina ya serikali na *backbenchers.*

Sasa sipingi maamuzi yako, lakini nimeamua kusimama kuhusu utaratibu kwa sababu ulipotaja kifungu hiki tulinyanyuka Wajumbe nafikiri kama watatu na tulikuwa na hoja tofauti nyengine kuhusu kifungu hicho hicho. Sasa nakhofia isije ikawa tukakipigia kura kwa hatua moja halafu zile hoja nyengine ambazo tunataka kuzitoa pia zikawa hazipati nafasi, ndio maana nikasema suala la kura ni hatua ya mwisho kabisa. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani Mhe. Mwenyekiti, ulikuwa utumie busara zako utuamulie, utakavyoamua mimi naheshimu kiti siku zote kama kawaida yangu kwamba tuzungumze zile hoja zote kwanza na ufahamu wetu kutokana na majumuisho ya Waziri, kwa sababu yote yanaingia katika *hansard*, hayo yatakuwa ni sehemu ya maamuzi ya chombo hiki, halafu tena mwisho uje uamue tuje tupige kura, naomba hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa. Muafaka uamuzi wako na ushauri wako, tunaomba walionyanyuka kutoa hoja nyengine wasimame ili tuwape nafasi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kama Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hili suala nilianza kusema mapema nilipochangia kama tunawaita wadau kwa sababu ya kupokea maoni yao na wao ili kuangalia lile zuri walilolileta tulifanyie kazi. Sasa ikiwa yote ambayo wanayaleta mazuri mengine tunayaacha basi itakuwa hatuna haja ya kuwaita, kwa sababu wenzetu tuliwaita na wakatoa maoni yao na wakasema kwamba jamani tunaomba iongezwe miaka 15 ni michache.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wasi wasi wetu badala ya kuwa tunatengeneza mambo mazuri tukaja kupata mabaya zaidi, kwa sababu baada ya kuwazuia wafanyabiashara wakawa hawaleti vyombo na uwezo tunao, itakuja kuwa chombo kilichopo ni kimoja au viwili tuving'ang'anie hivyo hivyo, halafu bei ikapandishwa maradufu, badala ya kuwapunguzia matatizo wananchi tutakuja kuwaongezea matatizo. Ni lazima tuangalie tunapopitisha sheria zetu, tumo humu kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu, hatumo humu kwa ajili ya maslahi yetu sisi wenyewe. Kwa hivyo, tuangalie tunapopitisha sheria, je hii sheria tunayoipitisha mwananchi hatumuonei. Kwa sababu baada ya kupunguza vyombo vikawa ni vichache basi mtu atapandisha bei anayoitaka yeye mwenyewe, basi wananchi itakuwa tunawapelekea usumbufu.

Naomba Mhe. Waziri miaka 18 iliyoombwa sio mingi ya kuwa tugombane tupige kura na kadhalika. Miaka 18 aliyosema Mhe. Hija Hassan, ile tume ya Rais ilipendekeza miaka 20 na sisi tukaona kwamba Tume ile ya Rais iliyoteuliwa ni tume ya kitaalamu, ilifanya kazi zake kitaalamu pesa nyingi za serikali zilikwenda kwa ajili ya wataalamu wale. Leo wameshatoa mapendekezo yao lakini hatuyafanyii kazi. Kwa hivyo, hizi tume zinaundwa kufanya kazi lakini hatuzithamini na wale ni wataalamu waliteuliwa na Rais, kwa kuwaona ni wataalamu wanaojiweza. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba ikiwa kuna uwezekano Mhe. Waziri akubali tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja yako?

Mhe. Subeit Khamis Faki: Hoja yangu ni kwamba namuomba Mhe. Waziri miaka 15 ni michache aongeze angalau hiyo miaka 18.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu niliunga mkono miaka 15 na nilitoa sababu. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, tumejifunza mambo mengi ambayo yametokea huko nyuma. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tusifanye utashi wa mtu kwa matakwa yake binafsi, tukafanya utashi tukayumba katika suala hili, kwa kweli tuliangalie. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana Wajumbe wenzangu wa Baraza, tukubali hiyo miaka 15, kwa sababu hicho chombo huko kinakotoka hatukijui kimetumika miaka mingapi, naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja tatu zimemaliza, kuna masuala mawili. Serikali imeleta miaka 15 pamoja na Mhe. Asha Bakari Makame na Wajumbe wawili wametaka miaka 18 kutoka 20. Sasa tusikilize maoni ya serikali kama imeridhika au haikuridhika tuamue Baraza zima kwa ujumla kwa kutumia kura. Hoja tatu tumeshazisikia zote, bado wana misimamo tofauti hawajakubaliana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hoja zimetolewa, sababu zimetolewa mbali mbali, lakini tunachosema kwa upande wa serikali ni kwamba mpaka kufikia hili limezingatia taarifa mbali mbali za kitaalamu na wadau walioitwa mimi nina wasi wasi, sijui kama ni wadau pamoja na wafiwa kwenye meli ama ni wenye meli tu, sina hakika. Lakini naamini wangeitwa na wadau wafiwa wa kwenye meli wangeungana na huu msimamo wa serikali.

Lakini katika mapendekezo ambayo yalitolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano, ambayo ilikutana baada ya ajali ya meli, moja katika mapendekezo au maelekezo yaliyotoka ni kwamba ni vizuri ku-*harmonize* muda wa umri wa meli baina ya hizi bandari mbili ambazo meli zetu zinafanya safari, baina ya wenzetu Bara na sisi ni vizuri tuka-*harmonize*. Wenzetu umri wa meli ni miaka 15 ndipo inapoanza kusajiliwa, *first registration* na sisi ni hivyo hivyo. Kwa hivyo, ndio msingi mkubwa kwa kweli serikali ikaja na mapendekezo hayo.

Baada ya kuzingatia hoja za kitaalamu, lakini na maelekezo na mapendekezo ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa, ndio hoja na ndio msingi mkubwa wa mapendekezo haya ya serikali, pamoja na hoja nyengine ambazo zilitolewa kuhusiana na tatizo la usimamizi, ku-*monitor* chombo ambacho kidogo umri wake ni mpya na chombo ambacho umri wake ni mkubwa hata gharama za kukifanyia ukaguzi basi ni kubwa zaidi. Kwa hivyo, serikali

imezingatia maelezo yote hayo pamoja na yale ambayo yalitolewa na Waheshimiwa Wawakilishi humu ndani ya Baraza.

Kwa hivyo, tunasema kwamba sio kwamba uamuzi uliotolewa ni kwa sababu kuna mtu ana meli yake, anaona kwamba pengine keshapata gharama ya kuisajili. Kama kuna mtu wa namna hiyo anataka kuja kusajili na awahi kabla sheria haijatiwa saini.. *(Makofi)*

Lakini nadhani kilichotolewa na serikali ni kwa kuzingatia kwamba kutokana na yaliyotufika basi tunatengeneza kanuni mpya na kwa kuzingatia maelekezo pamoja na mapendekezo ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa ndiyo iliyotoa mapendekezo haya ya ku-*harmonize* kufikia miaka 15. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji mumekubali maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia maamuzi iliyoleta serikali.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, uliposema kwamba hoja tatu zimekwisha nilivyotafsiri mimi ni kwamba kusema suala lile la umri wa meli limekwisha.

Kwa hivyo, kabla ya kupitisha hichi kifungu nataka kuitanabahisha Kamati ya Kutunga Sheria na Baraza la Mawaziri ndio limo, ili lipate kuelewa vizuri zaidi na mimi simo kwenye umri nafikiri tumeshaelewana na nashukuru kama nilivyosema haipendezi kila wakati kuonekana tunapiga kura kwa kila jambo dogo. *(Makofi)*

Namshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba amefanikiwa kutumia busara zake kuliwezesha Baraza kwa maamuzi haya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wakati alipokuwa akifanya majumuisho, katika ile hamu yake ya kutaka kuwashawishi Wajumbe wakubali alitamka neno mimi kidogo limenipa mashaka. Sasa hotuba ile ya majumuisho ni sehemu ya kumbukumbu za kikao hichi na kesho kutwa tutakuja kutafsiri dhamira ya yale ambayo tunayoyapitisha.

Kwa hivyo, wakati alipokuwa akitushawishi alitamka kwamba kinachozungumzwa kwenye miaka 15 ni kusajili, lakini leseni ni suala jengine na kifungu kilivyo ndani ya mswada hakisomeki hivyo. Sasa maelezo yake katika *hansard* yamekaa vile nilivyoyanukuu hapa, lakini kifungu kinasema Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kifungu cha 12 cha sheria mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 17A baada ya kifungu cha 17 kinaeleza hivi:-

"17A (1) Hakuna meli ambayo itazidi umri wa miaka 15 tokea tarehe ya kutumika kwake, itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa ajili ya kuchukua abiria na mizigo Zanzibar".

Kwa maana hiyo, nataka nijue hii dhamira ya watunga sheria wakati tunapitisha hichi kifungu, kwa sababu nakhofia kama tafsiri hiyo basi mimi naiafiki. Kwa kweli moja katika *concern* yangu ni kwamba mwaka jana au mwaka huu tunaoendelea nao serikali kupitia Baraza hili imetenga fedha kwa ajili ya kununua meli mpya.

Sasa najiuliza na hiyo ikiwa kifungu hichi tutakipitisha hivi baada ya miaka 15 maana yake nayo ama tuuze au tufanye *scraper*, lakini haitaweza kupata leseni tena kwa sababu itakuwa tayari imeshatimiza miaka 15 kikibakia hivi kama tunavyokipitisha hivi sasa. Mhe. Mwenyekiti, laa ikiwa tafsiri ndio ile aliyoisoma Mhe. Waziri katika majumuisho yake basi itabidi ukituhoji tuseme pamoja na marekebisho haya maneno au kupewa leseni yaondoka.

Kwa hiyo, tunataka tuwekewe *clear* na Mhe. Waziri kwa sababu mwenye mswada ni Mhe. Waziri kwa niaba ya serikali. Je, ni kusajili na kupewa leseni ama ni kusajili peke yake, ili tujue kabisa hapa nini tunachokipitisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hapo ni kusajili na kupewa leseni na sio hizi zinazopewa leseni kila mwaka na wala hazihusiki hizi zinazopewa leseni kila mwaka ni ile ya mwanzo ikisajiliwa itapewa na leseni, katika ya kiingereza tuiangalie kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunataka kupitisha nadhani tustahamili bado vifungu vichache tu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu kifungu 17A (1) kupitia mswada wa Kiingereza.

Kifungu cha 17A (1) kinaeleza hivi:-

"*No shipping has more than fifteen year of age from the date of its commission shall come for registration or live or license for the purpose of carrying passengers in the Zanzibar*".

Sasa tafsiri yake mimi nikisoma kwa Kiingereza ambacho nilichosomea hapa Lumumba haina tofauti na ilivyoandikwa kwa Kiswahili ni kusajiliwa au kupewa leseni.

Kwa kweli hii ni muhimu sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hapa nilisema kwamba tunaweka *records* za dhamira ikitokezea tofauti yoyote tukienda Mahakamani itakwenda kuangaliwa *hansard* kwa Wawakilishi wakati walipokuwa wakitunga sheria hii walikuwa na dhamira gani.

Kwa hivyo, nasema tuelewane hivyo tu, kwa sababu khofu yangu tusije tukatunga sheria kwa sababu hivi sasa tunataka kitu fulani na halafu kesho kutwa ikaja meli nyengine na tukataka tufanye marekebisho. Mhe. Mwenyekiti, kama tunatunga hivi basi tuelewane tu kwamba hata

hiyo tunayoinunua serikali baada ya mwaka huu wa 2013 baada ya miaka 15 kama nilivyosema itabidi ama tuuze au tukafanye *scraper*.

Lakini ikibakia neno au hapa maana yake ni yote mawili inasimama peke yake ni tofauti na kusema na. Kwa mfano, ukisema itakayosajiliwa na kupewa leseni yanakwenda pamoja, lakini ukisema itakayosajiliwa au kupewa leseni yanasimama kila moja peke yake, yaani kusajiliwa mbali na kupewa leseni mbali.

Sasa kama ni hivyo, basi dhamira ikae vizuri na kwa bahati nzuri tunae Mhe. Mwanasheria Mkuu ambaye ni mzoefu katika masuala ya uandishi wa sheria tusaidiane, ili tujue kwa sababu kama tumepitisha hivi maana yake inasema hata ikija meli mpya leo, basi baada ya kumi 15 hatuwezi tena kuipa leseni seuze kuisajili hata kuipa leseni.

Kwa hiyo, hili nataka likae sawa ili tuelewane tunapitisha hii na wala sina tatizo lolote, isipokuwa nataka Baraza liwe *clear* katika maamuzi yake. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa macho yake yenye weledi na makali na tafakari yake iliyoona mbali. *(Makofi)*

Pili niseme nikubaliane na hoja yake aliyoitoa kwamba kisheria kama tutatumia neno au maana yake ni kwamba tunavyo vitu viwili tofauti, kama tutatumia na maana yake tunakusudia kwamba hiyo ambayo itasajiliwa wakati huo ndio itakayohusika na suala hili.

Kwa hivyo, mimi nakubaliana na ushauri wake kwamba ni vizuri kusema kusajiliwa na kupewa leseni. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwenye kifungu hichi 17(3) naomba kunukuu.

> Kifungu cha 17A (3) kinaeleza hivi:-
>
> > “Hakuna meli itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa madhumuni ya kuchukua abiria ndani ya Zanzibar ikiwa meli hiyo imebadilishwa kutoka katika asili ya utengenezaji wake”.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kidogo hapa, kwamba hivi sasa kuna meli tokea asili yake inapakia abiria na imepewa leseni ya kupakia mizigo tu. Je, utakuwa tayari kama tokea asili yake inakotoka kupatia abiria leseni hiyo itatoka.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, hoja umeifahamu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, bora airudie tena.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, rejea tena kwa pole pole.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 17A (3) naomba ninukuu.

Kifungu cha 17A (3) kinaeleza hivi:-

> "Hakuna meli itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa madhumuni ya kuchukua abiria ndani ya Zanzibar ikiwa meli hiyo imebadilishwa kutoka katika asili ya utengenezaji wake".

Mhe. Waziri sijui ameshafahamu mpaka hapo, kuna meli tokea asili yake inakotoka inapakia abiria, lakini baadaye kutokea ghasia hizi zilizotokea imezuiliwa na kupewa kibali cha kupakia mizigo tu. Je, kuna maamuzi gani hapa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna majibu mawili, jibu la mwanzo ni kwamba sheria inawataka wamiliki wa vyombo walete zile *certificates* zao, kwa hiyo ndani ya *certificate* itaonesha kwamba ilikuwa imetengenezwa kwa ajili ya abiria au laa.

Pili ni kwamba hali iliyo ile meli inaweza ikawafanya wakaguzi wakaifelisha kuchukua abiria hata kama hapo mwanzo ilikuwa ikichukua abiria. Kwa maana hiyo, inategemea sasa mmiliki mwenyewe aende kwenye mamlaka na akaombe ukaguzi, ili ikaguliwe yote mambo mawili. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwa muwazi kweli na wala hakuna tatizo tumeshakubaliana tuendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Kifungu 13	Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 17A pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 14	Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 18A pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 15	Marekebisho ya kifungu cha 28.
Kifungu 16	Marekebisho ya kifungu cha 29.
Kifungu 17	Marekebisho ya kifungu cha 30.
Kifungu 18	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na hapa nataka kuweka kumbukumbu vizuri tu, kwamba nilipokuwa nikichangia nilivijumuisha pamoja vifungu vile cha 14 ambacho tayari tumeshakipita kuhusu kutunga kanuni na nikakijumuisha na kifungu hichi cha 18 kwa sababu lugha iliyotumika ni sawa sawa.

Sasa Mhe. Waziri alipokuwa akifanya majumuisho alitujibu kwa ufasaha kuhusu kile cha 14 kwa sababu wachangiaji wengi ndio walikigusa. Kwa hivyo, naomba kuweka *records* sawa tu na hapa vile vile kama nimemfahamu atanithibitishia kama ni sahihi ili tuendelee, kwamba na hapa tutarekebisha kwenye hichi kijifungu cha 4 kwa kuandika Waziri pia atatunga sio kwamba anaweza kutunga na tukishaelewana hivyo basi sina matatizo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naungana naye na nakubaliana na marekebisho hayo.

Kifungu 18 Marekebisho ya kifungu cha 43 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 19 Marekebisho ya kifungu cha 55.
Kifungu 20 Marekebisho ya kifungu cha 57.
Kifungu 21 Marekebisho ya kifungu cha 58.
Kifungu 22 Marekebisho ya kifungu cha 61.
Kifungu 23 Marekebisho ya kifungu cha 85.
Kifungu 24 Marekebisho ya kifungu cha 92.
Kifungu 25 Marekebisho ya kifungu cha 93 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 26 Marekebisho ya kifungu cha 94.
Kifungu 27 Marekebisho ya kifungu cha 95 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 28 Marekebisho ya kifungu cha 97 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 29 Marekebisho ya kifungu cha 99.
Kifungu 30 Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 99A.
Kifungu 31 Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 122A.
Kifungu 32 Kufutwa kwa vifungu vya 135,136 na majaduweli.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 2012

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 2012 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu juu ya kusomwa kwa mara ya tatu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa tuliyofanya tangu asubuhi pamoja na ushirikiano mkubwa mlionipa hadi kumaliza mswada wetu kwa salama.

Vile vile naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa kazi kubwa aliyoifanya, hivyo tunaomba sasa akatekeleze yale yote ambayo tumekubaliana.

Kwa kuwa shughuli zetu za leo zimemaliza naomba nitoe tangazo halafu tuakhirishe kikao chetu.

Tangazo la kwanza ni kwamba zile Kamati ambazo zina semina kesho shamba, basi lipo nje hapo kwa wale ambao wameshajiandaa wataingia kwenye gari na kwenda shamba kwa ajili ya semina kesho asubuhi.

Baada ya maelezo hayo, naakhirisha kikao chetu hichi hadi siku ya Jumatatu siku tarehe 21 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:15 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 21/01/2013 saa 3:00 za asubuhi)